

# **JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



## **BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**

### **TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2022 HADI JANUARI 2023**

[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]

Ofisi ya Bunge,  
Mtaa wa Makole,  
S.L.P. 941,  
41105 **DODOMA.**

Februari 2023

# **YALIYOMO**

<b>YALIYOMO .....</b>	i
<b>IKISIRI.....</b>	iii
<b>SEHEMU YA KWANZA .....</b>	1
<b>1.0 UTANGULIZI.....</b>	1
1.1 Maelezo ya Jumla .....	1
1.2 Muundo wa Taarifa .....	2
1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati.....	3
1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....	3
1.3.2 Kanuni za Kudumu za Bunge .....	6
1.3.3 Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 .....	7
1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika .....	9
<b>SEHEMU YA PILI .....</b>	11
<b>2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI.....</b>	11
2.1 Maelezo ya Jumla .....	11
2.1.1 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo .....	11
2.1.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni .....	13
2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo.....	14
2.2.1 Hatua ya Kutotekeleza Maazimio ya Bunge .....	17
2.2.2 Hatua ya kutojamiliwa kwa Rasimu ya Marekebisho.....	19
2.2.3 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho Kusubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki.....	22
2.2.4 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki .....	24
2.2.5 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali .....	25
2.2.6 Hatua ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali .....	27
2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo ambazo ziliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa .....	30
2.3.1 Maelezo ya Jumla.....	30
2.3.2 Mchanganuo wa Dosari zilizobainika .....	31
2.3.3 Dosari ya Kukinzana na Masharti ya Katiba .....	32

2.3.4 Dosari ya Kukinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za nchi.....	34
2.3.5 Dosari ya Kutoendana na Misingi Bora ya Uandishi wa Sheria	35
2.3.6 Dosari ya Kukosa Uhalsia.....	37
2.3.7 Dosari za Uandishi wa Majedwali .....	39
2.4 Majumuisho kuhusu yatokanayo na Shughuli zilizoteklezwa.....	40
<b>SEHEMU YA TATU .....</b>	<b>44</b>
<b>3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>44</b>
3.1 Maelezo ya Jumla .....	44
3.1.1 Sheria Ndogo Kukinzana na Masharti ya Katiba .....	45
3.1.2 Sheria Ndogo Kukinzana na Masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi .....	45
3.1.3 Sheria Ndogo kutozingatia Misingi ya Uandishi bora wa Sheria	45
3.1.4 Sheria Ndogo kuwa na Masharti yasiyozingatia Uhalsia .....	46
3.1.5 Sheria Ndogo kukosa Usahihi na Ufasaha katika Uandishi wa Majedwali.....	46
3.1.6 Uchelewaji katika Kutekeleza Maazimio yanayohusu Kurekebisha Sheria Ndogo .....	47
3.1.7 Kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge .....	47
3.2 Mapendekezo .....	49
3.2.1 Kukinzana na Masharti ya Katiba.....	49
3.2.2 Kukinzana na Masharti ya Sheria inayotoa Mamlaka ya Kutungwa kwa Sheria Ndogo au Sheria nyingine za Nchi.....	50
3.2.3 Kutozingatia Misingi ya Uandishi Bora wa Sheria .....	50
3.2.4 Masharti Yasiyo na Uhalsia.....	51
3.2.5 Dosari ya Uandishi wa Majedwali .....	51
3.2.6 Uchelewaji katika Kutekeleza Maazimio ya Kurekebisha Sheria Ndogo.....	52
3.2.7 Kutokutekelezwa kwa Maazimio .....	52
<b>SEHEMU YA NNE .....</b>	<b>54</b>
<b>4.0 HITIMISHO .....</b>	<b>54</b>
<b>4.1 Shukrani .....</b>	<b>54</b>
<b>4.2 Hoja .....</b>	<b>57</b>

## **IKISIRI**

Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 (Kanuni za Bunge). Madhumuni yake ni kuliwezesha Bunge kuijadili na hatimaye kuamua kutokana na mapendelekezo yanayotolewa. Ili kufanikisha hilo, Taarifa imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambapo, Sehemu ya Kwanza ni maelezo ya jumla inayofuatiwa na Sehemu Kuu Tatu na Sehemu ya mwisho inahitimisha. Sehemu ya Kwanza inabainisha Muundo wa Taarifa, Msingi wa shughuli za Kamati kutoka kwenye Katiba, Kanuni za Bunge na Sheria yaTafsiri ya Sheria, Sura ya 1. Aidha, sehemu hiyo inabainisha njia na mbinu zilizotumika.

Sehemu ya Pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa na Kamati. Shughuli hizo ni uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo na Uchambuzi wa Sheria Ndogo. Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji yameonesha hatua kuu Sita zilizofikiwa katika utekelezaji wa mapendelekezo yaliyokwishatolewa Bungeni kuhusu Sheria Ndogo. Hatua hizo ni, Hatua ya kutokutekelezwa kwa Maazimio, Hatua ya kutokukamilika kwa Rasimu ya Marekebisho, Hatua ya Rasimu ya Marekebisho inayosubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki, Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki, Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali na Hatua ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Aidha, ufanuzi unatolewa kuhusu mapendelekezo ambayo hayajafanyiwa kazi.

Aidha, sehemu hii inaonesha matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo thelathini na moja zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa. Matokeo ya uchambuzi yanabainisha dosari katika Sheria Ndogo thelathini na moja katika namna kuu tano ambazo ni; kukinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kukinzana na Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, kutoendana na misingi ya uandishi, kuweka masharti yasiyo na uhalisia na makosa ya maudhui ya majedwali.

Sehemu ya Tatu ambayo ni msingi wa mapendekezo imebainisha maoni kuhusu mambo makuu saba (7). Mambo hayo ni: Sheria Ndogo kukinzana na masharti ya Katiba, Sheria Ndogo kukinzana na masharti ya Sheria mama na sheria nyingine za nchi, Kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia na kukosa usahihi na ufasaha katika uandishi wa majedwali. Mengine ni uchelewaji katika utekelezaji wa Maazimio yaliyokwishatolewa na Bunge kuhusu Sheria Ndogo, Kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge. Kwa muhtasari, sehemu hii inapendekeza Bunge likubali mapendekezo yafuatayo:-

- (a) Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi zifanyiwe marekebisho ndani ya siku sitini kwa ajili ya kutatua dosari hiyo;
- (b) Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zenyeye kukinzana na masharti ya Sheria mama na Sheria nyingine za nchi, zirekebishe Sheria Ndogo hizo ndani ya siku sitini ili kuondoa dosari hiyo;
- (c) Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zilizo kutwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, zirekebishe dosari hiyo ndani ya sitini kuanzia leo ili kuleta tija kwa watumiaji wa sheria hizo;
- (d) Mamlaka zinazotunga Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho ndani ya siku sitini kuanzia leo, ili kuendana na uhalisia na kurahisisha utekelezaji wake;
- (e) Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo na kubainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali zifanye marekebisho ndani ya siku sitini kuanzia leo;
- (f) Mamlaka zilizobainika kuchelewa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, zikamilishe mchakato wa marekebisho ndani ya siku thelathini kuanzia leo na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wake wakati wa vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2023; na
- (g) Mamlaka zilizobainika kutotekeliza maazimio ya Bunge zitekeleze Maazimio hayo ndani ya siku thelathini kuanzia leo na kuwasilisha

Taarifa za Utekelezaji wake wakati wa vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2023.

Sehemu ya Nne na ya mwisho ya Taarifa, inahitimisha na kutoa hoja kwamba Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendelekezo yaliyotolewa.

## **SEHEMU YA KWANZA**

### **1.0 UTANGULIZI**

#### **1.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako, Taarifa hii ya mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Januari 2023.Taarifa hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge inayoweka sharti kwa kila Kamati kuwasilisha Bungeni Taarifa ya mwaka ya shughuli zake, kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa Mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inaelezea kwa undani shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023 kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020. Kwa kuwa Kanuni hizo zimefafanua majukumu maalumu ya Kamati hii, naomba kubainisha kwamba, shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi kinachotolewa taarifa zilihusu udhibiti wa madaraka ya Bunge ya kutunga Sheria yanayokasimiwa kwa mamlaka ya utendaji.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi chote kinachotolewa taarifa, Kamati ya Sheria Ndogo imeendelea kutekeleza majukumu iliyopewa na Bunge katika eneo la udhibiti wa Sheria Ndogo. Leo naomba kulijulisha Bunge hili kuhusu shughuli zilizofanyika, yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli hizo na mapendekezo kuhusu nini Bunge lifanye au

lisifanye kutokana na mambo yaliyobainika kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Januari 2023.

## 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa madhumuni ya Taarifa hii ni kutoa fursa kwa Bunge kuijadili na hatimaye kupokea na kufanya kazi Mapendekezo ya Kamati, naomba kutanguliza maelezo ya awali kuhusu muundo wa Taarifa hii. Naamini kwa kufanya hivyo, mawanda (scope) na mtiririko utakuwa bayana na rahisi kufuatiliwa kwa ajili ya kujadili ili hatimaye Bunge liamue inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni hayo Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

- (a) Sehemu ya Kwanza ni ya utangulizi ambayo inatoa maelezo ya jumla kuhusu taarifa hii ili kujenga msingi mzuri wa majadiliano;
- (b) Sehemu ya Pili inahusu ufanuzi wa shughuli zilizotekelizwa na Kamati kwa kipindi kinachohusika ambayo inatoa maelezo kuhusu shughuli hizo, msingi wake na mambo yaliyobainika;
- (c) Sehemu ya Tatu inafanya majumuisho ya maoni kutokana na shughuli zilizotekelizwa. Lengo la sehemu hii ni kujenga msingi wa mapendekezo katika hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo inayojadiliwa Bungeni leo; na
- (d) Sehemu ya Nne na ya mwisho inahitimisha hoja ili kuliomba Bunge lifanye uamuza.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni ya kumbukumbu na rejea thabiti inayotokana na majadiliano ya hoja hii ya Kamati ya Sheria Ndogo, naomba Bunge lako liipokee na kuijadili Taarifa hii ikiwa na Viambatisho vyake viwili. **Kiambatisho Na. 1** (Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita, na Mkutano wa Saba). **Kiambatisho Na. 2** (Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa) linaloonesha Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa.

### 1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa shughuli zote za Kamati hii, ni utekelezaji wa madaraka ya Bunge yaliyofafanuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 (Katiba). Madaraka hayo yanahusu matumizi ya mamlaka ya Bunge katika utungaji wa Sheria kwa namna iliyoelezwa kwenye Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap.1*) na kuwekewa utaratibu katika Kanuni za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Ufafanuzi kuhusu madaraka ya Bunge kwenye eneo la utungaji wa sheria, masharti yanayopaswa kuzingatiwa katika utungaji wa sheria na utaratibu unaohitaji kufuatwa ni mambo yanayofaa kuongoza majadiliano kuhusu Taarifa hii. Ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:-

#### 1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, Katiba ya nchi ni hati kuu inayotoa idhini kwa mambo yote ya kisheria, kisiasa na kijamii katika Taifa. Kwa maana hiyo, Katiba ni msingi wa shughuli zilizotekelawa na Kamati kutokana na kueleza dhamira ya shughuli zote za umma nchini zinazotungiwa Sheria na kuweka mgawanyo wa madaraka. Aidha, Katiba imekuwa msingi wa shughuli za Kamati hii kwa kuonesha shabaha ya utungaji wa sheria na msingi wa Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka zingine.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4** ya Katiba inagawanya Shughuli zote za Mamlaka ya Nchi katika Jamhuri ya Muungano kwenye vyombo viwili vyenye mamlaka ya utendaji, vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki, na vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Katika mgawanyo huo, Bunge ni chombo cha kutunga sheria, Ibara hii pia ndio chimbuko la mantiki ya shughuli za Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli zote hizo zilizogawanywa kwa vyombo vyenye mamlaka tofauti nchini, zinafafanuliwa katika Ibara ya **Ibara ya 8(1)** ya Katiba. Kwa mujibu wa Ibara hiyo, msingi wa mamlaka yote ya nchi yaliyogawanywa kwenye vyombo mbalimbali ni wananchi na kwamba, Serikali inapata mamlaka na madaraka yake yote kutoka kwa wananchi. Aidha, Ibara ya 8 (1) (b) inasisitiza lengo la Serikali kuwa ni

ustawi wa wananchi. Kwa sababu hiyo, haitarajiwi mamlaka yoyote ya nchi itumike kwa namna inayovuruga au inayozuia ustawi wa wananchi. Hali hiyo imekuwa msingi mkuu wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuwa na mamlaka ya kutunga Sheria, chini ya Ibara ya 97 (5) ya Katiba, Bunge limepewa uwezo wa kukasimu kwa mtu yeyote au kwa idara yoyote ya Serikali, madaraka ya kuweka Kanuni za nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu ya kisheria Kanuni zozote zilizowekwa na mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali. Msingi wa kukasimu madaraka hayo ni kuwezesha utekelezaji wa Sheria zinazotungwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge linapotekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria za nchi huzingatia mambo yote muhimu katika utungaji wa Sheria hizo ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa. Kwa mantiki hiyo, ni matarajio kuwa Mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutunga Sheria na Bunge zitaakisi namna Bunge linavyotekeliza madaraka hayo. Matarajio hayo yanahusiana na maneno ya Profesa Kenneth Bailey, aliyewahi kuwa Wakili Mkuu wa Serikali ya Australia (1930) ambaye alisema:

## NANUKUU

*“It is for the Executive in making regulations to declare what parliament itself would*

*have laid down had its mind been directed to the precise circumstances”* **MWISHO WA KUNUKUU**

Kwa tafsiri ya Kiswahili, tunaweza kusema kwamba:-

“....katika utunzi wa kanuni zake, Serikali inatakiwa kutamka kile ambacho Bunge lenyewe lingeweza kutamka kama lingeelekeza nguvu zake katika utunzi wa kanuni hizo kwa kuzingatia mazingira yanayohusika....”

**Mhesimiwa Spika**, Bunge la Tanzania kama yalivyo Mabunge mengine duniani linapaswa kuendelea na utaratibu wa kufuatiliana na kwa kufanya hivyo litaweza kujiridhisha iwapo madaraka yaliyokasimiwa yametumika kwa namna ambavyo Bunge lingeweza kuyatumia. Ili kutimiza azma hiyo, uwezo wa kuunda Kamati za Bunge chini ya Ibara ya 96 ya Katiba umetumika kuunda Kamati ya Sheria Ndogo. Lengo la kuwa na Kamati hii ni kuwezesha utekelezaji bora wa madaraka ya Bunge, ikiwemo kufuatilia utungaji wa Sheria Ndogo nchini. Shabaha kubwa ni kuona kama madaraka ya kutunga Sheria Ndogo yanatumika kwa namna ambayo Bunge lisilingeliweza kuyatumia tofauti.

### **1.3.2 Kanuni za Kudumu za Bunge**

**Mhesimiwa Spika**, Kanuni za Bunge zinatoa mwongozo kuhusu utaratibu, desturi na uendeshaji wa shughuli zote zinazohusu utekelezaji wa madaraka ya

Bunge. Kwa Tanzania, Kanuni za Bunge ni zao la Ibara ya 89 ya Katiba ya Tanzania. Kanuni hizo zimezingatia masharti ya Ibara ya 96 (1) kwa kuanzisha Kamati za Kudumu za Bunge kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 137 ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 11 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimefafanua majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Majukumu hayo ni kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo hazikinzani na Katiba, Sheria inayoruhusu kutungwa kwa Sheria Ndogo zinazohusika na Sheria nyingine za nchi. Kukamilisha jukumu hilo Kamati hutekeleza shughuli mbalimbali kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge lakini kwa lengo la kufaulisha udhibiti wa Sheria Ndogo.

### **1.3.3 Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi mwingine wa Shughuli za Kamati ya Sheria Ndogo ni Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1. Masharti ya Sheria hii ni kitovu cha shughuli za Kamati zinazohusu Udhibiti wa Sheria Ndogo nchini. Imekuwa hivyo kwa sababu, Sheria hii ndiyo inayojumuisha masharti yanayohusu muundo, matumizi, tafsiri, utumikaji wa Sheria za nchi na mambo mengine yanayoendana na hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kutohana na madhumuni yake, Sheria ya Tafsiri ya Sheria imeweka masharti

yanayohitaji kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Sheria Ndogo. Masharti hayo yanayohusu misingi ya uandishi wa sheria zikiwemo Sheria Ndogo na utaratibu wa kuzingatiwa katika mchakato wa uandaaji wa sheria hizo, utangazaji wake kwenye Gazeti la Serikali, kutumika kwake na nafasi ya Bunge katika mchakato huo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na masharti hayo, Sheria Ndogo huwekwa Mezani Bungeni kwa mujibu wa Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria. Kifungu hicho kimeweka sharti la kuweka Mezani Sheria Ndogo zote ndani ya siku sita za Mkutano wa Bunge unaofuata baada ya kuwa zimechapishwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Kwa mujibu wa Kifungu hicho, Bunge linaweza kuona iwapo Sheria Ndogo inayohusika inahitaji kubadilishwa, kurekebishwa au kuongezwa masharti mengine.

**Mheshimiwa Spika**, Mantiki ya uwezo huo wa Bunge inatokana na umuhimu wa Sheria Ndogo kukidhi malengo ya Sheria Mama au Sheria nyingine zilizotungwa na Bunge. Maelezo hayo yanazipa Shughuli za Kamati mashiko ya kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo zinaendana na masharti ya Katiba, Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi. Jumla ya shughuli hizo ni Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo ambaao ni jambo la lazima kwa Bunge lenye tija na ufanisi unaloliongoza.

## 1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, imeilazimu Kamati kubainisha njia na mbinu zilizotumika wakati wa kutekeleza majukumu yake. Kufanya hivyo, ni kutimiza masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayotaka Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni kuonesha njia au mbinu zilizotumiwa na Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Kwa masharti hayo naomba kubainisha njia au mbinu zilizotumika kama ifuatavyo:-

- (a) Kupitia Magazeti ya Serikali yaliyowasilishwa Mezani ili kupata orodha na jumla ya Sheria Ndogo zote. Lengo la mbinu hiyo ni kupata taswira ya wigo wa kazi ya uchambuzi na kubaini sekta zinazohusika;
- (b) Kufanya uchambuzi wa awali wa Sheria Ndogo ili kubaini masharti yanayowekwa na Sheria hizo. Lengo ni kupima uzingatiaji wa masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria zingine za Nchi;
- (c) Kuhakiki mtiririko wa maudhui kwa kulinganisha masharti yanayowekwa katika Sheria Ndogo ikiwa ni pamoja na ukamilifu wa Majedwali. Lengo ni kubaini ukamilifu uliokusudiwa na Bunge wakati wa kukasimu madaraka ya ufanuzi kwa kutumia Sheria Ndogo;
- (d) Kuoa mbinu zilizotumika na misingi iliyowekwa katika Katiba na Sheria Nyingine za nchi. Lengo ni kujiridhisha na ukubalifu wa Sheria

Ndogo kwa misingi ya Sheria za nchi inayopaswa kuzingatiwa;

- (e) Kupatanisha maudhui ya Sheria Ndogo na madhumuni ya Sheria Kuu iliyoruhusu kutungwa kwa Sheria Ndogo inayohusika, ili kuhakikisha kuwa maudhui ya Sheria Ndogo hayakinzani na madhumuni ya Sheria Mama. Lengo ni kulishauri Bunge kwa misingi iliyowekwa na Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria; na
- (f) Kufanya mahojiano na mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo kwa idhini ya Bunge kwa ajili ya kupata maelezo kuhusu hoja zilizobainishwa. Lengo ni kupata ufanuzi wa ziada na kufananisha uelewa kuhusu matokeo ya uchambuzi kati ya Kamati na Mamlaka inayohusika. Aidha, njia hii iliwezesha kuchuja hoja zilizotokana na uchambuzi kabla ya kutoa Taarifa hii Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, naomba kulihiakikishia Bunge kwamba, njia na mbinu nilizozitaja, ziliwezesha Kamati kupata matokeo ya uchambuzi kwa namna inayotoa matumaini. Niwashukuru Mawaziri waliohusika na Sheria Ndogo katika kipindi hicho, kwa kutoa ushirikiano mkubwa ambao, uliwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kukidhi matarajio ya uchambuzi wa Sheria Ndogo na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

## **SEHEMU YA PILI**

### **2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI**

#### **2.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya Kamati hii ni kuripoti Bungeni shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Januari, 2023. Lengo ni kuliwezesha Bunge kubaini mafanikio na changamoto zilizopo katika utekelezaji wa madaraka ya kuweka Kanuni yaliyokabidhiwa kwa Mamlaka nyingine kwa kipindi hicho. Madhumuni hayo yatatimia kwa kubainisha Shughuli zilizotekelezwa kabla ya kuonesha yatokanayo na shughuli hizo. Kwa urahisi wa kufuatilia mtiririko, shughuli hizo zimegawanyika katika makundi makuu mawili:-

- (a) Shughuli za Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo; na
- (b) Shughuli za Uchambuzi wa Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa kila shughuli ni chanzo cha mapendekezo katika hoja ya Kamati, naomba kufafanua Shughuli hizo. Ufafanuzi huo unahu Kamati ilivyofanyia kazi na matokeo ya kazi hiyo kama ifuatavyo:-

#### **2.1.1 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari 2023, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo ishirini na nne (24) ambazo ziliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne. Matokeo ya

ufuutiliaji wa Maazimio kuhusu Sheria Ndogo hizo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 21 Septemba, 2022 wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa maazimio kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba, matokeo yake yanaelezewa katika Taarifa hii. Lengo ni kulionesha Bunge hatua inayofikiwa katika kutekeleza maazimio yake kuhusu madaraka linayokasimu kwa mamlaka zingine kutunga Sheria Ndogo na kulishauri jambo la kufanya au la kutokufanya.

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli hiyo ilikamilishwa kwa mambo yafuatayo:-

- (a) Kupokea Taarifa za Utekelezaji kabla ya kukutana na mamlaka zilizohusika ili kuoanisha na Maazimio yaliyopitishwa na Bunge. Lengo ni kubaini hatua iliyokuwa imefikiwa katika utekelezaji;
- (b) Kuoanisha hatua iliyofikiwa na madhara ya dosari au hitilafu iliyokuwa imebainika. Lengo ni kulionesha Bunge iwapo utekelezaji umeendana na matarajio yake kuhusu madhara ya dosari yaliyopaswa kuondolewa; na
- (c) Kukutana na Mamlaka zinazohusika ili kupata ufanuzi wa kina kuhusu mashaka yaliyopatikana wakati wa uchambuzi wa taarifa

hizo. Lengo ni kuzingatia utaratibu mzuri wa misingi ya asili kisheria ili kufikia msimamo wa kutumainiwa juu ya jambo linalohusika.

**Mheshimiwa Spika**, hatua hizo zimechangia uthabiti wa matokeo ya uchambuzi yaliyotolewa taarifa hapo awali na mengine yanayoripotiwa leo hii. Kwa hakika ni utaratibu unaostahili kuendelezwa ili kuwawezesha wananchi kupata tija ya utekelezaji wa madaraka ya Bunge ambalo, kimsingi ni chombo chao cha uwakilishi.

### **2.1.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni**

**Mheshimiwa Spika**, Kundu la pili la Shughuli zilizotekelawa na Kamati zinahusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kwa kuwekewa utaratibu chini ya Kanuni ya 43(2) ya Kanuni za Bunge. Shughuli zilizotekelawa na Kamati linahusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Sita, Mkutano wa Saba, Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge yalikwisha wasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane, mnamo tarehe 21 Septemba, 2022. Taarifa hii inaeleza matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika

Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa ambayo hayajawasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli mahususi zilizotekelizwa katika Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizingatia umuhimu wa kubaini iwapo kuna dosari au hakuna dosari katika kutumia madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka zingine. Aidha, utaratibu wa kupata maelezo ya mamlaka zinazohusika ulizingatiwa. Lengo lilikuwa ni kukidhi masharti ya Kanuni za Bunge yanayohusu majukumu ya Kamati na utaratibu wa kutekeleza majukumu hayo.

## **2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lako linao wajibu wa kuhakikisha kwamba, madaraka yake ambayo yamekabidhiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika inavyostahili. Ili kutimiza wajibu huo ni jukumu la Bunge lenyewe kufuutilia ipasavyo namna madaraka hayo yanavyotumika. Kwa maneno mengine, Bunge halipaswi kuishia kwenye kubainisha dosari katika Sheria Ndogo na kuamua kwa njia ya maazimio. Kwa kawaida, Bunge linapaswa kujiridhisha iwapo dosari hizo zimerekebishwa kwa namna ilivyoazimiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Sheria Ndogo ni sehemu ya Sheria za nchi, dosari zinazojitokeza katika Sheria hizo, zinapaswa kufanyiwa kazi kwa utaratibu unaoendana na desturi za Bunge. Bila kufanya hivyo, madhara ya dosari zote yanavyoendelea yanaweza kuliweka Bunge kwenye

kulaumiwa na wananchi. Bunge hili ambalo ni chombo halisi cha wananchi haliwezi kuacha kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake kuhusu dosari katika Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha tija ya ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ulizingatia hatua iliyoripotiwa kuwa imefikiwa kwa kudadisi wa mambo yafuatayo:-

- (a) Iwapo hakuna Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ilioandalishi;
- (b) Iwapo marekebisho yaliyoazimiwa yamezingatiwa katika Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo inayohusika;
- (c) Iwapo Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo imepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki;
- (d) Iwapo Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefikia hatua ya kusubiri kutangazwa; na
- (e) Iwapo Rasimu ya marekebisho ya Sheria Ndogo inayohusika imetangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, udadisi kwa kuegemea katika vigezo hivyo, uliiwezesha Kamati kutathmini hali ya utekelezaji wa kila azimio lililotolewa na Bunge na hatimaye kupata matokeo halisi ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji. Matokeo hayo yataliwezesha Bunge kuamua kuhusu hatua inayofuata.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge yanafaa kuripotiwa. Matokeo hayo yanaonesha kwamba, hatua za utekelezaji zilizoripotiwa zinagawanyika katika makundi makuu sita yafuatayo:-

- (a) Hatua ya kutotekeliza Maazimio ya Bunge;
- (b) Hatua ya Kutokamilika kwa Rasimu ya Marekebisho;
- (c) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho inayosubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki;
- (d) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki;
- (e) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali; na
- (f) Hatua ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kufafanua hatua hizo za utekelezaji ili kuliwezesha Bunge kufuatilia ipasavyo na hatimaye kutoa maazimio yanayostahili. Katika kufanya hivyo, naomba kubainisha Wizara saba (7) zinazohusika na Sheria Ndogo zilizopata maazimio ya Bunge. Wizara hizo ni:-

- (a) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) iliyokuwa na Sheria Ndogo nne (4) zilizobainika kuwa na jumla ya hoja tisa (9);

- (b) Wizara ya Fedha na Mipango iliyokuwa na Sheria Ndogo nne (4) zilizokuwa na hoja saba (7);
- (c) Wizara ya Afya iliyokuwa na Sheria Ndogo Mbili ambazo zilibainika kuwa na jumla ya hoja tisa (9);
- (d) Wizara ya Nishati iliyohusika na Sheria Ndogo tatu zenye hoja tano (5);
- (e) Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo iliyohusika na Sheria Ndogo moja (1) ambayo ilikuwa na hoja sita (6);
- (f) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliyohusika na Sheria Ndogo nne (4) zenye hoja kumi na moja (11); na
- (g) Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliyokuwa na Sheria Ndogo tatu (3) zenye hoja sita (6).

**Mheshimiwa Spika**, Taswira halisi ya hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge inabainishwa katika **Kiambatisho Na. 1** (Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita, na Mkutano wa Saba). Jedwali hilo ambalo ni sehemu ya Taarifa hii linafafanua hatua iliyofikiwa na kila Wizara. Pamoja na hivyo, kwa madhumuni ya kuweka mtiririko unaowezesha majadiliano juu ya hoja hii, naomba kufafanua hatua hizo kama ifuatavyo:

### **2.2.1 Hatua ya Kutotekeleza Maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulibaini Kutotekelezwa kwa sehemu ya Maazimio ya Bunge, ambapo baadhi ya Wizara zimeandaa Marekebisho

ya Sheria Ndogo ambazo yamefika katika hatua mbalimbali pasipo kuzingatia maazimio yaliyotolewa na Bunge. Wizara zilizobainika kuwa katika hatua hii ni:-

- (a) Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara;
- (b) Wizara ya Afya;
- (c) Wizara ya Fedha na Mipango; na
- (d) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Maazimio ambayo hayajatekelezwa yanafafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii na yapo katika Sheria Ndogo zifuatazo:-

- (a) *The Standards (Cooperation in Execution of Powers and Functions) Regulations (TS. Na. 680 24/09/2021);*
- (b) *The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021 (TS Na. 685 24/9/2021);*
- (c) *The Mining (Government Minerals Warehouse) Regulations (TS Na. 58 28/01/2022); na*
- (d) *The Transport Licensing (Private Hire Services) Regulations, 2020 (TS Na. 795 3/12/2021).*

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya kutotekeleza Maazimio ya Bunge inaweza kuwa na taswira ya kutokuyapa uzito Maazimio ya Bunge. Hatua ya kutotekeleza maazimio ni kufifisha dhamira ya Bunge ya kuondoa dosari katika Sheria Ndogo zinazohusika hivyo kuendeleza dosari hizo ambazo zinasababisha changamoto.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa changamoto inayoendelea kutokana na kutokutekelezwa kwa

Maazimio ya Bunge ipo Sheria Ndogo ya The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021 (TS Na. 685 24/9/2021). **Kanuni ya 22(2)** ya Sheria Ndogo hizi, inaonesha kuwa iwapo sampuli zilizochukuliwa kwa lengo la kufanyiwa uhakiki na kubainika hazina madhara zitagawiwa kama msaada kwa taasisi za umma na vituo vya afya. Bunge liliona kuwa, masharti ya Kanuni hizi hayaoneshi uwezekano wa sampuli hizo kurejeshwa kwa mzalishaji au msambazaji ili aendelee na utaratibu wa kuzifanyia biashara kama alivyokusudia.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge hili liliazimia dosari hiyo irekebishwe ili kuonesha utaratibu wa kurejesha kwa mmiliki sampuli zilizohakikiwa na kubainika hazina madhara kwa matumizi. Kwa minajili hiyo, kutokuwepo kwa hatua yoyote ya utekelezaji wa azimio hili kunaendeleza kero kwa walengwa, jambo ambalo Bunge haliwezi kuacha dosari hiyo iendelee.

## **2.2.2 Hatua ya kutokamilika kwa Rasimu ya Marekebisho**

**Mheshimiwa Spika**, Hatua ya Kutokamilika kwa Rasimu ya Marekebisho inaonesha kuwa nyuma katika utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Kwa maneno mengine hatua hiyo ni kwamba inaendeleza dosari zilizobainishwa na madhara yake yanaendelea kuwepo bila kuwa yamefanyiwa kazi. Jambo hili

linaleta mashaka makubwa kwa Kamati kuhusu tija ya madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya kutokukamilika kwa Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ambayo chimbuko lake ni Maazimio ya Bunge inaweza kuwa na taswira kuchelewesha utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Ikumbukwe kuwa Maazimio ya Bunge yanalenga kusimamia madaraka yake yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine. Hatua ya kuchelewa katika utekelezaji wa maazimio inafifisha dhamira ya Bunge ya kuondoa dosari katika Sheria Ndogo zinazohusika hivyo kuendeleza dosari hizo ambazo zinasababisha changamoto mbalimbali mionganoni mwa walengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara zilizobainika kuwa katika hatua hii ni :-

- (a) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; na
- (b) Wizara ya Utamuduni Sanaa na Michezo.

Dosari za Sheria Ndogo ambazo bado zipo katika hatua ya kurekebishwa zinafafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 1** kwenye Sheria Ndogo zifuatazo ni:

- (a) *The Tanzania Meteorological Authority (Cost Recovery on Meteorological Services) Regulations* (TS Na. 642 03/09/2021); na
- (b) *The Copyright and Neighbouring Rights (Licensing and Rights to Benefit from Re-Sale), Regulations* (TS Na. 137 18/3/2022)

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa changamoto inayoendelea kutokana na kutokamilika kwa Rasimu ya Marekebisho kuhusu Maazimio ya Bunge inayohusu eneo la kukiuka Sheria ya Mikataba. Changamoto hiyo inatokana na Sheria Ndogo ya *The Copyright and Neighbouring Rights (Licensing and Rights to Benefit from Re-Sale), Regulations 2022* iliyo chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 3(2) (3)** cha Sheria kilikuwa na dosari ya kuweka sharti la lazima kuwa, kabla ya kuanza kutumika kwa Mkataba wowote ulioingiwa nchini Tanzania kati ya mwenye hakimiliki na kampuni au Taasisi, Mkataba huo utapaswa kupelekwa COSOTA, ili iupitie na kushauri, ambapo COSOTA itatoza 1% ya thamani ya Mkataba unaohusika kama gharama za huduma iliyotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge liliona kuwa, masharti ya Kanuni hii yanalazimisha kutokuanza kwa makubaliano kati ya wahusika hadi COSOTA itakapoamua, hali inaweza kutafsiriwa kuwa ni kuingilia makubaliano. Bunge hili liliazimia dosari hiyo irekebishwe ili kuondoa sharti la lazima la kuwasilisha Mkataba COSOTA kabla Mkataba unaohusika haujaanza kufanya kazi na kuonesha utaratibu wa kupitia Mkataba kwa atayetaka kufanya hivyo, ufanyike kabla ya Mkataba unaohusika haujafungwa. Aidha iliazimiwa kuwa, Kanuni iainishe muda ambao COSOTA itatumia wakati

mapitio ya Mikataba inayohusika ili kuondoa uwezekano wa kuchelewesha utekelezaji wa shughuli za wanaohusika na Mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa minajili hiyo ni vema Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoa msukumo wa haraka kukamilisha Kanuni kuhusu mfumo mpya wa ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kupitia vyama vya wasanii (CMOs). Aidha, Wizara nyingine zinazohusika na hatua hii, pia ziweke msukumo kwa hatua zilizobaki ili kutekeleza maazimio ya Bunge.

### **2.2.3 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho Kusubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki**

**Mheshimiwa Spika,** Hatua ya Rasimu ya Marekebisho kusubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki inaonesha kufanyika juhudzi za awali kurekebisha dosari. Hali hiyo ni mwelekeo wa kuepusha madhara yatokanayo na dosari hiso. Kwa kufanya hivyo, Mamlaka zinazohusika zimeanza kuzingatia maazimio ya Bunge ili kutatua changamoto. Hata hivyo, kasoro zilizobainishwa na kutolewa Maazimio na Bunge bado zingali zinaendelea kutokana na kutokufikia mwisho kwa mchakato wa marekebisheso. Kamati inaamini kuwa kazi ilioanza itahitimishwa inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** Hatua hii ya Utekelezaji wa Maazimio inafafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 1** cha

Taarifa. Wizara zilizohusika katika hatua hizo ni kama ifuatavyo:-

- (a) Wizara ya Nishati; na
- (b) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

**Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo zinazohusika katika hatua hii ni:-

- (a) *The Electricity (Electrical Installation Services) Rules, 2022* (TS Na. 113 4/3/2022);
- (b) *The Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations) Rules, 2022* (TS Na. 15025/3/2022);
- (c) Kanuni za Anwani za Makazi katika Mamlaka za Miji za Mwaka, 2022 (TS Na. 109 25/2/2022);
- (d) Kanuni za Anwani za Makazi katika Mamlaka za Wilaya, 2022 (TS Na. 110 25/2/2022);
- (e) Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, 2022 (TS. Na. 127 4/3/2022); na
- (f) Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, 2022 (TS Na. 128 4/3/2022).

**Mheshimiwa Spika**, hatua iliyofikiwa na Wizara zinazohusika bado haijatatu changamoto zilizobainishwa. Mfano wa **Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, 2022 (TS**

**Na. 128 4/3/2022**) ambayo chini ya Kifungu cha 3(1) (a) iliweka sharti kuwa mfugaji anayefuga ndani ya Halmashauri atapaswa kufuga mifugo kwa idadi itakayoamuliwa na Halmashauri. Azimio la Bunge lililenga kufuta uwezo wa Halmashauri kuamua kuhusu idadi ya mifugo itakayofugwa na mtu anayeishi ndani ya eneo la Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa azimio la Bunge ulilenga kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza kwa Halmashauri kuamua idadi ya mifugo watakayopaswa kufugwa. Hivyo hatua iliyofikiwa katika kutekeleza Maazimio ya Bunge inaendeleza changamoto zilizobainishwa katika Sheria Ndogo.

#### **2.2.4 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki**

**Mheshimiwa Spika**, kufikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho iliyowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki ni kiashiria cha hatua muhimu. Hatua hiyo inaonesha nia ya kuzingatia maazimio ya Bunge kwa lengo la kuondoa changamoto mbalimbali zilizobainishwa katika Sheria Ndogo zinazohusika. Wizara zilizofikia hatua hiyo ni Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika Sheria Ndogo zifuatazo:-

- (a) *The Tanzania Meteorological Authority (Complaints Handling Procedures) Regulations, 2021 (TS Na. 643 3 Septemba, 2021); na*

(b) *The Transport Licensing (Private Hire Services) Regulations, 2020 (TS Na. 795 3/12/2021).*

**Mheshimiwa Spika**, Kuwasilishwa kwa Rasimu ya Marekebisho ili ihakikiwe ni hatua ya pili kuelekea kutimiza azimio la Bunge kuhusu marekebisho ya Sheria Ndogo yenye lengo la kuondoa dosari. Mfano wa dosari iliyotolewa azimio na ambayo utaratibu umefikia hatua hii ni kuhusu sharti kwa mwenye leseni ya kutoa huduma ya usafiri binafsi wa kukodi kuhakikisha kwamba, utoaji huo wa huduma huingilii huduma ya mabasi ya daladala lililowekwa chini ya **Sheria Ndogo ya The Transport Licensing (Private Hire Services) Regulations, 2020 (TS Na. 795 3/12/2021).**

**Mheshimiwa Spika**, Azimio la Bunge katika Sheria Ndogo hii lilikuwa ni kuitaka mamlaka inayohusika ifanyiwe marekebisho kwa kuweka tafsiri ya neno “*interfere*” kwa lengo la kuondoa utata unaoweza kujitokeza kuhusu mantiki ya neno “*kuingilia*”. Hivyo, hatua iliyofikiwa iwapo ikikamilika itaondoa mkanganyiko wa tafsiri ya kuingilia huduma ya vyombo vyya usafiri wa umma.

#### **2.2.5 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali**

**Mheshimiwa Spika**, kukamilisha Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na inayosubiri Namba ya Tangazo la Serikali ni hatua ya

juu kabla ya kuchapishwa kwa marekebisho yatokanayo na utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Ingawa inaonekana ni hatua iliyochelewa kwa kiasi fulani, lakini ni utekelezaji na uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge unaoelekea kuondosha dosari na madhara yatokanayo na dosari hizo. Wizara zilizofikia hatua hiyo ya utekelezaji ni Wizara ya Afya, yenye Sheria Ndogo zinazorekeblishwa ambazo ni:-

- (a) *The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021* (TS Na. 685 24/9/2021); na
- (b) *The Tanzania Medicines and Medical Devices (Fees and Charges) Regulations, 2021* (TS Na. 686 /24/9/ 2021).

**Mheshimiwa Spika**, Hatua iliyofikiwa na Wizara hiyo kwenye Sheria Ndogo zinazohusika, inafanikisha dhamira ya Bunge kuondoa dosari katika Sheria Ndogo. Lengo ni kuondoa changamoto inayoweza kusababishwa na Sheria Ndogo katika hali halisi ya utekelezaji. Kwa mfano wa changamoto inayogusa hali halisi ambayo imetatuliwa kutokana na hatua ya marekebisho iliyofikiwa na Wizara ya Afya katika Sheria Ndogo ya ***The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021* (TS Na. 685 24/9/2021)**.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo hizo zilikuwa na dosari ya kuvuka mipaka iliyowekwa na Sheria Mama. Kanuni ya 2 ilionesa mipaka ya TMDA kufikia uwekaji wa utaratibu wa namna ya kuendesha shughuli za uchunguzi wa kimaabara katika udongo, sampuli za binadamu na wanyama. Bunge hili liliazimia dosari hiyo irekebishwe kwa kuwa jukumu la kushughulikia uchunguzi wa kimaabara katika udongo, sampuli za binadamu na wanyama liliowekwa katika Kanuni hizo ni kinyume na lengo la Sheria Mama ambalo ni udhibiti wa dawa, vifaa tiba, dawa za asili pamoja na sumu.

**Mheshimiwa Spika**, hatua ya utekelezaji wa azimio hili iwapo itakamilika itaboresha Kanuni hizi ili kuendana na Majukumu ya TMDA yaliyo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge. Hata hivyo, matokeo ya utekelezaji wa Azimio la Bunge yangekuwa na manufaa makubwa zaidi iwapo mamlaka zinazohusika zingekuwa zimekamilisha hatua hiyo mapema.

## 2.2.6 Hatua ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Marekebisho ya Sheria Ndogo Kutangazwa katika Gazeti la Serikali ni hatua iliyokamilishwa na Mamlaka zinazohusika na Sheria Ndogo hizo. Kwa ujumla hatua hii ni ya juu ya uzingatiaji wa maazimio ya Bunge. Kwa kufanya hivyo, mamlaka zinazohusika zimeweka juhudhi katika usahihishaji wa dosari zilizobainishwa. Kwa kufanya hivyo madhara ya dosari hizo yameondoshwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara zilizofikia hatua ya kutangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali ni:-

- (a) Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara;
- (b) Wizara ya Nishati;
- (c) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; na
- (d) Wizara ya Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo zinazohusika katika hatua hii ni:-

- (a) *The Standards (Imports Registration and Batch Certification) Regulations, 2021* (TS Na. 681 24 Septemba, 2021);
- (b) *The Standards (Recall, Seizure and Disposal of Product) Regulations, 2021* (TS Na. 682 24 Septemba, 2021);
- (c) *The Tanzania Shipping Agencies (Performance Benchmarks) Regulations, 2022* (TS Na. 116 4/3/2022);
- (d) *The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Products Price Setting) Rules* (TS Na. 57 28/01/2022);
- (e) *The Banking and Financial Institutions (Development Finance) Regulations* (TS. Na. 766 29/10/2021);
- (f) *The Mining (Government Minerals Warehouse) Regulations* (TS Na.58 28/01/2022);

- (g) The Tax Administration (Administration of Tax Ombudsman Services) Regulations (TS Na. 105 05/02/2022); na
- (h) The Tax Administration (Tax Ombudsman Services Complaint Procedures) Regulations (TS Na. 106 25/02/2022).

**Mhesimiwa Spika**, Mfano wa dosari ambayo imeondoshwa kutohakana na kutekelezwa kwa azimio la Bunge kwa hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ni dosari za Sheria Ndogo ya **The Standards (Recall, Seizure and Disposal of Product) Regulations, 2021 (TS Na. 682 24 Septemba, 2021)**. Azimio la Bunge katika Sheria Ndogo hizi lililenga kuondoa kasoro ya kutooneshwa utaratibu wa kutoa matangazo kwa umma kuhusu kurejesha bidhaa ambazo hazina viwango na kwamba, kutooneshwa kwa utaratibu huo, kungeliweza kusababisha kuendelea kusambaa zaidi kwa bidhaa zisizofaa pasipo kufahamika katika jamii.

**Mhesimiwa Spika**, Wizara imetekeliza azimio la Bunge kwa kuongeza **Kanuni 4 (3) (b)** inayoweka utaratibu wa namna ya kutoa matangazo kwa umma kuhusu kurejesha bidhaa zisizokidhi viwango. Marekebisho haya yanawezesha utekelezaji wa madhumuni ya usimamizi wa viwango na ubora wa bidhaa na huduma yaliyowekwa na Sheria Mama iliyotungwa na Bunge. Vilevile, marekebisho yaliyofanyika yatasaidia umma wa watanzania

kupata taarifa kuhusu bidhaa zisizokidhi viwango ambazo wanazitumia katika maisha ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo, hatua ya kutangaza marekebisho katika Gazeti ambayo imefikiwa na Wizara zinazohusika ni mwitikio mzuri wa maazimio ya Bunge yaliyolenga kuondoa changamoto zilizobainishwa katika Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, Ufanuzi huo kuhusu hatua za utekelezaji wa Maazimio, umeonesha taswira halisi ya hatua mbalimbali zilizofikiwa na mamlaka zinazohusika. Taswira hiyo italiwezesha Bunge hili kujadili na kutafakari na hatimaye kuazimia kwa kuzingatia matokeo ya tathmini kuhusu kila hatua ya utekelezaji iliyofikiwa.

## **2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo ambazo ziliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa**

### **2.3.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani nakala za Magazeti ya Serikali na nyongeza zake zikiwemo jumla ya Sheria Ndogo mia moja hamsini na nane (158). Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo hizo yanabainisha jumla ya Sheria Ndogo Thelathini na Moja (31) kuwa na dosari mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa urahisi wa kufuatilia dosari hizo, Taarifa hii imeambatisha Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika

Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa ambalo ni **Kiambatisho Na.2.** Naomba Majedwali yote yaliyoambatishwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) ili kuweka kumbukumbu za mtiririko mzuri wa mchakato wa udhibiti wa Sheria Ndogo zilizochambuliwa.

### **2.3.2 Mchanganuo wa Dosari zilizobainika**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inaonesha mchanganuo wa Sheria Ndogo pamoja na dosari ambapo baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari zaidi ya moja. Kwa sababu hiyo, jumla ya idadi ya Sheria Ndogo 31 zilizochambuliwa inaweza isifikiwe kwa kujumlisha idadi katika mchanganuo huo. Kwa ujumla, mchanganuo wa dosari hizo unaonesha kuwa:-

- (a) Jumla ya Sheria Ndogo Kumi na Tatu zina masharti yanayokinzana na Katiba;
- (b) Jumla ya Sheria Ndogo Kumi zina masharti yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi;
- (c) Jumla ya Sheria Ndogo Ishirini na Saba zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi. Makosa hayo nia kama vile kutorejea vifungu sahihi, kurejea vifungu ambavyo havipo, kutokukamilika kwa Sheria Ndogo kwa kutokuepo kwa baadhi ya vipengele muhimu vyta kisheria ili kukamilisha sheria husika;

- (d) Jumla ya Sheria Ndogo Kumi na Mbili zinaweka masharti yasiyo na uhalisia ambayo yataleta changamoto katika utekelezaji wake; na
- (e) Sheria Ndogo Kumi na Tano zina makosa ya maudhui ya majedwali kutofautiana na vifungu vinavyoyaanzisha au makosa ya kutokekamiliika kwa majedwali au kuanzishwa kwa majedwali yasiyokuwepo ama kukosekana kwa majedwali.

**Mhesimiwa Spika**, Kwa minajili ya kulitaarifu Bunge lako, mifano ya dosari zilizobainika katika Sheria Ndogo zilizochambuliwa inafafanuliwa kwenye aya za **2.3.3 - 2.3.7** zinazofuata.

### **2.3.3 Dosari ya Kukinzana na Masharti ya Katiba**

**Mhesimiwa Spika**, Sheria Ndogo hutungwa kwa madhumuni ya kufanikisha lengo kuu la Sheria Mama. Aidha, Sheria Ndogo zinatarajiwa kuendana na masharti ya Katiba ambayo ni sheria Kuu ya nchi. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha kuwa baadhi ya Sheria Ndogo ziliwa na maudhui yanayotofautiana na matakwa ya Katiba. Kwa mfano, **Kifungu cha 5 (5) cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, 2022 (TS Na. 586 30/09/2022)** kinampa uwezo afisa mwidhiniwa kuingia katika jengo lolote na muda wowote kwa lengo la kukusanya ada au ushuru.

**Mhesimiwa Spika**, Mamlaka anayopewa afisa mwidhiniwa kuingia katika jengo muda wowote usio

na kikomo cha ndani ya muda wa kazi yanaweza kusababisha ukiukwaji wa haki ya msingi ya faragha. Hali hiyo inasababisha kero kwa wananchi wanaowakilishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mwingine wa Sheria Ndogo iliyo na masharti yanayokinzana na Katiba ni **Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022, (TS Na. 219 15/04/2022)**. Kifungu cha 4(1) (a) cha Sheria Ndogo hii, pamoja na mambo mengine kinaweka sharti kwa mtu anayetaka kufanya shughuli ya kilimo ndani ya Halmashauri kufuata kalenda ya Kilimo ya Halmashauri. Masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi yana muonekano usiofaa kwa umma kwa kuondoa mnyumbuko wa shughuli za kilimo. Hii ni kutokana na kuwabana wananchi ili watekeleze shughuli za kilimo zilizopangwa na halmashauri, na matokeo yake kukiuka **Ibara ya 8(1)** ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inayolinda ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, ikiwa Bunge litaruhusu utaratibu unaowekwa na Kanuni hizo, basi litakuwa linabariki uvunjaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo chini ya **Ibara ya 16 (1)** ya Katiba ambayo imeelekeza bayana kuwa kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake na maisha yake binafsi na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake, na **Ibara ya 8(1)**

**(b)** inayotambua lengo kuu la Serikali kuwa ni ustawi wa wananchi. Hivyo, Sheria Ndogo haipaswi kukinzana na Katiba ya nchi ambayo ni Sheria mama ya Sheria zote na hivyo iwapo Sheria Ndogo itakinzana na Katiba basi Sheria Ndogo hiyo inakuwa ni batili.

#### **2.3.4 Dosari ya Kukinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za nchi**

**Mhesimiwa Spika**, Sheria Ndogo hutungwa ili kufafanua au kuwezesha utekelezaji wa malengo ya Sheria Mama inayoanzisha Sheria Ndogo inayohusika. Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa, umebaini kasoro ya Sheria Ndogo kuwa na maudhui yanayokinzana na Sheria Mama. Mfano wa Sheria Ndogo yenye maudhui hayo, ni **The Merchant Shipping (Maritime Labour), Regulations 2022 (TS Na. 228 22 Aprili 2022)**. **Kanuni ya 83** inaweka adhabu ya jumla, iwapo mtu amekiuka masharti yoyote ya Kanuni ambapo hakuna Kanuni mahsus iinayoweka adhabu ya kukiuka masharti hayo, mtu huyo atapaswa kulipa faini shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na dola za marekani 500 au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja. Wakati huo huo sheria mama chini ya **Kifungu cha 401**, imeweka adhabu ya jumla iwapo mtu atakiuka masharti ya sheria hiyo kuwa atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania zenyet thamani ya dola za kimarekani 1000 au kifungo cha muda

usiopungua miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika**, adhabu iliyowekwa katika Kanuni inakinzana na adhabu iliyowekwa na Sheria Mama ambapo, kukinzana huko ni kwenye kiasi cha faini kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo ambacho ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotajwa katika sheria Mama na adhabu ya kifungo inayowekwa na Sheria Ndogo ni kubwa kuliko iliyowekwa katika Sheria Mama.

**Mheshimiwa Spika**, ni matarajio ya Bunge kuwa, Mamlaka za Serikali zilizokasimiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo, zitunge sheria hizo kwa kuendana na matakwa ya Sheria Mama zilizotungwa na Bunge. Inapotokea Sheria Ndogo imeweka masharti yanayokinzana na Sheria Mama, kamwe Bunge haliwezi kufumbia macho dosari hiyo kwakuwa, inaweza kufifisha lengo lilokusudiwa na Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi zilizotungwa na Bunge.

### **2.3.5 Dosari ya Kutoendana na Misingi Bora ya Uandishi wa Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria za Bunge huandikwa kwa kuzingatia misingi ya uandishi wa Sheria. Misingi hiyo huwezesha kuweka mawazo ghafi katika ukamilifu unaoeleweka na wenyewe maana katika masharti ya sheria inayohusika. Bunge hili, huzingatia misingi hiyo kutokana na kazi nzuri ya Mwandishi Mkuu wa Sheria Nchini. Hivyo, Sheria Ndogo pia zinatarajiwa kuzingatia

ipasavyo misingi ya uandishi wa sheria nchini. Lakini, kutokana na uchambuzi wa kina, Sheria Ndogo zimebainika kuwa na dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa Sheria Ndogo yenyе dosari hii ni **Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022, (TS Na. 217 15 Aprili 2022), Kifungu cha 8** kinachohusu muda wa kusafirisha mazao kinaonesha mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kusafirisha mazao kuanzia saa 1:00 jioni hadi saa 12:00 asubuhi. Kifungu kimekosa ukamilifu wa sentensi, hivyo hakipo wazi kuhusu muda uliotajwa iwapo ni wa kusafirisha au unaokataza kusafirisha. Kutokukamilika kwa sentensi na maelezo kuhusu muda wa kusafirisha mazao kunatatanisha masharti hayo kuhusu muda.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria Ndogo nyingine yenyе dosari kutoendana na misingi bora ya uandishi ni **The Banking and Financial Institutions (Mortgage Refinance Companies) Regulations, 2022. (TS Na. 559 16 Septemba 2022)**. Kanuni ya 6(3) (b) inaweka kiwango cha ada ya usajili ya shilingi milioni tano au kiwango kingine kitakachoamuliwa na Benki Kuu, kwa mtu anayetaka kuanza biashara ya mortgage re – financing. Kanuni imetoa mwanya kwa Benki Kuu kutoza ada ya usajili inayoweza kuzidi au kupungua. Kiasi hicho kilichotajwa hakifafanui ukomo wa chini wala wa juu.

**Mheshimiwa Spika**, Hali hiyo inaweza kusababisha kutoeleweka kwa ada halisi ya usajili, uwezekano wa uwepo wa viwango mbalimbali vya ada ya usajili na kuleta mkanganyiko kwa watekelezaji wa kanuni hizi. Hii pia ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria inayotaka Sheria Ndogo ye yote inayotaja viwango vya ada na tozo kuainisha viwango kwa namna ambayo haitaleta utata katika utafsiri wake.

### **2.3.6 Dosari ya Kukosa Uhalsia**

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mambo mengine, Utungaji mzuri wa Sheria huzingatia uhalsia wa utekelezaji wa sheria inayohusika. Mojawapo ya mambo ya uhalsia yanayozingatiwa ni hali halisi ya walengwa wa sheria inayohusika. Lakini uchambuzi wa Kamati umebaini Sheria Ndogo kuwa na changamoto ya kuwa na masharti yasiyo na uhalsia. Kwa mfano, **Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022, (TS Na. 216 15 Aprili 2022) Kifungu cha 14(3)** cha Sheria Ndogo hizo kinachukulia kosa la abiria kutupa takataka nje ya chombo cha usafiri, limetendwa na mmiliki au dereva au kondakta wa chombo hicho. Kifungu hicho kinafafanua kuwa, mtendaji wa kosa hilo atalazimika kulipa kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushitakiwa mahakamani.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uhalsia adhabu hulenga kumuadhibu mtenda kosa na kuwaogofya wengine

wasitende kosa. Kwa namna ilivyoelezwa adhabu katika Kifungu cha 14 (3), mtenda kosa halisi ni msafiri aliyetupa taka nje ya chombo cha usafiri, lakini anayeadhibiwa ni mmiliki au dereva au kondakta wa chombo kinachohusika. Hali hiyo, inaonesha lengo la adhabu halimgusi mlengwa wala haliogofyi watu wengine kutenda kosa kwa kuwa watakaoadhibiwa sio watendaji wa kosa.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile sharti la adhabu liliowekwa katika Kifungu cha 14 (3) linasababisha usumbufu kwa wasiotenda kosa linalohusika. Kwa namna hiyo, Sheria Ndogo hiyo imeweka adhabu kwa masharti yasiyozingatia uhalisia katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi.

**Mheshimiwa Spika**, dosari ya kukosa uhalisia pia imebainika katika **Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, 2022 (TS Na. 605 21 Oktoba 2022). Kifungu cha cha 8 (2)** kinaeleza kwamba, itakuwa ni kosa kwa mwenye basi au dereva au kondakta iwapo abiria aliyeko ndani ya basi lake atatupa kitu chochote barabarani au stendi. Aidha Kifungu kidogo cha (3) kinaeleza kuwa mwenye basi au dereva au kondakta atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu hamsini baada ya kujaziwa fomu ya ilani na afisa mwidhiniwa wa Mji endapo abiria aliyeko ndani ya gari lake atatupa uchafu katika barabara au kituo cha mabasi.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu hiki kinawapa adhabu watu kwa makosa ya wengine. Wanaoadhibiwa hawana namna ya kumzuia mkosaji halisi na wala sio waliomshawishi mkosaji kutenda kosa. Hali hiyo haitimizi lengo la kuzuia kosa kurudiwa na mfanyaji wa kosa wala mtu mwingine kwa sababu atakaye adhibiwa siye mtenda kosa.

### **2.3.7 Dosari za Uandishi wa Majedwali**

**Mheshimiwa Spika**, uwepo wa Majedwali katika Sheria yeote hulenga katika kutimiza malengo yaliyokusudiwa na kifungu cha Sheria inayohusika, hivyo ni matarajio ya msomaji wa Sheria ya kuwa Majedwali ndani ya sheria kuendana na matakwa ya kifungu wezeshi. Kukiuka lolote kati ya haya katika uandishi wa Majedwali ni makosa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa Sheria Ndogo yenye dosari hizo ni **Sheria Ndogo (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Mji wa Bunda, 2022, (TS Na. 375/ 27 Mei 2022)**. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi linaonesha kuwa limetokana na Kifungu cha 25 linahusu ada ya ukaguzi wa afya. Kwa kawaida Kifungu kinachotajwa kuanzishwa kwa Jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha msomaji kwenye Jedwali linalohusika. Hata hivyo, Jedwali la Kwanza linarejea kuanzishwa chini ya Kifungu cha 25 ambacho maudhui yake hayahusiani na Jedwali hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kawaida uandishi wa Majedwali katika sheria unalenga kutoa ufanuzi wa ziada wa maudhui yaliyo katika vifungu. Kwa msingi huo, kutokuandika majedwali kwa ufasaha kunasababisha mkanganyiko katika usomaji wa sheria na unaoweza kuathiri malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano mwagine wa makosa katika Majedwali umeonekana katika **Sheria Ndogo za Ada na Vibali vya Burudani za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022 (TS Na. 560/ 16/09/2022)**. Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi linarejea kuanzishwa chini ya Kifungu cha 4(2) ambayo maudhui yake hayahusiani na Jedwali hilo. Urejeaji wa kanuni isiyoendana kimaudhui unakiuka matakwa yaliyowekwa na Kifungu cha 11 (3) Sheria ya Tafsiri ya Sheria inayoelekeza urejeaji sahihi wa vifungu katika Majedwali. Hali hii inaleta ugumu wa kueleweka kwa masharti ya kanuni na utekelezaji wa Sheria Mama.

**Mheshimiwa Spika**, Ili tija ya Bunge kukasimu madaraka ya kufafanua sheria kwa mamlaka nyingine ipatikane, matokeo ya matumizi ya madaraka hayo, yanapaswa kuzingatia dhamira ya Bunge katika Sheria Mama.

## 2.4 Majumuisho kuhusu yatokanayo na Shughuli zilizotekelizwa

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla shughuli zilizotekelizwa na Kamati zilitokana na misingi ya majukumu ya Kamati kuanzia masharti ya Katiba, Sheria ya Tafsiri ya Sheria na Kanuni za

Bunge. Shughuli hizo zililenga kulisaidia Bunge katika wajibu wake wa Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo. Mambo yaliyobainika kutohana na Shughuli hizo ni pamoja na dosari katika maeneo matano ya Sheria Ndogo. Maeneo hayo yanahusu kutokuendana na masharti ya Katiba, kukinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria Nyingine za nchi na Kutozingatia misingi ya Uandishi bora wa Sheria. Mengine ni kutokuzingatia uhalisia pamoja na makosa katika uandishi wa majedwali.

**Mhesimiwa Spika**, Matokeo hayo yanaonesha athari hasi katika utaratibu wa Bunge kukasimu kwa mtu au Mamlaka nyingine kutunga kanuni kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 97 (5) ya Katiba. Hali hiyo inalihitaji Bunge kusema jambo linaloweza kuondoa athari hiyo. Aidha, athari nyingine hasi inatokana na kubainika kwa hatua za utekelezaji wa maazimio ya Bunge zinazoweza kuainishwa katika makundi matano kulingana na athari zake. Makundi hayo ni:-

- (a) Hatua ya kutotekeliza Maazimio ya Bunge;
- (b) Hatua ambayo Rasimu ya Marekebisho haijakamilika;
- (c) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho inayosubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki;
- (d) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki;
- (e) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali; na

(f) Hatua ya Kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Hatua nzuri na ya kupongezwa ni ile ya kukamilisha marekebisho na kutangazwa katika Gazeti la Serikali, kwa sababu hatua hiyo inajielekeza kwenye kuondoa hitilafu zilizobainishwa. Kundi hili linahusu baadhi ya Sheria Ndogo za Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Nishati.

**Mheshimiwa Spika**, Kundi jingine linajumuisha hatua za Utekelezaji uliochelewa ambazo nayo inarekebisha hitilafu zilizobainika lakini kwa kuchelewa. Hatua hizo si mbaya ingawa ingelifaa kukamilisha mapema ili kupunguza muda wa athari hasi za dosari zilizobainishwa. Wizara zilizofikia hatua hizo ni:-

- (a) Wizara ya Afya, iliyofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali;
- (b) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, iliyofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki;
- (c) Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), iliyofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho inayosubiri kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki; na
- (d) Wizara za Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambazo bado zinaendelea kukamilisha mchakato wa Rasimu ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika baadhi ya Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la mwisho linahusu Wizara ambazo hazijatekeleza Maazimio ya Bunge katika baadhi ya Sheria Ndogo. Wizara hizo ni Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Mipango; na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Kutokontaktelezwa kwa maazimio kunaendeleza changamoto ambazo Bunge limeziona katika Sheria Ndogo mbalimbali hivyo kushindwa kutatua kero zilizokusudiwa kuondolewa na Bunge.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

#### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 136 (15)** ya Kanuni za Bunge, inaweka ulazima wa kila Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa Mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bunge la Bajeti. Nia ya utaratibu huu wa kikanuni ni kuliwezesha Bunge kujadili na kutoa uamuzi juu ya shughuli hizo kama zinavyoelekezwa na Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kamati ya Sheria Ndogo imepewa majukumu ya kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria inayotekelizwa na Sheria Ndogo husika pamoja na sheria nyingine za nchi ili kusimamia adhma ya matumizi sahihi ya madaraka ya Bunge ya kutunga sheria iliyokasimisha kwa mamlaka nyingine, mjadala wa taarifa hii unahitaji umakini wa hali ya juu ili kufanikisha lengo lilikusudiwa na Bunge wakati linakasimisha madaraka yake kwa mtu au mamlaka zingine. Aidha, ikizingatiwa kuwa Sheria Ndogo hugusa maisha ya wananchi moja kwa moja katika utekelezaji wake, ninaliomba Bunge lako lipokee mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii na kuifanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Ili Taarifa hii iweze kuwa na mantiki inayoendana na uchambuzi na mapendekezo naomba kudhihirisha mtazamo wa Kamati unaotokana na

uchambuzi. Kwa ufupi mtazamo huo upo kwenye mambo saba kama ifuatavyo:-

### **3.1.1 Sheria Ndogo Kukinzana na Masharti ya Katiba**

**Mhesimiwa Spika**, Dosari ya Sheria Ndogo kukinzana na Katiba ya Nchi ni dosari kubwa inayoitoa Sheria hiyo nje ya Misingi ya Utungaji wa Sheria. Kamati ina maoni kwamba, Bunge ambalo ni Mamlaka ya kutunga Sheria, halipaswi kuruhusu Madaraka yake yaliyokabidhiwa kwa Mamlaka nyingine yatumike kinyume na misingi ambayo lenyewe, halipaswi na haliwezi kuikiuka.

### **3.1.2 Sheria Ndogo Kukinzana na Masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi**

**Mhesimiwa Spika**, Dosari ya Sheria Ndogo kukinzana na Masharti ya Sheria Mama haipaswi kuendelea kuwepo. Dosari hiyo inavuka madaraka yaliyokabidhiwa kwa mamlaka inayohusika na vilevile, ni kinyume na matarajio ya Bunge ambalo limepewa mamlaka yote ya kutunga Sheria za nchi. Ni maoni ya Kamati kuwa, kuendelea kutumika kwa Sheria Ndogo hizo, si jambo jema kwa desturi na misingi ya Sheria.

### **3.1.3 Sheria Ndogo kutozingatia Misingi ya Uandishi bora wa Sheria**

**Mhesimiwa Spika**, Bunge hutunga Sheria kwa kuzingatia uandishi ulio bora ili kuwezesha malengo iliyoyakusudia katika Sheria inayohusika. Ni maoni ya Kamati kwamba, kutungwa kwa Sheria Ndogo

zinazotofautina na misingi ya uandishi bora wa sheria ni jambo lisiloendana na matarajio ya Bunge na linapaswa kurekebishwa inavyostahili.

### **3.1.4 Sheria Ndogo kuwa na Masharti yasiyozingatia Uhaliisa**

**Mhesimiwa Spika**, Sheria Ndogo zenyе Masharti yasiyozingatia uhaliisa zinaweza kukwamisha malengo ya Bunge kutunga Sheria Mama inayohusika. Ni maoni ya Kamati kuwa, zaidi ya kukwamisha malengo ya Sheria Mama, Sheria Ndogo zenyе dosari hiyo zinaweza kusababisha kero kwa Wananchi. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linahitaji kuona madaraka yake yanayokabidhiwa kwa mamlaka nyingine hayatumiki kusababisha kero kwa wananchi.

### **3.1.5 Sheria Ndogo kukosa Usahihi na Ufasaha katika Uandishi wa Majedwali**

**Mhesimiwa Spika**, Dosari ya Sheria Ndogo kukosa usahihi inaathiri ukamifu wa ufanuzi wa Sheria ya Bunge uliotarajiwa kutolewa kupitia Sheria Ndogo. Ni maoni ya Kamati kwamba, Sheria Ndogo zilizokosa usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali zinatatiza ufanuzi uliokusudiwa na Bunge wakati wa kukasimu madaraka yake kwa mamlaka zilizohusika. Kwa msingi huo, Bunge linatarajiwa kuonesha hatua zinazostahili ili kurekebisha dosari hiso.

### **3.1.6 Uchelewaji katika Kutekeleza Maazimio yanayohusu Kurekebisha Sheria Ndogo**

**Mheshimimiwa Spika**, Maazimio ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari katika Sheria Ndogo, yalilenga kuondoa madhara ya dosari hizo, ikiwemo uwezekano wa kero kwa wananchi. Bunge ambalo ni sauti ya wananchi halipaswi kutokusema chochote inapotokea dosari hiyo. Ni maoni ya Kamati kuwa kuchelewa kutekeleza maazimio ya Bunge yanayolenga kuondoa dosari za Sheria Ndogo, ni jambo linalochelewesha utatuzi wa kero za wananchi pale ambapo dosari hizo zinasababisha kero kwa watu.

### **3.1.7 Kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mambo mengine Maazimio ya Bunge hutolewa kwa lengo la kuelekeza utekelezaji wa jambo fulani ambalo Bunge limeshughulikia na kutoa uamuzi, ikiwemo Maazimio kuhusu marekebisho ya Sheria Ndogo. Ni maoni ya Kamati kuwa, kutokuzingatia Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo ni jambo linalokumbatia dosari zilizolengwa kurekebishwa. Bunge ambalo ndilo Mamlaka kuu ya Utungaji wa Sheria halitarajijiwi kuunga mkono desturi ya mamlaka iliyokasimiwa jukumu la kutunga Sheria Ndogo kuendelea kukumbatia dosari za Sheria Ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kujumuisha maoni ya Kamati, naomba kulikumbusha Bunge hili kuwa dosari zilizobainika zinaathiri tija ya Bunge kukasimu madaraka ya kuweka kanuni kwa mamlaka nyingine. Athari hizo ni pamoja na kuweka ugumu wa kueleweka kwa sheria na kusababisha kero kwa wananchi kutokana na hitilafu kwenye Sheria Ndogo. Madhara mengine ya dosari hizo ni uwezekano hafifu wa kutimia kwa lengo la baadhi ya Sheria zilizotungwa na Bunge na kuendelea kwa desturi isiyofaa katika utaratibu wa Sheria za nchi. Mambo hayo yanahitaji hatua za haraka za marekebisho na hasa kwa kuwa Sheria Ndogo zinagusa moja kwa moja maslahi ya wananchi katika utekelezaji wa shughuli za umma. Hali hiyo ndio hasa msingi wa mapendekezo ya maazimio ya Bunge katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile kuchelewa kutekeleza Maazimio ya Bunge yanayohusu marekebisho ya dosari za Sheria Ndogo ni jambo lenye madhara kwenye nia ya Bunge kukasimu mamlaka nyingine uwezo wa kufanua Sheria Kuu kupitia Sheria Ndogo. Madhara hayo ni pamoja na kuendeleza kero kwa wananchi licha ya kuwa zimebainishwa na chombo chao cha Uwakilishi. Aidha, hali hiyo inasababisha kuendeleza hitilafu ambazo Bunge ambalo ni chombo kikuu cha Utungaji wa Sheria nchini lisingeliweza na kamwe halitarajiwi kudumisha hitilafu hizo pale zinapobainikana. Kwa sababu hiyo Taarifa hii inajumuisha Mapendekezo ya Maazimio ya Bunge kwa lengo la kuondoa hitilafu hizo.

### **3.2 Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Mapendekezo ya Kamati ni maoni yake yaliyotokana na shughuli kubwa mbili. Shughuli hizo nilizitaja kuwa ni Uchambuzi wa Sheria Ndogo na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Kutokana na Maoni ya Kamati kuhusu dosari zilizojitokeza katika Sheria Ndogo, Kamati inapendekeza mambo saba kwa njia ya hoja kama inavyoelekeza Kanuni ya 61 ya Kanuni za Bunge. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

#### **3.2.1 Kukinzana na Masharti ya Katiba**

**KWA KUWA**, baadhi ya Sheria Ndogo zimebainika kukinzana na masharti ya katiba, suala ambalo ni kinyume na misingi ya sheria inayotambua Ukuu wa Katiba,

**NA KWA KUWA**, ukiukwaji wa msingi wa masharti ya Katiba kwa sheria yoyote ni kinyume na Ibara ya 64 (5) ya Katiba na endapo sheria nyingine yoyote itakiuka masharti itakua ni batili,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi zifanyiwe marekebisho ndani ya siku sitini kwa ajili ya kutatua dosari hiyo.

### **3.2.2 Kukinzana na Masharti ya Sheria inayotoa Mamlaka ya Kutungwa kwa Sheria Ndogo au Sheria nyingine za Nchi**

**KWA KUWA**, baadhi ya Sheria Ndogo zimebainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa Sheria Mama inayohusika,

**NA KWA KUWA**, Kwa mujibu wa Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Sheria Ndogo inayokinzana na Sheria Mama au sheria nyingine za nchi ni batili kwa kiwango cha dosari hiyo,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zenyet kuzingatia misingi ya uandishi bora wa sheria,

**NA KWA KUWA**, Dosari ya uandishi bora wa Sheria inaweza kuharibu urahisi wa kusomeka kwa Sheria Ndogo, jambo ambalo halina msaada kwa nia ya Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka zinazohusika,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo zilizo kutwa na dosari ya

kutozingatia misingi ya uandishi bora wa sheria, zirekebishe dosari hiyo ndani ya sitini kuanzia leo ili kuleta tija kwa watumiaji wa sheria hizo.

### **3.2.4 Masharti Yasiyo na Uhalisia**

**KWA KUWA**, dosari ya kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia imebainika katika baadhi ya Sheria Ndogo, jambo linaloweza kuchangia ugumu wa utekelezaji,

**NA KWA KUWA**, Athari ya ugumu katika utekelezaji wa Sheria Ndogo ni jambo linalovuruga upatikanaji wa tija ya Sheria Ndogo hizo na kuondoa maana ya madhumuni ya kukasimu madaraka ya Bunge kutunga Sheria,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zinazotunga Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na masharti yasiyozingatia uhalisia, zifanye marekebisho ndani ya siku sitini kuanzia leo, ili kuendana na uhalisia na kurahisisha utekelezaji wake.

### **3.2.5 Dosari ya Uandishi wa Majedwali**

**KWA KUWA**, Majedwali ni sehemu ya ufanuzi wa Sheria uliolenga kurahisisha uelewa na kutoa ufanuzi wa vifungu vya Sheria,

**NA KWA KUWA**, baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari ya uandishi wa Majedwali hali inayosababisha changamoto katika utekelezaji vifungu vya Sheria Ndogo inayohusika,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga Sheria Ndogo na kubainika kuwa na dosari katika uandishi wa majedwali zifanye marekebisho ndani ya siku sitini kuanzia leo.

### **3.2.6 Uchelewaji katika Kutekeleza Maazimio ya Kurekebisha Sheria Ndogo**

**KWA KUWA**, Baadhi ya Mamlaka zimechelewa kutekeleza maazimio ya Bunge kuhusu marekebisho ya Sheria Ndogo, jambo ambalo linaendeleza dosari zilizokuwa zimebainika wakati wa uchambuzi,

**NA KWA KUWA**, kuchelewa huko kunasababisha kuendelea kuwa na Sheria Ndogo zenyet dosari licha ya Bunge ambalo ni Chombo kikuu cha kutunga sheria kuelekeza tofauti,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizobainika kuchelewa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, zikamilishe mchakato wa marekebisho ndani ya siku thelathini kuanzia leo na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wake wakati wa vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2023.

### **3.2.7 Kutokutekelezwa kwa Maazimio**

**KWA KUWA**, zipo mamlaka ambazo hazijatekeleza kabisa maazimio ya Bunge kuhusu Marekebisho ya Sheria Ndogo hadi muda huu,

**NA KWA KUWA**, kutokutekelezwa kwa maazimio ya marekebisho ya Sheria Ndogo kama yalivyotolewa na Bunge ni ishara ya kuendeleza kuwabebesha mzigo

wananchi      wanaoguswa      na      Sheria      Ndogo  
zinazohusika,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizobainika kutotekeleza maazimio ya Bunge zitekeleze Maazimio hayo ndani ya siku thelathini kuanzia leo na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wake wakati wa vikao vya Kamati vya mwezi Machi, 2023.

## **SEHEMU YA NNE**

### **4.0 HITIMISHO**

#### **4.1 Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita, Mkutano wa Saba, Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge na hatimaye kufanikisha taarifa hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) – Mwenyekiti;
2. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, (Mb) - Makamu Mwenyekiti;
3. Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan, (Mb) Mjumbe;
4. Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar, (Mb) Mjumbe;
5. Mhe. Simai Hassan Sadiki, (Mb) Mjumbe;
6. Mhe. Sylvia Francis Sigula, (Mb) Mjumbe;
7. Mhe. Emmanuel Mageni Kasalali, (Mb) Mjumbe;
8. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, (Mb) Mjumbe;
9. Mhe. Edwin Enosy Swalle, (Mb) Mjumbe;
10. Mhe. Judith Salvio Kapinga, (Mb) Mjumbe;

11. Mhe. Santiel Erick Kirumba, (Mb) Mjumbe;
12. Mhe. Jacob Tarimo Priscus, (Mb) Mjumbe;
13. Mhe. Regina Ndege Qwaray, (Mb) Mjumbe;
14. Mhe. Esther Edwin Malleko, (Mb) Mjumbe;
15. Mhe. Amour Khamis Mbarouk, (Mb) Mjumbe;
16. Mhe. Esther Lukago Midimu, (Mb) Mjumbe;
17. Mhe. Minza Simon Mjika, (Mb) Mjumbe;
18. Mhe. Khamis Ali Vuai, (Mb) Mjumbe;
19. Mhe. Nicholaus George Ngassa, (Mb) Mjumbe;
20. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, (Mb) Mjumbe;
21. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, (Mb) Mjumbe;
22. Mhe. Eng.Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho, (Mb)  
Mjumbe;
23. Mhe. Ally Yahaya Mhata, (Mb) Mjumbe;
24. Mhe. Francis Isack Mtinga, (Mb) Mjumbe; na
25. Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, (Mb) Mjumbe.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mhe. George Simbachawene (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa uratibu ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao katika Vikao vya Uchambuzi wa Sheria Ndogo na Vikao vya kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, ndc kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, ndc akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Gerald S. Magili kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru makatibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg. Gwantwa Alex Mwakijungu, Ndg. Emmy Peter na Ndg. Ganjatuni Kilemle wakisaidiwa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Imelda Ntimba kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

## 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.



Jasson S. Rweikiza (Mb)  
**MWENYEKITI**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo**  
8 Februari, 2023

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**

**JEDWALI LA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KUHUSU SHERIA NDOGO  
ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA TANO, MKUTANO WA SITA NA**

**MKUTANO WA SABA WA BUNGE**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
<b>WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI</b>					
1.	<p>The Tanzania Meteorological Authority (Cost Recovery on Meteorological Services) Regulations, 2021  <b>(TS Na. 642</b>  <b>3 Septemba, 2021)</b></p>	<p>1. <b>Kanuni ya 3</b> imetafsiri baadhi tu ya huduma za hali ya hewa zikiwemo consultancy services, industrial activities, marine services, marine meteorological services.</p> <p><b>Tatizo</b>  Kanuni haijaweka tafsiri ya huduma nyingine za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya hali ya hewa.  Hali hii inaweza kusababisha baadhi ya wanaotoa huduma zilizoachwa kutofahamu wigo wa huduma wanayoweza kupatiwa na Mamlaka kwa kutokana na shughuli wanazozitekeleza.</p>	<p>1. <b>Kanuni ya 3</b> ifanyiwe marekebisho ili kuweka tafsiri ya huduma nyingine za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya hali ya hewa kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kusababisha kutofahamika wigo wa huduma zinazotolewa kwa shughuli inayohusika.</p>	<p>1. Azimio halijatekelezwa</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b>  Wizara imetoa maelezo kwamba, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) inaendelea kufanya kazi azamio hili. Msingi wa kuendelea kufanya kazi ni kwasababu suala hili ni la kimataifa, linahitaji kuwasiliana na taasisi za kimataifa zinazosimamia miongozo ya masuala ya hali ya hewa kikanda na kimataifa. ili kutoleta mkanganyiko katika tafsiri ya maneno husika katika Kanuni.</p> <p>Wizara inaadidi</p>	<p>1. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni itakuwa imekamilika mpaka kufikia tarehe 30 Januari, 2023.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
				<p>itakuwa imekamilika na marekebisho kuyawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi kufikia tarehe 30 Januari, 2023.</p> <p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b></p> <p>Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge ni kuendeleza changamoto kwa baadhi ya wanaotoa huduma zilizoachwa kutokufahamu wigo wa huduma wanayoweza kupatiwa na Mamlaka.</p> <p>2. Kanuni haziijaonesha uwezekano wa wachimbaji wadogo kupatiwa huduma za taarifa za hali ya</p> <p>2. Wizara itafakari ili kuona umuhimu kuwapa fursa Wachimbaji wadogo wa madini kupata</p> <p>2. Azimio halijatekelezwa</p> <p><b><u>Maelezo ya Wizara</u></b></p> <p>Wizara imetoa</p>	<p>2. Azimio la Bunge litekelezwe kuondoa changamoto iliyobainishwa.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		hewa iwapo watahitaji kupatiwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zao za uchimbaji wa madini.	huduma mahsus za hali ya hewa badala ya kuwekwa katika kundi la ambalo linapatiwa huduma za hali ya hewa kwa ujumla.	maelezo kwamba, kushirikiana na TMA iliratibu kikao kilichohusika wawakilishi wa wachimbaji wadogo na viongozi wa FEMATA ili kujadiliana nao kuhusu wachimbaji wadogo kupatiwa huduma mahsus za hali ya hewa na mapendekoz ya uchangiaji gharama za huduma za hali ya hewa lakini hawakuwa tayari na hawakutoa ushirikiano kwa madai kwamba wao hawataki masuala ya kuchangia gharama. Aidha, TMA iliandika barua kwenda Tume ya Madini yenye Kumb.Na.	

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
				<p>TMAC/1000/6 ya tarehe 26 Agosti, 2022 kwa ajili ya uratibu wa kikao kingine na nakala ya barua hiyo ilitumwa kwa kwa Katibu Mkuu wa FEMATA.</p> <p>Hadi sasa TMA hajijapata majibu ya barua husika.</p> <p>Hata hivyo, Wizara kwa kushirikiana na TMA itaendelea na uratibu wa vikao na wachimbaji wadogo na pindi yatakapofikiwa makubaliano Kanuni husika zitafanyiwa marekebisho.</p> <p>Hata hivyo, TMA itaandaa mwongozo ushirikishwaji wachimbaji wadogo katika</p>	

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
				<p>kupatiwa huduma mahsus za hali ya hewa.</p> <p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b></p> <p>Kutokutekelezwa kwa kwa azimio la Bunge kunaendeleza changamoto ya wachimbaji wadogo kutokupata huduma mahsus za taarifa hali za hewa.</p>	
2.	<p><i>The Tanzania Meteorological Authority (Complaints Handling Procedures) Regulations, 2021 (TS Na. 643 3 Septemba, 2021)</i></p>	<p><b>Jedwali la Pili</b> la Kanuni hizi linalohusu hati ya wito.</p> <p><b>Tatizo</b> Jedwali limerejea kimakosa kuanzishwa chini ya <b>Kanuni ya 18(2)</b> badala ya <b>Kanuni ya 17(2)</b> ambayo ndio mahsus kuhusu hati ya wito (summons).</p>	<p><b>Jedwali la Pili</b> lifanyiwe marekebisho ili kufuta <b>Kanuni ya 18(2)</b> inayorejewa na badala yake irejewe <b>Kanuni ya 17(2)</b>.</p>	<p>Rasimu ya marekebisho ya Kanuni imeandaliwa kwa kufuta <b>Kanuni ya 18(2)</b> inayorejewa na kurejea Kanuni ya <b>Kanuni ya 17(2)</b>.</p> <p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b> Iwapo Marekebisho yaliyofanywa</p>	<p>Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuitia barua yenyeye Kumb. Na. CAD.26/315/01-C/77 ya tarehe 28 Disemba, 2022 kwa ajili ya uhakiki.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		Hali hiyo inaathiri mtiririko wa usomaji unaoshikamanisha Kanuni na Majedwali yake, hivyo kutatiza usomaji na uelewa unaotakiwa.		yatakamilika yataondoa mkanganyiko wa usomaji wa Kanuni hizi kwa walengwa.	
3.	<i>The Transport Licensing (Private Hire Services) Regulations, 2020 (TS Na. 795 3/12/2021)</i>	<p>1. <b>Kanuni ya 15 (h)</b> inaweka sharti kwa mwenye leseni ya kutoa huduma ya usafiri binafsi wa kukodi kuhakikisha kwamba, utoaji huo wa huduma hatingilia huduma ya mabasi ya daladala.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Utekelezaji wa masharti hayo unaweza kusababisha changamoto pale ambapo wateja wa usafiri binafsi wa kukodi watasimama</p>	<p>1. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka kutafsiri ya neno “interfere” kwa lengo la kuondoa utata unaoweza kujitokeza kuhusu mantiki ya neno “kuingilia”</p>	<p>1. Rasimu marekebisho ya Kanuni 3 imeandaliwa kwa kuweka tafsiri ya neno “interfere”.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Iwapo Marekebisho haya yatakamilika, yatondoa mkanganyiko wa tafsiri ya kuingilia huduma ya vyombo vyaa usafiri wa umma.</p>	<p>1. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>katika vituo vya daladala na kusimamisha bajaji, pikipiki au Taxi zinazopita kwa lengo la kutumia huduma hiyo.</p> <p>Hali hiyo inaweza kutafsiriwa kuwa wameingilia huduma zinazotolewa na wenyewe leseni ya daladala.</p> <p>2. <b>Kanuni ya 15 (n)</b> inamtaka mtu mwenye leseni ya kutoa huduma ya usafiri wa kukodi, kutii masharti mengine yoyote kama yatakavyoamriwa na LATRA.</p> <p><b>Tatizo</b> Masharti ya Kanuni ya 15(n) yanaweza kusababisha watoa</p>	<p>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta <b>Kanuni ya 15 (n)</b> ili kuondoa masharti ya jumla katika Kanuni.</p>	<p>2. Rasimu ya marekebisho imeandaliwa kwa kufuta Kanuni ya 15 (n).</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b> Iwapo Marekebisho yatakamilika, yataondoa hatari ya matumizi ya mamlaka ya kikanuni yasiyo na</p>	<p>2. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>huduma kulazimika kutekeleza masharti mengine ambayo hayapo kwa mujibu wa Kanuni</p> <p>Athari ni hatari ya kuongezwa kwa masharti yasiyokusudiwa na Sheria Mama.</p> <p>3. <b>Kanuni ya 16 (d)</b> inaonesha mwenye leseni ya kutoa huduma ya usafiri wa bajaji na pipipiki atatoa sare kwa madereva wake kama itakavyo amuliwa na LATRA.</p> <p><b>Tatizo</b> Mashaka katika masharti hayo, ni uwezekano wa LATRA kutozingatia umuhimu wa kupata maoni ya wahusika kuhusu</p>	<p>3. Kanuni ziweke sharti kwa LATRA kuwashirikisha watoa huduma, ili kuepuwa uwezekano wa kutamka sare zisizozingatia mambo halisi katika huduma inayohusika.</p>	<p>ukomo.</p> <p>3. Azimio halijatekelezwa</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b> Rasimu ya marekebisho ya Kanuni imeandaliiwa na kutambua mamlaka za serikali za mitaa katika kuainisha aina ya sare na utambulisho.</p> <p><b>Athari za Marekebisho</b> Kutokutekeleza Azimio hili</p>	<p>3. Azimio la Bunge litekelezwe.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>uhalisia katika utekelezaji wake.</p> <p>4. Kanuni zimeeleza kwa ujumla kwamba, mwenye leseni ya teksi atapaswa kuweka alama ya rangi itakayoamuliwa na LATRA, pasipo kufafanua aina ya alama.</p> <p><b>Tatizo</b> Hali hiyo ni inaweka mkanganyiko kuhusu aina ya alama, iwapo itakuwa ni rangi ya kudumu au ya kubandika (stika).</p> <p>Kutokuwekwa kwa sharti la mahususi la aina ya rangi kwa alama inayokusudiwa inaacha uwezekano</p>	<p>4. Kanuni zifanyiwe marekebisho ili kuonesha sharti la rangi ya alama itakayowekwa katika teksi kwamba itakuwa ni ya kudumu.</p>	<p>kunaendeleza tatizo la kutokusirikishwa kwa watoa huduma katika zoezi la uchaguzi wa sare.</p> <p>4. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni imeandalialiwa kwa kuweka sharti la teksi kuwekewa alama za kudumu za utambuzi.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b> Iwapo marekebisho ya Kanuni yatakamilika yataondoa mkanganyiko kuhusu aina ya alama iwapo itakuwa ni rangi ya kudumu au ya kubandika (stika).</p>	<p>4. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>wa:-</p> <p>(i) Gari ambayo ni tekci kutumika katika matukio kama vile ya uhalifu pasipo kutambulika kama ni tekci pale ambapo alama itakuwa ni ya kubandika na ikabanduliwa; na</p> <p>(ii) Kuwafanya wasiokuwa na leseni ya kufanya biashara ya huduma hiyo kutumia mwanya uliopo kwa stika za kubandika na kufanya biashara hiyo pasipo kulipia leseni kama wafanyabiashara wengine katika huduma hiyo.</p>			

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>5. Kanuni zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, pasipo kuwa na toleo la lugha ya kiswahili.</p> <p>Hali hiyo inachangia ugumu wa walengwa wa kanuni hizo kutambua na kuzingatia masharti yaliyomo.</p> <p>6. Kanuni sehemu inayotaja kufanya kazi na vyama vya wenyewe leseni za watoa huduma za usafiri wa kukodi.</p> <p>Hali hii inaweza</p>	<p>5. Kanuni zitafsiriwe katika lugha ya kiswahili ili kuwawezesha walengwa kuyaelewa masharti yaliyomo katika Kanuni inavyostahili.</p> <p>6. Kanuni zifanyiwe marekebisho ili kutambua mashirikisho na vyama vya watoa huduma za usafiri zinazosimamiwa chini ya Kanuni hizo</p>	<p>5. Kanuni tayari zimeshatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na nakala ya tafsiri imeambatishwa.</p> <p><b><u>Athari za Marekebisho</u></b> Marekebisho ya kuandika Kanuni kwa lugha ya Kiswahili yatasaidia wanaolengwa na Kanuni hizo kufahamu masharti yaliyomo, hivyo itasaidia urahisi katika utekelezaji wake.</p> <p>6. Azimio halijatekelezwa</p> <p><b><u>Maelezo ya Wizara</u></b> Wizara imefafanua kwamba, hitaji hili liliondolewa kwenye Kanuni za mwaka</p>	<p>5. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki.</p> <p>6. Azimio la Bunge litekelezwe</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		kuonesha mwanya wa kutoshirikisha wadau katika masuala mbalimbali yahayohusu huduma inayotolewa.	kwa ajili ya kuchochea usimamizi mzuri wa sekta ya huduma za usafiri wa kukodi.	2020 baada ya kutumiwa vibaya na viongozi wa vyama vyatotoa huduma za usafiri ambao waliweka tozo kubwa kwa wanachana wao hadi kufikia 50,000/= kwa kila mwanachama hasa walipohitaji kutambulishwa kwa Mamlaka kwa lengo la kukata leseni. Hatua hii iliongeza gharama za huduma kwa abiria. Vilevile, vyama vyatotoa huduma mbalimbali husajiliwa chini ya Msajili wa vyama vyatotoa kijamii ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hivyo suala hili likishughulikiwa na LATRA linaweza	

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
				<p>kusababisha muingiliano wa majukumu. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ilioandalialiwa imezingatia uwezeshaji wa suala hili.</p> <p>Aidha, Mamlaka inapanga kuvijengea uwezo vyama vilivyopo ili viwe na muundo wa ushirika.</p> <p><b><u>Athari za</u></b> <b><u>Marekebisho</u></b></p> <p>Kutokutekelezwa kwa azimio kuendeleza uwezekano wa kutoshirikishwa wadau katika masuala yanayowahusu kwa mujibu wa Kanuni hizi.</p>	

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
7.	<i>The Tanzania Shipping Agencies (Performance Benchmarks) Regulations, 2022 (TS Na. 116 4/3/2022)</i>	<p>1. Kanuni za Wakala wa Meli (Alama Teule ya Utendaji) zimeweka jedwali linalohusu notisi ya ukubalifu (Compliance notice). Aidha, <b>Kanuni ya 16</b> inayohusu kutolewa kwa notisi ya ukubalifu inaelekeza kuwa Wakala wa Meli atatoa Notisi kwa namna ilivyofafanuliwa katika <b>Jedwali la Tatu</b>. Kwa ujumla Kanuni hizi zina majedwali matatu, Jedwali la Kwanza na la Pili yamepewa namba na kurejea Kanuni. Jedwali la mwisho halijapewa namba.</p>	<p>1. Jedwali lifanyiwe marekebisho kwa kuandika kichwa cha habari "<b>Third Schedule</b>" na kuonesha kuwa linatokana na <b>Kanuni ya 16</b>.</p>	<p>1. Azimio halijatekelezwa <b>Maelezo ya Wizara</b> Maelezo ya Kamati yanafafanua kwamba, baada ya Wataalam wa Wizara na TASAC kupitia Kanuni husika ilibainika kuwa, Jedwali la Tatu limewekwa kichwa cha habari yaani "<b>Third Schedule</b>". Aidha, pia ilibainika kuwa, Kanuni iliyoanzisha Jedwali hilo imetajwa ipasavyo ambayo ni Kanuni ya 16.</p>	<p>1. Kutokutekelezwa kwa Azimio, hakuna athari utekelezaji wa Kanuni hizi.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p><b>Tatizo</b></p> <p>Jedwali linalohusu  Notisi ya Ukubalifu halioneshi kanuni iliyoanzisha Jedwali hilo, vilevile Jedwali hilo halina namba. Hali hiyo inaathiri mtiririko wa usomaji unaoshikamanisha Kanuni na Majedwali yake, hivyo kutatiza usomaji na uelewa unaotakiwa.</p> <p>2. <b>Kanuni ya 14(2)</b> inampa mamlaka Waziri kuteua watu ambao watafanya tathmini ya utendaji wa Kampuni inayohusika na usafirishaji wataodumu katika nafasi hiyo kwa muda</p>	<p>2. <b>Kanuni ya 14</b> ifanyiwe marekebisho ili kuainisha sifa za wateuliwa ikiwemo Kada, Tasnia, aina, kategoria, pia ifafanue kinachoweza kufanyika iwapo</p>	<p>2. <b>Kanuni ya 14</b> imefanyiwa marekebisho kwa kuainisha sifa za wateuliwa ikiwemo kada, tasnia, aina, kategoria pamoja na kufafanua hatua za kuchukuliwa iwapo walioteuliwa</p>	<p>2. Mchakato wa marekebisho umekamilika na tayari yameshachapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 661/2022.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>wa miaka mitatu.          Kwa kawaida          wanaoteuliwa          hupatikana kutoka          aina ya watu au          wataalamu au kada          au tasnia fulani</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanani hazioneshi          watakapotoka          wanaoteuliwa (Kada,          Tasnia, aina,          kategoria n.k.).          Vilevile, Kanuni          hazibainishi sifa          zinazohitajika          kuzingatiwa katika          kufanya uteuzi wala          hazifafanui          kinachoweza          kufanyika iwapo          walioteuliwa          watashindwa          kukamilisha</p>	<p>walioteuliwa          watashindwa          kukamilisha          utekelezaji wa          majukumu ndani ya          muda waliopewa.</p>	<p>watashindwa          kukamilisha          utekelezaji wa          majukumu ndani ya          muda waliopewa.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Utekelezaji wa          azimio hili          utawezesha kanuni          kutekeleza malengo          ya sheria mama          kama yalivvolengwa          na Bunge wakati wa          utunzi wake.</p>	

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>utekelezaji wa majukumu ndani ya muda waliopewa.</p> <p>Kutokupambanuliwa kwa masuala hayo kunafifisha azma ya Sheria Ndogo kufafanua masharti ya Sheria Mama. Kwa hali hiyo, Kanuni hizo zinaweza kukosa uwezo wa kufanikisha madhumuni ya Sheria Mama ilipokasimu madaraka ya kufafanua masharti yake.</p>			

### WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

8.	The Standards (Cooperation in Execution of Powers and Functions) Regulations,	Kanuni ya 2 imetafsiri neno “standards” kwa kunakili tafsiri iliyopo kwenye Sheria mama.	Marekebisho yafanyike ili kufanya rejea ya kifungu cha sheria mama.	Azimio halijatekelezwa <b><u>Maelezo ya Wizara</u></b> Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara	Azimio la Bunge litekelezwe
----	---	--	---	---	--------------------------------

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	<p>2021  <b>(TS Na. 680</b>  <b>24 Septemba,</b>  <b>2021)</b></p>	<p><b>Tatizo</b>  Hali hiyo imeongeza maneno ya kutafsiri pasipo sababu ya msingi ili hali ingeweza kurejea tafsiri katika Sheria mama.</p>		<p>imetoa maelezo kwamba, kwa mujibu wa Kanuni za Uandishi wa Sheria (<i>Principles of Drafting</i>), neno lililotumika kwenye Sheria mama linaweza kutafsiriwa kwenye kanuni endapo limetumika mara nyingi kwenye kanuni inayohusika.</p> <p>Vivyo hivyo, neno 'standards' limetumika kwenye maeneo mengi katika Kanuni (<i>Kanuni ya 4, 5, 14, 20 na Jedwali</i>).</p> <p>Hivyo ili kurahisisha rejea ni vyema tafsiri hii ikaendelea kubaki. Aidha, utaratibu huu pia umetumika kwenye tafsiri ya maneno</p>	

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
				<p>product, commodity, Bureau, Director General, inspector.</p> <p><b><u>Athari ya kutorekebisha</u></b></p> <p>Kutokutekelezwa kwa azimio ni:-</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(i) Kuendeleza hali ya sheria ndogo kutoendana na malengo yaliyokusudiwa na sheria mama;</li> <li>(ii) kuendeleza mkanganyiko wa tafsiri ya neno “standard” kwa walengwa.</li> </ul>	
9.	The Standards (Imports Registration and Batch Certification) Regulations, 2021	<b>Fomu Na. 10 katika Jedwali la Kwanza</b> inarejea kuanzishwa chini ya Kanuni ya 18(2).	<b>Fomu Na. 10</b> ifanyiwe marekebisho kwa kufuta Kanuni ya 18(2) inayorejewa na badala yake irejee Kanuni ya 18(1)	Marekebiso ya <b>Fomu Na. 10</b> yamefanywa kwa kufuta Kanuni ya 18(2) inayorejewa na badala yake imerejewa Kanuni ya 18(1).	Mchakato wa marekebiso umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 12 Aprili, 2022 (TS

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	(TS Na. 681 24 Septemba, 2021)	<p><b>Tatizo</b></p> <p><b>Kanuni ya 18(2)</b></p> <p>iliyorejewa haihusiani na kibali cha kuruhusu uingizaji wa bidhaa kutoka nje (<i>Import clearance permit</i>). Kanuni sahihi kuhusu kibali cha kuruhusi uingizaji wa bidhaa kutoka nje (<i>Import clearance permit</i>) ni 18(1).</p>		<p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Marekebisho yaliyofanywa yameondoa mkanganyiko wa usomaji wa Kanuni hizi kwa walengwa.</p>	Na. 210)
10.	<p>The Standards (Recall, Seizure and Disposal of Product) Regulations, 2021</p> <p>(TS Na. 682 24 Septemba, 2021)</p>	<p>1. Kanuni zimerejea kuanzhwa chini ya <b>Kifungu cha 36(3)(f)</b></p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni haijarejea kuanzhwa chini ya <b>Kifungu cha 36(1)</b> ambacho kinaweka mamlaka ya jumla ya Waziri kutunga</p>	<p>1. Kanuni ifayiwe marekebisho ili kufanya rejea ya Kifungu cha 36(1).</p>	<p>1. Marekebisho yamefanyika kwa kufuta Kifungu cha 36(3)(f) kinachorejewa kama Kifungu kinachoanzisha Kanuni hizi na kuweka <b>Kifungu cha 36(1) na 3(g)</b>.</p>	<p>1. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 17 Juni, 2022 (TS Na. 416).</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>Kanuni.</p> <p>2. <b>Kanuni ya 2</b> imetafsiri neno “product” kuwa linajumuisha huduma “services” zilizobuniwa kwa lengo la kutolewa au kuzinduliwa. Hata hivyo, Kanuni yote inazungumzia kuhusu bidhaa na si huduma kama ilivyotafsiriwa katika Kanuni ya 2.</p>	<p>2. <b>Kanuni ya 2</b> ifanyiwe marekebisho ili kuondoa neno “services” tafsiri ya neno “product” ili kuendana na muktadha na Kanuni hii.</p>	<p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b> Marekebisho yaliyofanywa yamezingatia matakwa ya Sheria Mama iliyotungwa na Bunge ambayo ilielekeza Kanuni hizi kutungwa chini ya Kifungu cha 36(1).</p> <p>2. Azimio la Bunge halijatekelezwa</p> <p><b><u>Maelezo ya Wizara</u></b> Wizara imewasilisha maelezo kwamba, neno “product” libaki kama lilivyo kwa kuwa limetafsiriwa na kutumika kwenye Sheria ya Viwango Na. 2 ya Mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia</p>	<p>2. Kutokutekelezwa kwa azimio hakuna athari katika madaraka ya Bunge na utekelezaji wa Kanuni hizi.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>3. Kanuni hazioneshi utaratibu wa kutoa matangazo kwa umma kuhusu kurejesha bidhaa ambazo hazina viwango.</p> <p>Kutooneshwa kwa utaratibu huo, kunaweza kusababisha kuendelea kusambaa zaidi kwa bidhaa zisizofaa pasipo kufahamika katika jamii.</p>	<p>3. Kanuni zifanyiwe marekebisho ili kuongeza utaratibu wa utoaji wa matangazo kwa umma.</p>	<p>Sheria ya Fedha Na. 8 ya Mwaka 2019.</p> <p>3. Marekebisho yamefanyika kwa kuongeza <b>Kanuni 4(3)(b)</b> inayoweka utaratibu wa namna ya kutoa matangazo kwa umma kuhusu kurejesha bidhaa zisizokidhi viwango.</p> <p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b> Marekebisho ya kuweka utaratibu wa kutoa matangazo kwa umma kuhusu kurejesha bidhaa zisizokidhi viwango yanawezesha:</p> <p>(i) utekelezaji wa madhumuni ya Sheria Mama</p>	<p>3. Mchakato wa marekebisho umekamilika kwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 17 Juni, 2022 (TS Na. 416).</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>4. <b>Kanuni ya 3(2)</b> inaweka wajibu kwa msambazaji au mzalishaji wa bidhaa kutoa taarifa kuhusu bidhaa zisizo na ubora.</p>	<p>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka utaratibu wa namna ambavyo walaji pia wataweza kutoa taarifa kuhusu bidhaa zisizo na ubora.</p>	<p>iliyotungwa na Bunge.  (ii) marekebisho hayo yatasaidia umma wa watanzania kupata taarifa kuhusu bidhaa zisizokidhi viwango ambazo wanazizotumia katika maisha ya kila siku.</p> <p>4. Marekebisho yamefanyika kwa kuongeza neno "consumer" kwenye Kanuni ya 4(1) ambayo inaweka utaratibu wa Shirika kupokea taarifa kutoka kwenye chanzo chochote na kufanya</p>	<p>4. Mchakato wa Marekebisho umekamilika na kuchapishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 416 la tarehe 17/06/2022.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni hazioneishi namna ambavyo walaji pia wanaweza kutoa taarifa kuhusu bidhaa zisizo na ubora.</p> <p>Kukosekana kwa fursa hiyo kunaminya wigo wa upatikanaji wa taarifa kuhusu bidhaa zisizo na ubora kwa kuwa walaji ndio wanaweza kuwa na taarifa nzuri kuhusu ubora wa bidhaa wanazotumia.</p> <p>5. <b>Kanuni ya 5</b> inaweka utaratibu wa namna ya kushughulikia malalamiko yanayotokana na bidhaa za</p>		<p>uchunguzi.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Marekebisho yaliyofanyika yatasaidia ufanikishaji wa lengo la Sheria Mama la kulinda usalama wa watumiaji na ubora wa bidhaa.</p> <p>5. Kanuni zifanyiwe marekebisho ili kuonesha pia jukumu la kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko</p> <p>5. Marekebisho yamefanyika katika Kanuni ya 4 kwa kuongeza kanuni ndogo (5) inayoipa Shirika jukumu la kupokea,</p>	<p>5. Mchakato wa Marekebisho umekamilika na kuchapishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 416 la tarehe</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>wasambazaji au wazalishaji.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Msambazaji au mzalishaji wa bidhaa amepewa wajibu wa kuandaa nyaraka zinazoweka utaratibu wa kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko yanayotokana na bidhaa zao.</p> <p>Masharti ya Kanuni hiyo yanaweza kusababisha msambazaji au mzalishaji kupokea malalamiko dhidi yao na hivyo kuondoa uwajibikaji.</p>	<p>litafanyika na TBS kama msimamizi mkuu wa viwango vyaa bidhaa nchini.</p>	<p>kuchunguza na kushughulikia malalamiko.</p> <p><b>Athari za Marekebisho</b></p> <p>Marekebisho yaliyofanyika yameondoa wasiwasi uliokuwepo kuhusu uwezekano wa msambazaji au mzalishaji anayelalamikiwa kuijwekea utaratibu dhidi yake.</p>	17/06/2022.

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
<b>WIZARA YA AFYA</b>					
11.	The Tanzania Medicines and Medical Devices (Laboratory Analysis of Medical and Non Medical Products) Regulations, 2021 <b>(TS Na. 685</b> <b>24/9/2021)</b>	<p>1. <b>Kanuni ya 2</b> imeonesha kuwa Kanuni hizi zitatumika kuweka utaratibu wa namna ya kuendesha shughuli za uchunguzi wa kimaabara katika udongo, sampuli za binadamu na wanyama.</p> <p><b>Tatizo</b> Jukumu la kushughulikia uchunguzi wa kimaabara katika udongo, sampuli za binadamu na wanyama ni kinyume na lengo la Sheria Mama ambalo ni udhibiti wa dawa, vifaa tiba, dawa za asili pamoja na sumu.</p>	<p>1. <b>Kanuni ya 2</b> ifanyiwe marekebisho ii kuendana na majukumu ya TMDA yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria Mama.</p>	<p>1. Rasimu ya marekebisho ya <b>Kanuni ya 2</b> imeandaliwa kwa kufuta Jukumu la TMDA kushughulikia uchunguzi wa kimaabara katika udongo, sampuli za binadamu na wanyama.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b> Marekebisho ya kufuta jukumu la TMDA kushughulikia uchunguzi wa kimaabara katika udongo, sampuli za binadamu na wanyama, iwapo yatakamilika yataboresha Kanuni hizi ili kuendana na Majukumu ya TMDA yaliyo kwa mujibu wa Sheria Mama</p>	<p>1. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Kanuni imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Hata hivyo, imechukua zaidi ya miezi kumi na moja kufanya kazi azimio la Bunge kuhusu dosari ya Sheria Ndogo inayohusika. Hali hiyo imeendeleza tatizo la kukiuka masharti ya Sheria Mama kwa muda huo.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>Aidha, ni kinyume na Kifungu cha 122 (1) (t) (z) cha Sheria Mama ambacho kimempa Waziri mamlaka ya kutunga Kanuni za kuanzisha maabara za kupima dawa chakula, vipodozi na dawa za asili.</p> <p>2. <b>Kanuni ya 21(2)</b> inarejea Jedwali la Tano na Sita kuhusu Certificate of analysis.</p> <p><b>Tatizo</b> Jedwali la Tano na Sita hayapo katika Kanuni hizi.</p> <p>Hali hiyo inaweza kuwa imetokana na kusahalika kwa</p>	<p>2. <b>Kanuni ya 21(2)</b> ifanyiwe marekebisho ili kufuta rejea ya majedwali na badala yake Kanuni hii itaweka rejea ya Kanuni ya 17(2) inayoanzisha Form No. 2 kuhusu certificate of analysis na Fomu Na. 3 kuhusu Certificate of Conformity katika Jedwali la Kwanza.</p>	<p>iliyotungwa na Bunge.</p> <p>2. Rasimu ya marekebisho ya <b>Kanuni ya 21(2)</b> imeandaliwa kwa kufuta rejea ya majedwali tajwa na badala yake Kanuni ya kurejea Kanuni ya 17 inayoanzisha fomu Na. 2 na 3 zilizokusudiwa na maudhui ya Kanuni katika jedwali la kwanza.</p>	<p>2. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Kanuni imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>Hata hivyo, imechukua zaidi ya miezi kumi na moja kufanya kazi azimio</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>Jedwali na Tano na Sita katika Kanuni hizi hali inayoweza kusababisha kutokamilika kwa tija iliyokusudiwa katika Kanuni hizi.</p> <p>3. <b>Kanuni ya 22(1)</b> inaelekeza kuwa sampuli pekee za</p>		<p><b>Athari ya Marekebisho</b> Iwapo marekebisho Marekebisho yaliyofanyika yatakamilika:-</p> <p>(i) yataondoa mkanganyiko wa usomaji Kanuni hizi kwa walengwa;</p> <p>(ii) Yataendana na lengo la ukasimishwaji wa madaraka ya Bunge kwa mamlaka kutunga sheria au kanuni zinazoeleweka kwa watumiaji.</p> <p>3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuainisha utaratibu</p>	<p>la Bunge kuhusu dosari ya Sheria Ndogo inayohusika.</p> <p>3. Azimio halijatekelezwa</p> <p>3. Kutokutekelezwa kwa azimio hakuna athari katika</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>bidhaa zilizohakikiwa katika Maabara ya Mamlaka ndizo zitaharibiwa kwa utaratibu wa Kanuni za Kuharibu Bidhaa.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni hazioneshi utaratibu wa namna ya kuharibu sampuli za bidhaa ambazo zimehakikiwa na maabara ambazo zimekasimiwa jukumu la kuhakiki sampuli kwa niaba ya Mamlaka.</p> <p>4. <b>Kanuni ya 22(2)</b> inaonesha kuwa iwapo sampuli zilizochukuliwa ili kufanyiwa uhakiki na zikabainika hazina</p>	<p>wa kikanuni wa kuharibu sampuli za bidhaa ambazo zimehakikiwa na maabara nyingine tofauti na Maabara ya TMDA.</p> <p>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha utaratibiwa kurejesha wa mmiliki sampuli zilizohakikiwa na kubainika hazina madhara kwa</p>	<p><b>Maelezo ya Wizara</b></p> <p>Kanuni ya 22(1) imeainisha utaratibu wa kuharibu Sampuli zinazotokana na Maabara za TMDA pekee yake kwa kuwa Maabara zingine hazipo ndani ya mipaka ya kisheria inayosimamiwa na TMDA hivyo zinaturatibu wao wa kuharibu Sampuli katika Maabara zao.</p> <p>4. Azimio halijatekelezwa</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b></p> <p>Wizara imefafanua kwamba, marekebisho</p>	<p>utekelezaji wa Kanuni hizi.</p> <p>4. Hakuna hatua ya utekelezaji iliyofikiwa na Wizara mpaka hivi sasa.</p> <p>Ni zaidi ya miezi kumi na moja mpaka</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati																				
		<p>madhara zitagawiwa kama msaada kwa taasisi za umma na vituo vya afya.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <table> <tbody> <tr><td>Kanuni</td><td>hazioneshi</td></tr> <tr><td>uwezekano</td><td>wa</td></tr> <tr><td>sampuli</td><td>hizo</td></tr> <tr><td>kurejeshwa</td><td>kwa</td></tr> <tr><td>mzalishaji</td><td>au</td></tr> <tr><td>msambazaji</td><td>ili</td></tr> <tr><td>aendelee</td><td>na</td></tr> <tr><td>utaratibu</td><td>wa</td></tr> <tr><td>kuzifanya</td><td>biashara</td></tr> <tr><td>kama alivyokusudia.</td><td></td></tr> </tbody> </table>	Kanuni	hazioneshi	uwezekano	wa	sampuli	hizo	kurejeshwa	kwa	mzalishaji	au	msambazaji	ili	aendelee	na	utaratibu	wa	kuzifanya	biashara	kama alivyokusudia.		matumizi.	<p>yamefanyika kwa kufuta Kanuni ya <b>22(2)</b> na kuiandika upya ili kuanzisha hati ya makabidhiano na rejestra ya sampuli zinazogawiwa kama msaada kwenye vituo vya afya vya umma, zinazorejeshwa kwa mteja na zile ambazo zinaharibiwa moja kwa moja.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Kutokurekebishwa kwa Kanuni hiyo, kunaendeleza dosari inayosababisha wazalishaji na wasambazaji kutorudishiwa umiliki wa bidhaa zao baada ya kuwa</p>	sasa, lakini azimio la Bunge kuhusu dosari hiyo bado halijafanyiwa kazi.
Kanuni	hazioneshi																								
uwezekano	wa																								
sampuli	hizo																								
kurejeshwa	kwa																								
mzalishaji	au																								
msambazaji	ili																								
aendelee	na																								
utaratibu	wa																								
kuzifanya	biashara																								
kama alivyokusudia.																									

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>5. <b>Kanuni ya 33 (e)</b> inafafanua kwamba ikiwa mjambe wa Kamati ya Kitaalamu ya Maabara (<i>Laboratory Technical Committee</i>) atashitakiwa na kupatikana na hatia ya kosa lolote na kuhukumiwa kufungwa kifungo kinachozidi miezi sita, itasababisha kusababisha ujumbe wake kukoma.</p>	<p>5. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha makosa yatakayosababisha mjambe wa Kamati ya Kitaalamu ya Maabara (<i>Laboratory Technical Committee</i>) kukoma kuwa ni yale ambayo yanahusiana na majukumu yake.</p>	<p>zimepimwa na kugundulika hazina madhara. Hali hiyo inaendeleza athari ya uminywaji wa haki ya umiliki hivyo kuathiri biashara zao.</p> <p>5. Marekebisho yamefanywa katika Kanuni ya 33(e) kwa kuonesha kuwa, ujumbe wa Kamati utasitishwa iwapo utatokana na makosa ya jinai yatakayothibitishwa na Mahakama kuwa yametokana na kutenda kosa linalohusu majukumu ya mwanachama kwa mujibu wa Kanuni hii.</p> <p style="text-align: right;"><u><b>Athari za Marekebisho</b></u></p>	<p>5. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Kanuni imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>Hata hivyo, imechukua zaidi ya miezi kumi na moja kufanya kazi azimio la Bunge kuhusu dosari ya Sheria Ndogo inayohusika.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni haijaonesha makosa ya jinai kuwa ni lazima yatokane/yahusiane moja kwa moja na majukumu yanayotekelizwa na Mjumbe.</p> <p>6. <b>Kanuni ya 62</b> inaweka utaratibu wa namna ya kushughulikia rufaa.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Hata hivyo, Kanuni haioneshi muda ambaa rufaa iliyowasilishwa itashughulikiwa na sharti la mkata rufaa kujulishwa kuhusu uamuzi uliotolewa na</p>		<p>Marekebisho yaliyofanyika yatasahihisha dosari ya kuweka uwezekano wa Wajumbe kuadhibiwa chini ya Kanuni hizi kwa makosa ya jinai yasiyohusiana na majukumu yao.</p> <p>6. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka muda wa kushughulikia rufaa na utaratibu wa kumjulisha mrufani kuhusu uamuzi uliotolewa.</p>	<p>6. Marekebisho yamefanywa kwa kuongeza Kanuni ya 62 (4) ambayo inaweka utaratibu wa Waziri kutoa Taarifa kwa mrufani baada ya kufanya uamuzi juu ya rufaa yake.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Marekebisho haya yakikamilika yatampa mrufani</p> <p>6. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Kanuni imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.</p> <p>Hata hivyo, imechukua zaidi ya miezi kumi na moja kufanya kazi azimio la Bunge kuhusu</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		Mamlaka.		<p>fursa ya kutambua hali ya rufaa yake na kuchukua uamuzi unastahili.</p> <p><b><u>Maelezo</u></b>            Hata hivyo, azimio la pili kuhusu muda wa Waziri kushughulikia rufaa halijatekelezwa.</p> <p><b><u>Athari ya kutotekelezwa</u></b>            Kutokutekelezwa kwa azimio:-</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(i) Kunaendeleza uwezekano wa kuchelewa kwa maamuzi ya rufaa; na</li> <li>(ii) Kunaondoa uwajibikaji kwa Waziri katika kushughulikia rufaa kwa muda maalum.</li> </ul>	<p>dosari ya Sheria Ndogo inayohusika.</p> <p>7. Marekebisho yapo</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p><b>Jedwali la Kwanza</b> inayoonesha mfano wa Cheti cha Mafunzo imerejea kuanzishwa chini ya Kanuni ya 56.</p> <p><b>Tatizo</b> Kanuni ya 56 inayorejewa kuanzisha Fomu Na. 5 haihusiani na Cheti cha Mafunzo. Hali hiyo inaathiri mtiririko wa usomaji unaoshikamanisha Kanuni na Majedwali yake, hivyo kutatiza usomaji na uelewa unaotakiwa.</p>	<p>kufuta Kanuni ya 56 na kurejea Kanuni sahihi inayoanzisha Fomu hiyo.</p>	<p>yamefanyika katika Fomu Na. 5 kwa kufuta Kanuni ya 56 na badala yake kurejea Kanuni ya 55.</p> <p><b>Athari za Marekebisho</b> Marekebisho yaliyofanyika iwapo yatakamilika, yataboresha mtiririko wa usomaji unaoshikamanisha Kanuni na Majedwali yake na hatimaye kurahisisha usomaji na uelewa unaotakiwa. Hali hii inakamilisha lengo la ukasimishwaji wa madaraka ya Bunge kwa mamlaka kutunga sheria au kanuni zitakazo eleweka kwa watumiaji.</p>	<p>katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Kanuni imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Hata hivyo, imechukua zaidi ya miezi kumi na moja kufanya kazi azimio la Bunge kuhusu dosari ya Sheria Ndogo inayohusika.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
12.	The Tanzania Medicines and Medical Devices (Fees and Charges) Regulations, 2021 <b>(TS Na. 686 24/9/ 2021)</b>	<p>1. <b>Kipengele cha 65 hadi 68 vya Jedwali la Kwanza</b>          vinazungumzia kuhusu mbalimbali huduma majaribio maabara “clinical trials”.</p> <p><b>Tatizo</b>          Kiwango cha Ada kinachowekwa kipo katika viwango vya dola za marekani pasipo kuonesha iwapo huduma inayokudusiwa ni ya ndani au kutoka nje ya Tanzania au ni kwa ajili ya Watanzania.</p>	<p>1. Kanuni ifanyiwe marebisho ili kuonesha kuwa viwango vilivyowekwa ni kwa ajili ya watafiti wa nje na wale wanafanya utafiti kwa kutumia wafadhili kutoka nje. Aidha, Kanuni iweke viwango vinavyopaswa kulipwa na watafiti wa ndani.</p>	<p>1. Rasimu ya marekebisho ya <b>Kipengele cha 65 hadi 68 vya Jedwali la Kwanza</b> imeandaliwa kwa kubadilisha viwango vya ada vilivyoandikwa kwa dola za kimarekani na badala yake kuwa katika shilingi za kitanzania.</p> <p><b>Athari za Marekebisho</b>          Marekebisho yaliyofanyika iwapo yatakamilika:-          (i) yatarahisisha uelewa juu ya viwango vinavyokusudiwa na kanuni hizi;          (ii) Yatasaidia</p>	<p>1. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Kanuni imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.          Hata hivyo, imechukua zaidi ya miezi kumi na moja kufanya kazi azimio la Bunge kuhusu dosari ya Sheria Ndogo inayohusika.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>2. <b>Kanuni ya 3</b> imetafsiri maneno Local Government Authority, innovator product, alterartion or innovation fee, animal biological specimens, annual retention fee, ceiling Price, customer, domestic product, donation, medical supplier.</p> <p><b>Tatizo</b> Maneno hayo hayajatumika katika</p>	<p>2. <b>Kanuni ya 3</b> ifanyiwe marekebisho ili kufuta maneno yaliyowekwa katika tafsiri pasipo kutumiwa katika Kanuni hizi.</p>	<p>Kuonesha iwapo huduma inayokusudiwa ni ya ndani ya nchi au kutoka nje ya nchi.</p> <p>2. Rasimu ya marekebisho ya Kanuni ya 3 imeandaliwa ili kufuta tafsiri ya maneno:- Local Government Authority, innovator product, alterartion or innovation fee, animal biological specimens, annual retention fee, ceiling Price, customer, domestic product, donation, medical supplier.</p>	<p>2. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Kanuni imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Hata hivyo, imechukua zaidi ya miezi kumi na moja kufanya kazi azimio la Bunge kuhusu dosari ya Sheria Ndogo inayohusika.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		sehemu yoyote ndani ya Kanuni hizi.		<p><u><b>Athari za Marekebisho</b></u>          Iwapo marekebisheso hayo yatakamilika, yanaweza kuondoa wasiwasi kiuandishi na usomaji kutokana na kuwa na maneno yaliyotafsiriwa lakini hayaonekani popote katika Kanuni.</p>	

### WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

13.	The Banking and Financial Institutions (Development Finance) Regulations, 2021 <b>(TS Na. 766 29/10/ 2021)</b>	<p>1. <b>Jedwali la Nne</b> limerejea kuanzishwa chini ya <b>Kanuni ya 19(1).</b></p> <p><b>Tatizo</b>  <b>Kanuni ya 19 (1)</b> haihusiani na <b>Jedwali la Nne</b> badala ya <b>Kanuni ya 18(1).</b></p> <p>Hali inasababisha kukosekana</p>	<p>1. <b>Jedwali la Nne</b> lifanyiwe marekebisheso kwa kufuta rejea ya <b>Kanuni ya 19(1)</b> na badala yake kurejea <b>Kanuni ya 18(1).</b></p>	<p>1. Azimio la Bunge limetekelizwa kwa kufanya marekebisheso ya kiuandishi katika Jedwali la Nne kwa kufuta rejea ya Kanuni ya 19(1) na badala yake kurejea Kanuni ya 18(1).</p>	<p>1. Mchakato wa Marekebisheso umekamilika na kuchapishwa kuitia Tangazo la Serikali <b>Na. 31 la tarehe 20 Januari, 2023</b></p>
-----	---	---	---	---	--

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>mtiririko mzuri wa usomaji wa Kanuni hizi.</p> <p>2. <b>Jedwali la Tano</b> limerejea kuanzishwa chini ya <b>Kanuni ya 19(3)</b>.</p> <p><b>Tatizo</b> <b>Kanuni ya 19(3)</b> haihusiani na Jedwali la Tano badala ya <b>Kanuni ya 18(3)</b>. Hali hiyo inasababisha kukosekana kwa mtiririko mzuri wa usomaji wa Kanuni hizi.</p>	<p>2. <b>Jedwali la Tano</b> lifanyiwe marekebisho kwa kufuta rejea ya <b>Kanuni ya 19(3)</b> na badala yake kurejea <b>Kanuni ya 18(3)</b></p>	<p><b>Athari za Marekebisho</b> Marekebisho yaliyofanyika yamewezesha uwepo wa mtiririko mzurii wa usomaji wa kanuni hizi.</p> <p>2. Azimio la Bunge limetekelizwa kwa kufanya marekebisho katika Jedwali la Tano ili kufuta rejea ya <b>Kanuni ya 19(3)</b> na badala yake kurejea <b>Kanuni ya 18(3)</b>.</p> <p><b>Athari za Marekebisho</b> Marekebisho</p>	<p>2. Mchakato wa Marekebisho umekamilika na kuchapishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 31 la tarehe 20 Januari, 2023</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
				yaliyofanyika yamewezesha uwepo wa mtiririko mzuri wakati wa usomaji wa kanuni hizi.	
14.	<i>The Mining (Government Minerals Warehouse) Regulations (TS Na. 58 28/01/2022)</i>	<p>1. Makosa ya kurejewa kwa Kanuni ya 24 (6) katika <b>Fomu Na. 3</b> kwenye Jedwali la Kwanza.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni iliyorejewa haihusiani na maudhui ya Fomu Na. 3. Kanuni sahihi ni 24 (5) ambayo ni mahsus kwa ajili fomu ya kuweka/ kutoa madini.</p> <p>Kosa hilo la kutokurejea Kanuni sahihi, linasababisha changamoto katika mtiririko wa usomaji</p>	<p>1. <b>Fomu Na. 3</b> katika Jedwali la Kwanza ifanyiwe marekebisho ili kufuta Kanuni Ndogo ya (6) na badala yake kufanya rejea ya Kanuni Ndogo ya (5).</p>	<p>1. Azimio la Bunge limetekelizwa kwa kufanya marekebisho katika Jedwali la Kwanza la Kanuni za <i>The Mining (Government Minerals Warehouse) Regulations</i> ili kufuta kanuni ndogo ya (6) iliyorejewa katika Fomu Na. 3.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Marekebisho yaliyofanyika yanaondoa changamoto katika mtiririko wa usomaji</p>	<p>1. Mchakato wa Marekebisho umekamilika na kuchapishwa kuitia Tangazo la Serikali Na. 31 la tarehe 20 Januari, 2023</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		kutoka kanuni inayohusika kwenda Fomu Na. 3 katika Jedwali la Kwanza Athari za changamoto hiyo ni inataabisha tija ya kanuni kufafanua sheria mama.		kutoka kanuni inayohusika.	
		<p>2. Luga ya Kiingereza imetumika kwa pamoja na luga ya Kiswahili katika Fomu Na. 3 kwenye Jedwali la Kwanza tofauti na ilivyo kwenye fomu nyingine za Jedwali hilo.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>(i) Ingawa Fomu Na. 3 na Fomu Na. 1 zinamlenga mhusika mmoja, lakini, zimetofautiana matumizi ya lugha ili hali mantiki ya lugha zake</p>	<p>2. <b>Fomu Na. 3</b> katika Jedwali la Kwanza ifanyiwe marekebisho ili kufuta maneno ya Kiswahili.</p>	<p>2. Azimio la Bunge halijatekelezwa</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b></p> <p>Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa maelezo kuwa, matumizi ya lugha ya Kiswahili katika fomu Na. 3 ni kurahisisha matumizi ya Fomu hiyo kwa walengwa wa watumiaji wa fomu hiyo hata hivyo, ufanuzi wa kina kuhusu matumizi ya lugha hiyo yatatolewa na</p>	<p>Azimio la Bunge litekelezwe kufikia tarehe 14 Februari, 2023</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>inapaswa kulingana.</p> <p>(ii) Kutofautiana kwa mtindo wa matumizi ya lugha katika Kanuni hiyo ni jambo linalokanganya mtiririko na mantiki ya uandishi.</p>		<p>Mwandishi Mkuu wa Sheria.</p> <p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b></p> <p>Iwapo marekebisho yatafanyika, yataondoa changamoto ya mkanganyiko uliojitokeza na kuleta mtiririko mzuri na mantiki bora ya uandishi.</p>	
15.	<p>The Tax Administration (Administration of Tax Ombudsman Service) Regulations, 2022  <b>(TS Na. 105 5/2/2022)</b></p>	<p><b>Kanuni ya 6</b> inakataza mtu aliyeajiriwa kama mchunguzi maalumu wa masuala ya kikodi (ombudsman) kuwa katika shughuli nyingine ambayo ina masharti ya malipo ya mshahara.</p> <p>Hata hivyo, Kanuni hiyo hazifafanui kazi zinazokatazwa kugusia kazi</p>	<p><b>Kanuni ya 6</b> ifanyiwe marekebisho ili kuonesha ufanuzi wa kazi zinazokatazwa kufanywa na mchunguzi maalumu wa masuala ya kikodi kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kuingiliana majukumu na anayoyatekeleza.</p>	<p>Azimio la Bunge limetekelawa katika Kanuni ya 6 kwa kufanya marekebisho ili kuweka sharti kwa Mchunguzi wa Kodi kutofanya kazi zinazoweza kuwa na mgongano wa kimaslahi na majukumu ya Ofisi ya Msuluhishi wa Kodi.</p> <p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b></p> <p>Marekebisho</p>	<p>Mchakato wa Marekebisho umekamilika na kuchapishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 787 la tarehe 30 Desemba, 2022</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>zinazoingiliana na majukumu yanayotekelawa na mchunguzi wa masuala ya kikodi.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kutokufafanua kazi zinazokatazwa kwa kuzingatia masharti ya katazo hilo kuwa ni kuhusiana na masuala ya kikodi, kunamtatanisha mchunguzi anayehusika. Hali hiyo ni tofauti na lengo la Bunge kutunga Sheria mama iliyolenga kurahisisha taratibu za kikodi.</p>		<p>yaliyofanyika yanakamilisha lengo la Bunge kutunga Sheria mama iliyolenga kurahisisha taratibu za kikodi.</p>	
16.	The Tax Administration (Tax Ombudsman Service)	<p>1. <b>Kanuni ya 2</b> inatafsiri neno lalamiko la kikodi "Complaint" na kuonesha kuwa</p>	<p>1. <b>Kanuni ya 4(2)</b> ifanyiwe marekebisho ili kutambua njia ya</p>	<p>1. Azimio la Bunge limetekelawa kwa kufanya marekebisho katika</p>	<p>1. Mchakato wa Marekebisho umekamilika na kuchapishwa kupitia Tangazo la Serikali</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	Complaint Procedure) Regulations, 2022 <b>(TS Na. 106</b> <b>25/2/2022)</b>	litawasilishwa kwa Ombudsman kwa njia ya maneno, maandishi au kielektroniki.  <b>Tatizo</b> <b>Kanuni ya 4(2)</b> imetambua njia ya maneno na maandishi pekee kwa ajili ya kuwasilisha malalamiko ya kikodi. Kutokutambua njia ya kielektroniki kuwa mionganini mwa njia za kuwasilisha malalamiko kwa mchunguzi maalumu, inawatatanisha wahuksika wanaotaka kutoa malalamiko ya kikodi.	kielektroniki kama moja ya zitazotumika kuwasilisha malalamiko ya kikodi.	Kanuni ya 4(2) ili kutambua njia ya kielektroniki kama moja ya njia zitazotumika kuwasilisha malalamiko ya kikodi.  <b>Athari ya Marekebisho</b> Marekebisho yaliyofanyika yanatoa fursa kwa wahusika wanaotaka kutoa malalamiko ya kikodi kutumia njia zote tatu zilizoainishwa na kanuni hizi.	Na. 786 la Tarehe 30 Desemba, 2022
	2. <b>Kanuni ya 11</b> inaeleza kuwa Waziri	2. <b>Kanuni ya 11</b> ifanyiwe	2. Azimio la Bunge limetekelizwa kwa	Mchakato wa Marekebisho	

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>atakapopokea mapendekozo ya Ombudsman atatoa maelekezo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuhusu namna ya kufanya kazi mapendekozo hayo.</p> <p><b>Tatizo</b> Kanuni haijaonesha muda mahsus wa ambao Waziri atoa maelekezo kwa Mamlaka kuhusu ya utekelezaji wa mapendekozo.</p>	<p>marekebisho ili ioneshe muda mahsus amba Waziri atoa maelekezo kwa Mamlaka kuhusu ya utekelezaji wa mapendekozo.</p>	<p>kufanya marekebisho katika Kanuni ya 11 ili kuonesha muda wa siku thelathini ambao Waziri atatoa maelekezo kwa Mamlaka kuhusu ya utekelezaji wa mapendekozo.</p>	<p>umekamilika na kuchapishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 786 la Tarehe 30 Desemba,2022</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
<b>WIZARA YA NISHATI</b>					
17.	The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Products Price Setting) Rules <b>(TS Na. 57 28/01/2022)</b>	<p>Kanuni ya 8 (3) inaweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja ikiwa mtu atatiwa hatiani kwa kosa la kutoitika wito uliotolewa na EWURA.</p> <p>Adhabu inayowekwa na Kanuni ya 8(3) ipo kinyume na adhabu inayowekwa na Kifungu cha 18(5) cha Sheria Mama ya faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na tano au adhabu zote pamoja.</p> <p>Dosari ya sheria ndogo kukinzana na Sheria Mama ni kinyume cha Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1.</p>	<p>Kanuni ya 8 (3) ifanyiwe marekebisho ili kuendana na adhabu iliyowekwa na sheria mama.</p>	<p>Kanuni ya 8 (3) imefanyiwa marekebisho ili kuendana na adhabu iliyowekwa na sheria mama kama ilivyopendekezwa na Kamati.</p> <p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b> Marekebisho yaliyofanyika yatasaidia ufanikishaji wa lengo la Sheria Mama la kulinda usalama wa watumiaji na ubora wa bidhaa.</p>	Marekebisho yamefanyika kupitia Tangazo la Serikali Na. 207/2022 lililochapishwa tarehe 15/4/2022.
18.	The Electricity (Electrical	1. Kanuni zinaweka	1. <b>Kanuni ya 6</b> ifanyiwe	1. Rasimu ya Marekebisho	1. Marekebisho yapo katika hatua ya

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
	<p>Installation Services) Rules, 2022 <b>(TS Na. 113 4/3/2022)</b></p> <p><b>Tatizo</b> Kutokulindwa kwa wenyewe leseni wa ndani ya nchi.</p>	<p>masharti yanayofanana kwa waombaji wa leseni za kuunganisha umeme ambao ni raia wa Tanzania na waombaji ambao si raia wa Tanzania.</p>	<p>marekebisho ili kuongeza sharti la leseni ambazo zitaombwa na wenyewe leseni wa ndani pekee.</p>	<p>imeandaliwa kwa kuongeza kanuni ndogo ya nne (4) katika kanuni ya 7 ili kufanya leseni za madaraja ya S3, D na C kuwa za wazawa tu.</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b> Wizara ilitoa maelezo kwamba, Maboresho haya yaliwasilishwa kwenye Kamati ya Bodi ya Sheria na Fedha tarehe 19 Desemba 2022 ambayo imeyapitia na kuruhusu Kanuni ziende kwa wadau kwa ajili ya kupatiwa maoni. Kikao cha wadau kinakusudiwa kufanyika tarehe 13 Januari, 2023. Baada ya hapo,</p>	<p>kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
				<p>kanuni zitawasilishwa Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa na kwa Mwandishi wa Sheria kwa ajili ya hatua zaidi ikiwemo upekuzi na uchapishaji.</p> <p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b> Kukamilika kwa mabadiliko haya kutawapa rai raia wa Tanzania na kuwalindia fursa katika masuala ya umeme.</p> <p><b>2. Kanuni ya 13(4)</b> inaeleza kuwa, Mamlaka itakapositisha leseni, itamfahamisha mhusika kwa maandishi kuhusu muda ambao leseni</p> <p><b>2. Kanuni ya 13</b> ifanyiwe marekebisho ili kuonesha muda mahsusii ambao leseni inaweza kuwa imesitishwa.</p> <p><b>2. Rasimu ya Marekebisho</b> Kanuni ya 13(4) imeandaliiwa kwa kuweka ukomo wa usitishwaji leseni kuwa miezi 12</p>	<p>2. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>hiyo imesitishwa.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni haijaonesha muda mahsusini wa usitishwaji wa leseni. Hali hiyo inaweza kusababisha usitishaji leseni usiofuata miongozo.</p>		<p><b>Maelezo ya Wizara</b></p> <p>Wizara ilitoa maelezo kwamba, Maboresho haya yaliwasilishwa kwenye Kamati ya Bodi ya Sheria na Fedha tarehe 19 Desemba 2022 ambayo imeyapitia na kuruhusu Kanuni ziende kwa wadau kwa ajili ya kupatiwa maoni. Kikao cha wadau kinakusudiwa kufanyika tarehe 13 Januari, 2023. Baada ya hapo, kanuni zitawasilishwa Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa na kwa Mwandishi wa Sheria kwa ajili ya hatua zaidi ikiwemo upukuzi na uchapishaji.</p>	

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p><b>3. Kanuni ya 19(3)</b> inaweka masharti kwa Mwenye Leseni ya kuunganisha umeme kumpatia mteja wake cheti kama kinavyooneshwa kwenye Jedwali la Nne la Kanuni, baada ya kukamilisha Ukaguzi wa miundombinu ya Umeme.</p> <p><b>Tatizo</b>  <b>Jedwali la Nne</b> linalorejewa katika <b>Kanuni ya 19(3)</b></p>	<p><b>3. Jedwali la Nne</b> lifanyiwe marekebisho ili kuonesha aina ya cheti kinachotajwa na <b>Kanuni ya 19(3)</b>.</p>	<p><b>Athari ya Marekebisho</b>  Iwapo marekebisho yatakamilika, yatasaidia kuondoa usitishwaji wa leseni usiokua na muongozo maalum.</p> <p><b>Maelelezo ya Wizara</b>  Wizara ilitoa maelezo kwamba, Maboresho haya yaliwasilishwa kwenye Kamati ya Bodi ya Sheria na Fedha tarehe 19</p>	<p>3. Rasimu ya Kanuni ya 19(3) pamoja na Jedwali la Nne imeandaliwa kwa kuondoa matumizi ya neno "Cheti" na badala yake kutumia neno "Taarifa".</p> <p>3. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>halioneshi aina ya cheti kinachohusika na badala yake kuna maelekezo ya kuambatisha maelekezo yanayoonesha upungufu uliobainika. Hali hiyo inatatiza uelewekaji wa masharti na hivyo kuathiri ufanisi katika utekelezaji wa Sheria Mama.</p>		<p>Desemba 2022 ambayo imeyapitia na kuruhusu Kanuni ziende kwa wadau kwa ajili ya kupatiwa maoni. Kikao cha wadau kinakusudiwa kufanyika tarehe 13 Januari, 2023. Baada ya hapo, kanuni zitawasilishwa Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa na kwa Mwandishi wa Sheria kwa ajili ya hatua zaidi ikiwemo upekuzi na uchapishaji.</p> <p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b>  Marekebisho haya yakikamilika yataondoa utata na kusaidia uelewekaji masharti</p>	

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>4. <b>Kanuni ya 4</b> imeweka wajibu wa kuomba na kupata leseni kwa ajili ya kufanya shughuli ya kuunganisha umeme. Katika kukazia wajibu huo, <b>Kanuni ya 4(2)</b> inatambua shughuli ya kuunganisha umeme inayofanyika tofauti na masharti yanayotaka kuwa na leseni kuwa ni kosa. Hivyo, inaweka adhabu ya faini isiyozidi shillingi milioni moja au kifungo ha muda usiozidi miaka mitano au vyote.</p>	<p>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka adhabu inayoendana na Sheria Mama.</p>	<p>na hivyo kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa Sheria Mama.</p> <p>4. Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni ya 4(2) imeandaliwa kwa kuweka adhabu ya shillingi milioni 10 ambayo ipo kwenye Sheria Mama.</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b></p> <p>Wizara ilitoa maelezo kwamba, Maboresho haya yaliwasilishwa kwenye Kamati ya Bodi ya Sheria na Fedha tarehe 19 Desemba 2022 ambayo imeyapitia na kuruhusu Kanuni ziende kwa wadau</p>	<p>4. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>Vilevile <b>Kanuni ya 21(1)</b> inaweka adhabu ya faini ya shilingi laki mbili kwa mwenye leseni anayefanya kazi ya kuunganisha umeme iliyo nje ya wigo wa leseni yake.</p> <p>Kwa kawaida, leseni ni idhini maalumu kutoka kwenye mamlaka inayohusika ili kufanya shughuli au kazi mahususi. Shughuli au kazi yoyote nje ya idhini hiyo au bila ya idhini hiyo inahesabika kufanyika bila leseni.</p> <p>Kanuni hizi zimetungwa chini ya <b>Kifungu cha 8(3), 33(2)(b) na 45. Kifungu cha 8 (1) (h)</b> kinaweka sharti la kuwa na leseni</p>		<p>kwa ajili ya kupatiwa maoni. Kikao cha wadau kinakusudiwa kufanyika tarehe 13 Januari, 2023. Baada ya hapo, kanuni zitawasilishwa Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa na kwa Mwandishi wa Sheria kwa ajili ya hatua zaidi ikiwemo upekuzi na uchapishaji.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho.</b></p> <p>Ukamilifu wa marekebisho haya utasaidia kuondoa mkanganyiko uliobainika na kupelekea azma ya mamlaka ya Bunge katika utungaji wa sheria ndogo</p>	

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kwa ajili ya kufanya kazi au shughuli za kuunganisha umeme.</p> <p>Vilevile <b>Kifungu 8(3)</b></p> <p>kinaitaka EWURA</p> <p>kutunga Kanuni</p> <p>zinazoweka utaratibu wa kuomba leseni.</p> <p>Aidha, <b>Kifungu cha 8(5)</b> kinatilia nguvu masharti yote yaliyowekwa katika <b>Kifungu cha 8</b> kwa kutaja adhabu ya shilingi zisizozidi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja kwa kosa la kukiuka maelekezo kuhusu leseni.</p> <p><b>Tatizo</b> <b>Kanuni ya 4(2) na</b></p>		<p>isiyokinzana na sheria mama inatimizwa.</p>	

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<b>21(1)</b> zinazuia kutolewa kwa adhabu kwa kiwango kilichowekwa na Sheria Mama dhidi ya ukiukaji wa maelekezo kuhusu leseni.			
19.	The Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations) Rules, 2022 <b>(TS Na. 150</b> <b>25/3/2022)</b>	<p><b>Kanuni ya 8</b> inaelekeza kuwa, kibali cha ujenzi kilichotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji kitasita/kitakoma iwapo aliyepatiwa kibali kinachohusika ameshindwa kuanza ujenzi ndani ya miezi ishirini na nne tangu kutolewa kwa kibali kinachohusika.</p> <p><b>Tatizo</b> Kanuni haioneshi yafuatayo:- (i) Mazingira</p>	<p>Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuongeza sharti litakalomwezesha mtu kupatiwa muda wa ziada iwapo atatoa sababu za msingi za kushindwa kuanza ujenzi ndani ya muda ulipo katika kibali.</p>	<p>Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni ya 8 imeandaliwa kwa kuiwezesha EWURA kutoa muda wa ziada kwa mtu aliyepewa kibali cha ujenzi. Aidha, Kanuni hiyo imeeleza vigezo ambavyo vitazingatiwa na EWURA kabla ya kutoa muda wa ziada. Kanuni pia imeboreshwa kwa kuwekwa kwa sababu za kushindwa kuanza ujenzi kwa kipindi</p>	<p>Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>yanayomwezesha aliyepewa kibali kuonesha sababu za kushindwa kuanza ujenzi kwa kipindi kilichopangwa; na</p> <p>(ii) Uwezekano wa kuongeza muda wa nyongeza kwa kibali kilichotolewa ikiwa mhusika atatao sababu zinazojitosheleza.</p> <p>Kukosekana kwa masharti hayo kunaweza kusababisha hasara kwa mwekezaji aliyepata kibali akashindwa kuanza ujenzi kwa sababu za msingi.</p>		<p>kilichopangwa.</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b> Wizara ilitoa maelezo kwamba, Maboresho haya yaliwasilishwa kwenye Kamati ya Bodi ya Sheria na Fedha tarehe 19 Desemba 2022 ambayo imeyapitia na kuruhusu Kanuni ziende kwa wadau kwa ajili ya kupatiwa maoni. Kikao cha wadau kinakusudiwa kufanyika tarehe 13 Januari, 2023. Baada ya hapo, kanuni zitawasilishwa Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa na kwa Mwandishi wa Sheria kwa ajili ya hatua zaidi ikiwemo upekuzi na uchapishajji.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b> Marekebisho haya</p>	

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
				<p>iwapo yatakamilika, yatatoa nafasi ya kuendelea na ujenzi kwa wawekezaji walioshindwa kuanza ujenzi huo kwa sababu za msingi na kuwaepusha na hasara zitakazojitokeza ikiwa nafasi hio isingekuwepo.</p>	

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

20.	<p>Kanuni za Anwani za Makazi katika Mamlaka za Miji za Mwaka, 2022 <b>(TS Na. 109 25/2/2022)</b></p>	<p>1. <b>Kanuni ya 8(a)</b> inaweka wajibu kwa Katibu Tawala wa Mkoa kupokea Taarifa ya utekelezaji wa anwani za makazi ya kila robo mwaka kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya. Ingawa Kanuni hiyo inamtaka Katibu Tawala wa Mkoa atakapopokea</p>	<p>1. Marekebisho yatanyike katika Kanuni ya 8(a) kwa kuondoa maneno “<b>Katibu Tawala wa Mkoa</b>” na na badala yake kuweka “<b>Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI</b>” Ili kumtaka Katibu Tawala wa Mkoa mara baada ya kupokea taarifa</p>	<p>1. Rasimu ya Marekebisho ya <b>Kanuni ya 8 (a)</b> imeandaliwa kwa kuondoa maneno “<b>Katibu Tawala wa Mkoa</b>” na na badala yake kuweka “<b>Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tamisemi</b>” Ili kumtaka Katibu Tawala wa Mkoa</p>	<p>1. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>
-----	---	---	--	--	---

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>Taarifa hiyo aiwasilishe kwa Katibu Tawala wa Mkoa.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni haioneshi daraja la juu ya ambalo Katibu Tawala atawasilisha Taarifa hiyo baada kuwa ameipokea kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya.</p> <p><b>2. Kanuni ya 8(b)</b> inaeleza kuwa uamuzi utakaotolewa na Katibu Tawala kwenye shauri la rufaa utakuwa ni wa</p>	<p>kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu.</p> <p><b>2. Kanuni ya 8(b)</b> ifanyiwe marekebisho ili kuonesha fursa ya kukataa rufaa katika vyombo vyaa juu</p>	<p>mara baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Marekebisho haya iwapo yatakamilika yataondoa mkanganyiko kuhusu daraja la juu ya ambalo Katibu Tawala atawasilisha Taarifa hiyo baada kuwa ameipokea kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya</p> <p><b>2. Rasimu ya Marekebisho <b>Kanuni ya 8(b)imeandaliwa</b></b> kwa kufuta masharti ya ukomo wa rufaa ya</p>	

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>mwisho.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni inaminya haki za watusika ambao hawataridhika na uamuzi wa Katibu Tawala wa Mkoa.</p> <p>3. <b>Kanuni ya 22 (b)</b> haiendani na masharti yaliyokusudiwa katika <b>Kanuni ya 8</b> inayorejelewa. Kanuni hizi zikisomwa kwa pamoja, Katibu Tawala wa Mkoa anatakiwa kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku saba</p>	<p>iwapo mtu hajaridhishwa na uamuzi wa Katibu Tawala.</p> <p>3. Marekebisho yafanyike ili kurekebisha <b>kifungu cha 22 (b)</b> kwa kufuta maneno “<b>Katibu Tawala wa Mkoa</b>” baada ya maneno “<b>Uamuzi wa na kuweka badala yake</b>” maneno “<b>Katibu Tawala wa</b></p>	<p>uamuzi wa Katibu Tawala wa Mkoa ni wa kiutawala.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Marekebisho haya iwapo yatakamilika yatawezesha uwepo wa haki ya rufaa kwa watusika ambao hawataridhika na uamuzi wa Katibu Tawala wa Mkoa.</p> <p>3. Rasimu ya Marekebisho ya <b>kifungu cha 22 (b)</b> imeandaliwa kwa kufuta maneno “<b>Katibu Tawala wa Mkoa</b>” baada ya maneno “<b>Uamuzi wa na kuweka badala yake</b>” maneno “<b>Katibu</b></p>	<p>Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p> <p>3. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kuanzia tarehe ya uamuzi wa Katibu Tawala wa Wilaya, ingawa <b>Kanuni ya 22(b)</b> imemtaja Katibu Tawala wa Mkoa.</p> <p><b>Tatizo la Kwanza</b>  <b>Kanuni ya 22(b)</b>          haibainishi madaraja ya ukataji wa rufaa kutoka kwa Katibu Tawala Wilaya</p> <p><b>Tatizo la Pili</b>  <b>Kanuni ya 22(b)</b>          inavyosomeka sasa inakinzana na misingi asili ya utoaji haki, kwa kumpa Katibu Tawala wa Mkoa uwezo wa kupokea rufaa dhidi ya uamuzi alioutoa mwenyewe.</p>	<p><b>Wilaya".</b></p>	<p><b>Tawala wa Wilaya".</b></p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b>          Iwapo marekebisho yatakamilika yataondoa mkanganyiko kuhusu madaraja ya ukataji wa rufaa kutoka kwa Katibu Tawala Wilaya. Pia itaondoa tatizo la Sheria Ndogo kukinzana na misingi asili ya utoaji haki yaliyokuwa yakimpa Katibu Tawala wa Mkoa uwezo wa kupokea rufaa dhidi ya uamuzi alioutoa mwenyewe.</p>	

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
21.	Kanuni za Anwani za Makazi katika Mamlaka za Wilaya, 2022 <b>(TS Na. 110 25/2/2022)</b>	<p>1. <b>Kanuni ya 8(a)</b> inaweka wajibu kwa Katibu Tawala wa Mkoa kupokea Taarifa ya utekelezaji wa anwani za makazi ya kila robo mwaka kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya. Ingawa Kanuni hiyo inamtaka Katibu Tawala wa Mkoa atakapopokea Taarifa hiyo aiwasilishe kwa Katibu Tawala wa Mkoa.</p> <p><b>Tatizo</b> Kanuni haioneshi daraja la juu ya ambalo Katibu Tawala atawasilisha Taarifa hiyo baada kuwa ameipokea kutoka kwa Katibu</p>	<p>1. Marekebisho yafanyike katika <b>Kanuni ya 8(a)</b> kwa kuondoa maneno “<b>Katibu Tawala wa Mkoa</b>” na na badala yake kuweka “<b>Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI</b>” ili kumtaka Katibu Tawala wa Mkoa mara baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu.</p>	<p>1. Rasimu ya Marekebisho ya <b>Kanuni ya 8 (a)</b> imeandaliwa kwa kuondoa maneno “<b>Katibu Tawala wa Mkoa</b>” na na badala yake kuweka “<b>Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tamisemi</b>” ili kumtaka Katibu Tawala wa Mkoa mara baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b> Marekebisho haya iwapo yatakamilika yataondoa mkanganyiko</p>	<p>1. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>Tawala wa Wilaya.</p> <p>2. <b>Kanuni ya 8(b)</b> inaeleza kuwa uamuzi utakaotolewa na Katibu Tawala kwenye shauri la rufaa utakuwa ni wa mwisho.</p> <p><b>Tatizo</b> Kanuni inaminya haki za wahusika ambao hawataridhika na uamuzi wa Katibu Tawala wa Mkoa.</p>	<p>2. <b>Kanuni ya 8(b)</b> ifanyiwe marekebisho ili kuonesha fursa ya kukataa rufaa katika vyombo vya juu iwapo mtu hajaridhishwa na uamuzi wa Katibu Tawala.</p>	<p>kuhusu daraja la juu ya ambalo Katibu Tawala atawasilisha Taarifa hiyo baada kuwa ameipokea kutoka kwa Katibu Tawala wa Wilaya.</p> <p>2. Rasimu ya Marekebisho ya <b>Kanuni ya 8(b)</b> imeandaliwa kwa kufuta masharti ya ukomo wa rufaa ya uamuzi wa Katibu Tawala wa Mkoa ni wa kiutawala.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b> Iwapo marekebisho haya yatakamilika yataondoa utata kuhusu utaratibu wa ukataji rufaa dhidi ya uamuzi wa Katibu Tawala wa</p>	<p>2. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>3. <b>Kanuni ya 22 (b)</b> inayorejea <b>Kanuni ya 8</b> haina ufanuzi unaosaidia kwakuwa, <b>Kanuni ya 8</b> pia badala ya kufafanua inarejea <b>Kanuni ya 22(b)</b>.</p> <p><b>Tatizo la Kwanza</b> Kila Kanuni inarejea Kanuni nyingine ilhalii Kanuni zote hazifafanui rufaa inayopokewa na Katibu Tawala wa Mkoa</p> <p><b>Tatizo la Pili</b> <b>Kanuni ya 22(b)</b> haibainishi madaraja ya ukataji wa rufaa kutoka kwa Katibu Tawala Wilaya.</p>	<p>3. Marekebisho yafanyike katika <b>kifungu cha 22 (b)</b> kwa kufuta maneno “<b>Katibu Tawala wa Mkoa</b>” baada ya maneno “<b>Uamuzi wa</b> “ na kuweka badala yake maneno “<b>Katibu Tawala wa Wilaya</b>”.</p>	<p>Mkoa.</p> <p>3. Rasimu ya Marekebisho ya <b>Kanuni ya 22 (b)</b> imeandaliwa kwa kufuta maneno “<b>Katibu Tawala wa Mkoa</b>” baada ya maneno “<b>Uamuzi wa</b> “ na kuweka badala yake maneno “<b>Katibu Tawala wa Wilaya</b>”.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b> Iwapo marekebisho yatakamilika yatondoa mkanganyiko kuhusu madaraja ya ukataji wa rufaa kutoka kwa Katibu Tawala Wilaya. Pia itaondoa tatizo la</p>	<p>3. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p><b><u>Tatizo la Tatu</u></b></p> <p><b>Kanuni ya 22(b)</b></p> <p>inavyosomeka sasa inakinzana na misingi asili ya utoaji haki, kwa kumpa Katibu Tawala wa Mkoa uwezo wa kupokea rufaa dhidi ya uamuzi alioutoa mwenyewe.</p>		<p>Sheria Ndogo kukinzana na misingi asili ya utoaji haki yaliyokuwa yakimpa Katibu Tawala wa Mkoa uwezo wa kupokea rufaa dhidi ya uamuzi alioutoa mwenyewe.</p>	
22	<p>Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, 2022     (TS. Na. 127     4/3/2022)</p>	<p>1. <b>Kifungu cha 3(1)(a)</b></p> <p>kinaweka sharti kuwa mfugaji anayefuga ndani ya Halmashauri atapaswa kufuga mifugo kwa idadi itakayoamuliwa na Halmashauri.</p> <p><b><u>Tatizo la kwanza</u></b></p> <p>Kifungu hakibainishi idadi ya mifugo hiyo;</p> <p><b><u>Tatizo la pili</u></b></p> <p>Masharti ya Kifungu</p>	<p>1. Marekebisho yafanyike kwa kufuta uwezo wa Halmashauri kuamua kuhusu idadi ya mifugo itakayofugwa na mtu anayeishi ndani ya eneo la Halmashauri.</p>	<p>1. Rasimu ya Marekebisho ya <b>Kifungu cha 3 (1) (a) yamefanyika</b> kwa kufuta uwezo wa Halmashauri kuamua kuhusu idadi ya mifugo itakayofugwa na mtu anayeishi ndani ya eneo la Halmashauri.</p> <p><b><u>Athari ya Marekebisho</u></b></p>	<p>1. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>hiki yanaweza kuwa na tafsiri kwamba Halmashauri inawapangia wananchi kiwango cha mali wanachopaswa kumiliki</p> <p><b>2. Kifungu cha 4(1) (a)</b> pamoja na mambo mengine kinaweka sharti kwa mtu anayetaka kufanya shughuli ndani ya Halmashauri kufuata kalenda ya Kilimo ya Halmashauri.</p> <p><b>Tatizo la kwanza</b> Sheria Ndogo haioneshi bayana nini maana ya kalenda</p>		<p>Iwapo marekebisho yatakamilika yataondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza kwa Halmashauri kuamua idadi ya mifugo watakayopaswa kufugwa.</p> <p>2. Marekebisho yafanyike kwa kufuta sharti la mtu anayetaka kufanya shughuli ndani ya Halmashauri kufuata kalenda ya Kilimo ya Halmashauri.</p>	<p>2. Rasimu ya Marekebisho ya <b>Kifungu cha 4 (1) (a)</b> imeandaliwa kwa kufuta sharti kwa mtu anayetaka kufanya shughuli ndani ya Halmashauri kufuata kalenda ya Kilimo ya Halmashauri.</p> <p>2. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

**KIAMBATISHO NA. 1**

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>ya Halmashauri.</p> <p><b>Tatizo la pili</b></p> <p>Masharti yaliyowekwa yana muonekano usiofaa kwa umma kwa kuondoa mnyumbuko wa shughuli za kilimo. Hii ni kutohana na kuwabana wananchi ili watekeleze shughuli za kilimo zilizopangwa na halmashauri.</p>		<p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Ikiwa mchakato wa marekebisho utakamilika utaondoaa tatizo la wanachi kubanwa kutekeleza za shughuli za kilimo kwa kufuata kalenda ya halmashauri.</p>	
23.	<p>Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, 2022 TS Na. 128 4/3/2022)</p>	<p><b>Kifungu cha 14(3)</b></p> <p>kinaeleza kuwa iwapo abiria atatupa takataka nje ya chombo cha usafiri, kosa litachukuliwa kuwa limetendwa mmiliki wa gari au dereva au kondakta na watalazimika kulipa kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini chini ya</p>	<p><b>Kifungu cha 14(3)</b></p> <p>kifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la kuadhibu mtu aliyetenda kosa la kutupa uchafu nje ya chombo cha usafiri.</p>	<p>Rasimu ya Marekebisho ya <b>Kifungu cha 14 (3)</b> imeandaliwa kwa kuweka sharti la kumtaka mkosaji aweze kuadhibiwa kwa kosa alilolifanya.</p> <p><b>Athari ya Marekebisho</b></p> <p>Iwapo marekebisho yatakamilika yatondonaa mkanganyiko kuhusu anayepaswa</p>	<p>Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Kanuni inasubiri mchakato wa kupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki.</p>

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>utaratibu wa kufilisha kosa au kushitakiwa mahakamani.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p><b>Kifungu cha 14 (3)</b></p> <p>kinawapa adhabu watu kwa makosa ya wengine ili hali wanaoadhibiwa hawana namna ya kumzia mkosaji wala sio waliomshawishi mkosaji kutenda kosa.</p>		<p>kuadhibiwa kwa kosa la utupaji wa takataka nje ya vyombo vyua usafiri.</p>	

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAANNA NA MICHEZO**

24.	The Copyright and Neighbouring Rights (Licensing and Rights to Benefit from Re-Sale), Regulations 2022 <b>(TS Na. 137 18/3/2022)</b>	<p><b>1. Kanuni ya 3(1)</b></p> <p>inayohusu leseni kwa ajili ya kutumbuiza kwenye umma, kuzalisha, kutangaza na kuwasiliana na umma kuhusu kazi ya sanaa yenye haki miliki inamzuia mtu kutumbuiza au kuzalisha au</p>	<p>1. Tafsiri ya neno "public performance" ifanyiwe marekebisho ili kutoa tafsiri pana ya maneno "dancing" na "playing"</p>	<p>1. Azimio hallijatekelezwa <b>Maelezo ya Wizara</b></p> <p>Wizara ilifafanua kwamba, kutokutekelezwa kwa Azimio kunatokana na kusubiri kukamilika kwa mfumo mpya wa ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kupitia vyama vyua wasanii (CMOs).</p>	<p>1. Azimio litekelezwe kwa kutoa msukumo wa haraka kuanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kupitia vyama vyua wasanii (CMOs).</p>
-----	---	---	---	---	---

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kutangaza kazi yenyе haki miliki bila leseni ya COSOTA au idhini ya mmiliki wa kazi.</p> <p>Kwa kawaida makatazo yanayowekwa na sheria yanahitaji kusimamiwa na kwamba, usimamizi wake unahitaji kuonekana unatekelezeka.</p> <p>Suala hapa ni iwapo mtu anayevutiwa kucheza muziki “dancing” au kucheza “playing” akiwa kwenye umma kama ilivyofasiliwa katika <b>Kanuni ya 2</b> ya Kanuni hizi atakuwa ametenda kosa na iwapo itakuwa rahisi kudhibiti makosa ya</p>		<p>vyama vyा wasanii (CMOs).</p> <p><b><u>Athari za kutokutekelezwa.</u></b> Kutokutekelezwa ka azimio la Bunge kutaendelea kuleta mkanganyiko kwa watumiaji kw nye tafsiri ya maneno “dancing” na “playing”.</p>	

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>aina hiyo.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni hajafafanua:-</p> <p>(i) Ni aina gani ya kucheza muziki “dancing” kunakokusudiwa; na</p> <p>(ii) Aina gani ya kucheza “playing” kunakosudiwa. Hali hiyo inaweza kusababisha mkanganyiko wa tafsiri wakati wa utekelezaji wa Kanuni hizi.</p> <p>2. <b>Kanuni ya 3(2)(3)</b> inaweka sharti la lazima kuwa, kabla ya kuanza kutumika kwa Mkataba wowote ulioingiwa</p>	<p>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili:-</p> <p>(i) kuondoa sharti la lazima la kuwasilisha</p>	<p>2. Azimio halijatekelezwa</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b></p> <p>Wizara ilitoa maelezo kwamba, Mikataba ya</p>	<p>2. Azimio la Bunge litekelezwe Azimio litekelezwe kwa kutoa msukumo wa haraka kuanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji na</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>nchini Tanzania kati ya mwenye hakimiliki na kampuni au Taasisi, Makataba huo utapaswa kupelekwa COSOTA, ili iupitie na kushauri, ambapo COSOTA itatoza 1% ya thamani ya Mkataba unaohusika kama gharama za huduma iliyotolewa.</p> <p><b>Tatizo la kwanza</b>  Masharti ya Kanuni hii yanalamizimisha kutokuanza kwa makubaliano kati ya wahusika hadi COSOTA itakapoamua. Hii inaweza kutafsiriwa kuwa ni kuingilia makubaliano.</p>	<p>Mkataba COSOTA kabla</p> <p>Mkataba unaohusika haujaanza kufanya kazi;</p> <p>(ii) Kanuni ioneshe utaratibu wa kupidia Mkataba kwa atayetaka kufanya hivyo, ufanyike kabla ya Mkataba unaohusika haujafungwa; na</p> <p>(iii) Kanuni iainishe muda ambao COSOTA itatumia wakati mapitio ya Mikataba inayohusika.</p>	<p>namna hii ni vema kuwasilishwa COSOTA kwa ajili ya ushauri ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ulinzi thabiti wa hakimiliki.</p> <p>Kumekuwepo pia na migogoro mingi na malalamiko mengi ambayo huwasilishwa serikalini kwenye eneo la mikataba hasa pale inapotokea walioingia kwenye mikataba wanaposhindwa kuelewana.</p> <p>Kutokana na kuwa Serikali inakuwa haina taarifa kuhusu mikataba hiyo wala kuwahi kuiona wala kutoa ushauri katika</p>	<p>ugawaji wa mirabaha kupitia vyama vya wasanii (CMOs).</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p><b>Tatizo la pili</b></p> <p>Masharti ya kutaka wahusika kuwasilisha Mkataba COSOTA yanasaababisha kutokutambuliwa kwa Mikataba ilyoingiwa kwa mazungumzo (Oral contracts)</p> <p><b>Tatizo la tatu</b></p> <p>Kanuni haioneshi muda ambao COSOTA itatumia kufanya mapitio ya Mikataba inayohusika.</p> <p>Hali hiyo inaweza kuchelewesha kuanza kwa makubaliano mbalimbali ya kibiashara.</p>		<p>mikataba hiyo, inapelekea Serikali kutumia nguvu nyingi, muda na rasilimali fedha nyingi ili kutatua migogoro hiyo kwa njia ya Amani.</p> <p><b>Athari za kutokutekelezwa</b></p> <p>Kutokutekelezwa ka azimio la Bunge kutaendelea kuleta mkanganyiko kwa watumiaji kwa kuruhusu COSOTA kuendelea kuingilia uhuru wa mikataba. Pia kutokutekelezwa kwa Azimio kutaendelea kuleta mkanganyiko kwenye mikataba itakayoingiwa kwa mdomo (Oral Contracts) na Pia kuendelea kuleta</p>	

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>3. <b>Kanuni ya 10(1)</b> inaipa COSOTA uwezo wa kufuta au <b>kusitisha</b> leseni ya kutumia kazi za wasanii zilizo na haki miliki. Kwa kawaida, kusitisha ni hatua ya kufanya jambo au shughuli fulani isiendelee kufanyika hadi wakati mwingine unaoweza kuwa umebainishwa.</p> <p><b>Tatizo</b> Kanuni hazibainishi ukomo wa usitishwaji wala fursa ya</p>	<p>3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka utaratibu utakaowezesha kurejeshwa kwa leseni ikiwa mhusika aliyesitishiwa leseni atarekebisha kasoro zilizosababisha kusitishwa kwa leseni inayohusika.</p>	<p>mkanganyiko kwenye kujua muda gani COSOTA itautumia kufanya mapitio ya mikataba husika.</p> <p>3. Azimio la Bunge halijatekelezwa</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b> Wizara ilifafanua kwamba, kutokutekelezwa kwa Azimio kunatokana na kusubiri kukamilika kwa mfumo mpya wa ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kuitia vyama vya wasanii (CMOs) ambao pia utashughulikia masuala haya.</p> <p><b>Athari za kutokutekelezwa.</b> Kutokutekelezwa ka</p>	<p>3. Azimio litekelezwe kwa kutoa msukumo wa haraka kuanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kuitia vyama vya wasanii (CMOs).</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kurejeshwa kwa leseni inayohusika, ikiwa mhusika atarekebisha kasoro zilizosababisha kusitishwa leseni hiyo. Athari ya kukosekana kwa sharti la kurejeshwa leseni baada ya kufanya marekebisho ni kuwanyima wahusika fursa ya kuendelea kunufaika na biashara zitokanazo na kazi za wasanii zilizo na haki miliki.</p> <p>4. Kwa ujumla Kanuni hizi zimeweka viwango viwili tofauti vyatilimia ya ghamama za uendeshaji zitakazokatwa na COSOTA kutoka</p>	<p>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka kiwango kimoja cha ukomo wa tilimia za ghamama za uendeshaji.</p>	<p>azimio la Bunge kutaendelea kuleta mkanganyiko kwa watumiaji kwenye kutambua ukomo wa adahabu iwapo mhsuika atarekebisha kasoro zilizosababisha kusitishwa leseni yake.</p> <p>4. Azimio la Bunge halijatekelezwa</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b> Wizara ilifafanua kwamba, kutokutekelezwa kwa Azimio kunatokana na kusubiri kukamilika</p>	<p>4. Azimio litekelezwe kwa kutoa msukumo wa haraka kuanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kupitia vyama vyatilimia (CMOs).</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>katika jumla ya mauzo ya kazi za msanii kabla msanii anayehusika kulipwa mrabaha.</p> <p>Viwango hivyo vimetajwa katika <b>Kanuni ya 25</b> na katika <b>Kipengele cha 4(2)</b> cha <b>Jedwali la Nne</b>.</p> <p>Katika <b>Kanuni ya 25</b> kiwango cha ukomo wa gharama za uendeshaji hazitazidi 35% ya gharama za uendeshaji, wakati <b>Kipengele cha 4 (2)</b> cha <b>Jedwali la Nne</b> ni gharama zisizozidi 30%.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kuwepo kwa viwango viwili vya</p>		<p>kwa mfumo mpya wa ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kupitia vyama vya wasanii (CMOs) ambao pia utashughulikia masuala haya.</p> <p><b><u>Athari za kutokutekelezwa.</u></b></p> <p>Kutokutekelezwa kwa azimio la bunge kutaendelea kuleta mkanganyiko kwa watumiaji katika kutambua ukomo wa asilimia za gharama za uendeshaji.</p>	

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>makato ya aina moja (gharama za uendeshaji)</p> <p>kunaweza kuleta mkanganyiko wa ukokotoaji wa gharama na kusababisha wasanii</p> <p>kukatwa kidogo au zaidi kinyume na ilivyokusudiwa na Sheria Ndogo hii.</p> <p><b>5. Kanuni ya 26 (1)</b> inatoa fursa ya kukata rufaa kwa mtu yeyote ambaye hajaridhika na uamuzi wa COSOTA.</p> <p><b>Tatizo</b> Kanuni hazijaonesha rufaa itakatwa kwa kutumia mfumo au nyaraka ya aina gani</p>	<p>5. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka fomu maalumu kwa ajili ya uwasilishaji wa rufaa.</p>	<p>5. Azimio la Bunge halijatekelezwa <b>Maelezo ya Wizara</b> Marekebisho yatafanyika kwa kutoa ufanuzi wa jinsi mawasiliano hayo ya maandishi yanavyoweza kufanyika kwa kuweka fomu maalumu itakayoonesha taarifa za</p>	<p>5. Bunge Azimio litekelezwe kwa kutoa msukumo wa haraka kuanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kupitia vyama vya wasanii (CMOs).</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>(format). Hali hiyo inaweza kusababisha kutokuelewaka kwa utaratibu wa ukataji rufaa.</p> <p>6. <b>Jedwali la Nne</b> linaonesha kuwa limetokana na Kanuni ya 29 linahusu “distribution rules for public performance and broadcasting” kwa kawaida Kifungu kinachotajwa</p>	<p>6. <b>Jedwali la Nne</b> lifanyiwe marekebisho kwa kufuta Kanuni ya 29 inayorejewa na bdala yake kurejea Kanuni ya 25.</p>	<p>mlalamikaji, malalamiko anayotoa na taarifa ya eneo lake la biashara na maombi mahususi anayofanya.</p> <p><b>Athari ya kutokufanyika</b> Kutokutekelezwa ka azimio la Bunge kutaendelea kuleta mkanganyiko kwa watumiaji kutokujua mfumo gani watatumia kukata rufaa.</p> <p>6. Azimio la Bunge halijatekelezwa</p> <p><b>Maelezo ya Wizara</b> Hoja hii inapokelewa. Makosa ya kiuchapaji yalitokea ambapo Na. 9 iliandikwa badala</p>	<p>6. Azimio litekelezwe kwa kutoa msukumo wa haraka kuanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kupitia vyama vyaya wasanii (CMOs).</p>

## KIAMBATISHO NA. 1

#	Jina la Sheria Ndogo	Changamoto iliyobainishwa	Azimio la Bunge	Hatua iliyofikiwa	Maoni ya Kamati
		<p>kuanzishwa kwa Jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha msomaji kwenye Jedwali linalohusika.</p> <p><b>Tatizo</b>  <b>Jedwali la Nne</b>  linarejea kuanzishwa chini ya Kanuni <b>ya 29</b> ambayo maudhui yake hayahusiani <b>Jedwali</b> hilo.</p>		<p>ya Na. 5. Kwa mantiki hiyo, marekebisho yatafanyika ili kutaja Kanuni ya 25 ambayo naiyo inayohusuhu <i>Distribution of Royalties</i> badala ya kanuni ya 29.</p> <p><b>Athari za Marekebisho</b>  Kutokontaktelezwa ka azimio la Bunge kutaendelea kuleta mkanganyiko kwa kuondoa mtiririko mzuri wa usomaji.</p>	

Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb.

**MWENYEKITI**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo**

8 Februari, 2023

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO

JEDWALI LA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KATIKA  
MKUTANO WA NANE NA MKUTANO WA TISA.

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
<b>SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA NANE WA BUNGE</b>						
1.	(TS Na. 216) 15/04/2022	Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022	Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287) <i>(Imetungwa chini ya kifungu cha 153)</i>	Ofisi ya Rais TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungu cha 14(3)</b> kinaeleza kwamba, iwapo abiria atatupa taka nje ya chombo cha usafiri, kosa litachukuliwa kuwa limetendwa na mmiliki wa gari au dereva au kondakta. Aidha, kinaelekeza kuwa watu hao watalazimika kulipa kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushitakiwa mahakamani.</p> <p><b>Tatizo</b> <b>Kifungu cha 14 (3)</b> kinawapa adhabu</p>	<p>1. <b>Kifungu cha 14(3)</b> kifanyiwe Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii ili kumtaka mkosaji mwenyewe aweze kuadhibiwa kwa kosa alilolifanya.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>watu kwa makosa ya wengine.  Wanaodhibiwa  hawana namna ya kumzuia mkosaji halisi  na wala sio waliomshawishi  mkosaji kutenda kosa.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 14</b>  kinaweka adhabu  kwa mmiliki wa gari  au dereva au  kondakta kulipa kiasi  kisichozidi shilingi elfu  hamsini chini ya  utaratibu wa  kufifilisha kosa au  kushtakiwa  mahakamani ikiwa  abiria anayesarifi  katika chombo chao  cha usafiri atatupa  takataka.</p>	<p>2. <b>Kifungu cha 14</b>  kifanyiwe  marekebisho kwa kubainisha adhabu  mahususi kwa kosa  mahususi chini ya kanuni hii ili  kuondoa mkanganyiko  wakati utekelezaji wa  kanuni hizi.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>Aidha, kifungu cha 23 kinatoa adhabu ya jumla kwa mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote viwili kwa pamoja.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Sheria Ndogo imeweka adhabu mahsus i kwa makosa, lakini pia inaweka adhabu ya jumla kwa kosa lolote liliotendwa chini ya Sheria Ndogo hizi.</p> <p>Hali hii inaweza kuleta mkanganyiko wakati</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					wa utekelezaji kuhusu adhabu inayostahili kuadhibiwa mtu aliyeziuka masharti ya Sheria Ndogo hizi.	
2.	<b>(TS Na. 217) 15/04/2022</b>	Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, (Sura ya 290)  Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)	Ofisi ya Rais TAMISEMI	<p><b>Kifungu cha 8</b> kinachohusu muda wa kusafirisha mazao kinaonesha mtu yejote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kusafirisha mazao kuanzia saa 1:00 jioni hadi saa 12:00 asubuhi.</p> <p><b>Tatizo</b> Kifungu kimekosa ukamilifu wa sentensi, hivyo hakipo wazi kuhusu muda uliotajwa iwapo ni wa kusafirisha au unaokataza kusafirisha.  Kutokukamilika kwa</p>	<p><b>Kifungu cha 8</b> kifanyiwe Marekebisho ili kubainisha muda mahsusili uliokusudiwa na kanuni hizi wakati wa usafirishaji wa mazao.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					sentensi na maelezo kuhusu muda wa kusafirisha mazao kunatatanisha masharti hayo kuhusu muda.	
3.	<b>(TS Na. 219) 15/04/2022</b>	Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022	Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287) <i>(Imetungwa chini ya kifungu cha 153)</i>	Ofisi ya Rais TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungu cha 3(1) (a)</b> kinaweka sharti kuwa mfugaji anayefuga ndani ya Halmashauri atapaswa kufuga mifugo kwa idadi itakayoamuliwa na Halmashauri.</p> <p><b>Tatizo la kwanza</b> Kigezo cha idadi ya mifugo kuamuliwa na Halmashauri hakina uhalisia.</p> <p><b>Tatizo la pili</b> Masharti ya Kifungu hiki yanaweza kuwa na tafsiri kwamba,</p>	<p>1. <b>Kifungu cha 3(1) (a)</b> kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa mamlaka ya Halmashauri kuamua kuhusu idadi ya mifugo itakayofugwa na mtu anayeishi ndani ya eneo la Halmashauri hiyo.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>Halmashauri inawapangia wananchi kiwango cha mali wanachopaswa kumiliki jambo ambalo linaacha ukakasi.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 4(1) (a)</b> pamoja na mambo mengine kinaweka sharti kwa mtu anayetaka kufanya shughuli ya kilimo ndani ya Halmashauri kuftuata kalenda ya Kilimo ya Halmashauri.</p> <p><b><u>Tatizo la kwanza</u></b> Sheria Ndogo haioneshi bayana nini maana ya kalenda ya Halmashauri. Hali</p>	<p>2. <b>kifungu cha 4(1) (a)</b> kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa sharti la mtu anayetaka kufanya shughuli ndani ya Halmashauri kuftuata kalenda ya Kilimo ya Halmashauri.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>hiyo, inasababisha kutokuelewaka vizuri kwa sheria, jambo linaloweza kuwaathiri wananchi wakati wa utekelezaji.</p> <p><b><u>Tatizo la pili</u></b>  Masharti yaliyowekwa yana muonekano usiofaa kwa umma kwa kuondoa mnyumbuko wa shughuli za kilimo. Hii ni kutokana na kuwabana wananchi ili watekeleze shughuli za kilimo zilizopangwa na halmashauri.  Hali hiyo, inaweza kufifiza juhudii za uzalishaji zinazofanywa na wananchi.</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
4.	<b>(TS Na. 224) 15/04/2022</b>	Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, 2022	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura 290)  (Imetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))	Ofisi ya Rais TAMISEMI	<b>Sehemu H ya Jedwali la Kwanza</b> inabainisha viwango vya ushuru wa kituo cha mabasi kwa mchanganuo ufuatao:- (i) Basi la abiria zaidi ya 40 (basi kubwa) litalipiwa shilingi 1000/-;  (ii) Basi la abiria ya zaidi ya 20 chini ya 40 (coaster) litalipiwa shilingi 1,000/-;  (iii) Basi la abiria chini ya 20 (Hiace) litalipiwa shilingi 500/-; na  (iv) Magari madogo kama Taksi, Noah na mengine yatlipiwa shilingi 500/-.	<b>Sehemu H ya jedwali la kwanza</b> ifanyiwe marekebisho ili kubainisha muda wa malipo ya ushuru wa kituo cha mabasi uliokusudiwa na kanuni hizi.

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p><b>Tatizo</b></p> <p>Sheria ndogo haijabainisha iwapo viwango vya ushuru vitalipwa kwa siku au kwa tripu au vinginevyo. Kutokubainishwa kwa muda mahsus wa malipo ya ushuru huo kunaweza kusababisha utozaji usiokuwa na mwongozo.</p>	
5.	<b>(TS Na. 228) 22/04/2022</b>	Regulations under The Merchant Shipping (Maritime Labour), 2022	The Merchant Shipping Act, (Sura ya 165) (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 123 na 427)	Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi	<p>1. <b>Kanuni ya 83</b> inaweka adhabu ya jumla, iwapo mtu amekiuka masharti yoyote ya Kanuni ambapo hakuna kanuni mahsus inayoweka adhabu ya kukiuka masharti hayo, mtu huyo atapaswa kulipa faini shilingi za Tanzania ambazo ni</p>	<p>1. <b>kanuni ya 83</b> inayotoa adhabu ya jumla ifanyiwe marekebisho ili kuendana na matakwa ya adhabu ya jumla iliyowekwa na sheria mama.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>sawa na dola 500 au kifungo      kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja.</p> <p>Vilevile <b>Kifungu cha 401</b> cha sheria mama, kimeweka kifungu cha jumla cha adhabu iwapo mtu atakiuka masharti ya sheria hiyo na hakuna kifungu mahsusini kinachoweka adhabu. Mhusika aliyekiuka sheria mama atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania zenye</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>thamani ya dola 1000 za kimarekani au kifungo cha muda usiopungua miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b></p> <p>Adhabu iliyowekwa katika Kanuni inakinzana na adhabu iliyookekwa na Sheria Mama. Kukinzana huko ni kwenye:-</p> <p>(i) Kiasi cha faini kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotajwa katika sheria Mama; na Adhabu ya kifungo</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					inayowekwa na Sheria Ndogo ni kubwa kuliko iliyowekwa katika Sheria Mama.	
6.	<b>(TS Na. 229) 22/04/2022</b>	<i>The Merchant Shipping (Seafarers' Identity Document) Regulations, 2022</i>	The Merchant Shipping Act, (Sura ya 165) (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 427)	Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi	<b>Kanuni ya 26</b> inaweka adhabu ya jumla, iwapo mtu amekiuka masharti yoyote ya Kanuni ambapo hakuna kanuni mahsusii inayoweka adhabu ya kukiuka masharti hayo, mtu huyo atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na dola 200 na isiyozidi shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na dola 500 au kifungo cha miezi sita au adhabu zote kwa pamoja.	<b>Kanuni ya 26</b> inayotoa adhabu ya jumla ifanyiwe marekebisho ili kuendana na matakwa ya adhabu ya jumla iliyowekwa na sheria mama.

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p><b>Kifungu cha 401</b> cha sheria mama, kimeweke kifungu cha jumla cha adhabu iwapo mtu atakiuka masharti ya sheria hiyo na hakuna kifungu mahsusini kinachoweka adhabu. Mhusika aliyeikiuka sheria mama atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania zenyet thamani ya dola 1000 za kimarekani au kifungo cha muda usiopungua miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.</p> <p><b>Tatizo</b> Adhabu iliyowekwa katika Kanuni inakinzana na adhabu ilioowekwa na Sheria Mama. Kukinzana huko ni</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>kwenye:-</p> <p>(i) Kiasi cha faini kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotajwa katika sheria Mama; na</p> <p>Sheria Ndogo imelazimisha adhabu ya miezi sita ili hali Sheria Mama imeruhusu busara ya kuamua adhabu kifungo chini ya miezi sita.</p>	
7.	<b>(TS Na. 230) 22/04/2022</b>	<i>The Merchant Shipping (Continous Discharge Certificate) Regulations, 2022</i>	The Merchant Shipping Act, (Sura ya 165)  (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 123 na 427)	Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi	<p>1. <b>Kanuni ya 21</b> inaweka adhabu ya jumla, iwapo mtu amekiuka masharti yoyote ya Kanuni ambapo hakuna kanuni mahsusii inayoweka adhabu ya kukiuka</p>	<p>1. <b>Kanuni ya 21</b> inayotoa adhabu ya jumla ifanyiwe marekebisho ili kuendana na matakwa ya adhabu ya jumla iliyowekwa na</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>masharti hayo, mtu huyo atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na dola 200 na isiyozidi shilingi za kitanzania ambazo ni sawa na dola 500 au kifungo cha miezi sita au adhabu zote kwa pamoja.</p> <p><b>Kifungu cha 401</b> cha sheria mama, kimeweka kifungu cha jumla cha adhabu iwapo mtu atakiuka masharti ya sheria hiyo na hakuna kifungu mahsusii kinachoweka adhabu. Mhusika aliyeikiuka sheria</p>	<p>sheria mama.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>mama atapaswa kulipa faini ya shilingi za Tanzania zenyet thamani ya dola 1000 za kimarekani au kifungo cha muda usiopungua miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Adhabu iliyowekwa katika Kanuni inakinzana na adhabu ilioowekwa na Sheria Mama. Kukinzana huko ni kwenye:-</p> <p>(i) Kiasi cha faini kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotajwa</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					katika sheria Mama; na (ii) Sheria Ndogo imelazimisha adhabu ya miezi sita ili hali Sheria Mama imeruhusu busara ya kuamua adhabu kifungo chini ya miezi sita.	
8.	<b>(TS Na. 291) 6/05/2022</b>	<i>The Environmental Management (Prohibition of Plastic Carrier Bags and Plastic Bottle Cap Regulations , 2022</i>	The Environmental Management Act, (Sura ya 191) (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 230(2)(f))	Ofisi ya Makamu wa Rais , Muungano na Mazingira	<p>1. <b>Kanuni ya 32</b> inatoa fursa kwa mtu yeyote ambaye hajaridhika na uamuzi wowote uliotolewa chini ya Kanuni hizi ya kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini baada ya uamuzi.</p> <p><b>Tatizo la kwanza</b> Kanuni haijaweka muda mahsus</p>	<b>Kanuni ya 32</b> ifanyiwe marekebisho kwa kubainisha muda mahsus ambao Waziri atautumia kushughulikia shauri la rufaa.

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>ambao Waziri atashughulikia shauri la rufaa.</p> <p>Hali hiyo inaweza kutoa mwanya wa ucheleweshaji wa mashauri ya rufani.</p> <p><b><u>Tatizo la pili</u></b></p> <p>Kanuni hazijaonesha muundo wa hati ya kukata rufaa, jambo linaloacha utatanishi katika ukataji wa rufaa. Hali hiyo inasababisha kutoeleweka kwa namna ya kutumia fursa ya kukata rufaa.</p>	
9.	<b>(TS Na. 294) 13/05/2022</b>	<i>The Foreign Exchange Regulation, 2022</i>	The Foreign Exchange Act (Sura ya 271)  (Zimetungwa chini)	Wizara ya Fedha na Mipango	<p>1. <b>Kanuni ya 3</b> inahusu miamala ya fedha za kigeni, ambapo inazungumzia utaratibu wa kuuza</p>	<p>1. <b>Kanuni ya 3 (1) (b)</b> ifanyiwe marekebisho na kuongezwa maneno “except</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
			ya Kifungu cha 6 (1))		<p>na kununua fedha za kigeni kutoka katika benki, taasisi za fedha na maduka ya kubadilisha fedha.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni inaweka utaratibu wa aina mbili kuhusu namna ya kununua na kuuza fedha za kigeni katika benki, taasisi za kifedha na maduka ya kubadilisha fedha:-</p> <p>(i) <b>Kanuni ya 3(1) (b)</b></p> <p>inampa mtu yeyote uhiari wa kuuza au kununua kiasi chochote cha fedha za kigeni kutoka kwenye benki, ;</p>	<p>an "exporter" baada ya maneno "any person" ili kuondoa mkanganyiko na kuleta uhusiano wa kimaana na sehemu nyine za kanuni hii.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>taasisi ya fedha au maduka ya kubadilisha fedha;</p> <p>(ii) <b>Kanuni ya 3(7)</b> inaweka ulazima kwa msafirishaji wa bidhaa nje ya nchi, kuuza fedha za kigeni katika benki ambayo ana uhusiano wa kiakaunti.</p> <p>Masharti ya yaliyowekwa na katika <b>Kanuni ya 3(7)</b> yanakinzana na <b>Kifungu cha 4 (b)</b> cha Sheria Mama ambacho kinaweka uhiari wa kufungua akaunti ya benki ya fedha za kigeni.</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>2. <b>Kanuni ya 25(7)</b> inatoa adhabu ya malipo ya shilingi milioni moja kwa siku kutokana na kushindwa kuwasilisha nyaraka za mkopo kutoka nje ya nchi baada ya kuisha kipindi cha siku 14.</p> <p><b>Tatizo</b> Adhabu iliyowekwa na Kanuni ya 25(7) haionekani kwa mujibu wa adhabu zinazowekwa na Sheria Mama.</p> <p>3. <b>Kanuni ya 26</b> inaweka utaratibu wa namna ya kusajili mikopo kutoka nje ya nchi. Ambapo pia imeweka vigezo</p>	<p>2. <b>Kanuni ya 25 (7)</b> ifanyiwe marekebisho ya adhabu iliyotajwa ili na kanuni hii ili kuendana na adhabu zilizo ainishwa na sheria mama.</p> <p>3. <b>Kanuni ya 26 (3)</b> ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa utashi wa kuongeza vigezo vingine</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>vitakavyozingatiwa ili kuisajili au kutoisajili mikopo hiyo.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni imetoa utashi wa kuongeza vigezo vingine vitavyozingatiwa wakati wa kusajili mkopo pasipo kuvianisha.</p> <p>4. <b>Kanuni ya 26</b> imeandikwa kwa mpangilio unaoanza kwa kutaja vigezo vitakavyozingatiwa wakati wa kusajili mkopo kutoka nje ya nchi. Ikifuatiwa na maelezo ya jumla ambayo yanaweka katazo kwa benki kutokusajili mikopo</p>	<p>vitakavyozingatiwa wakati wa kusajili wa mikopo ya nje na kuitaka mamlaka husika kutangaza vingezo vingine vilivyotumika katika kukataa usajili wa mikopo ya nje kwenye gazeti.</p> <p>4. <b>Kanuni ya 26</b> ifanyiwe marekebisho ya mpangilio kwa kuanza na kanuni ndogo ya tatu, ikifuatiwa na kwanza na mbili</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>ambayo haijakidhi masharti yaliyotajwa na <b>Kanuni 26 (1)(2)</b>.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kanuni hiyo haijaandikwa kwa mpangilio. Hali inayoweza kuleta changamoto katika usomaji wake.</p>	
10.	<b>(TS Na. 324) 13/05/2022</b>	Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale, 2022	Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) (Sura ya 287)  (Imetungwa chini ya kifungu cha 153(1))	Ofisi ya Rais TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungu cha 3</b> kinatafsiri neno "Taka hatari" kuwa ni taka ngumu, miminika na hewa ambazo zina kiwango kibubwa cha kemikali ambazo husababisha sumu na kuathiri maisha ya binadamu, viumbe wengine pamoja na mazingira kwa ujumla wake.</p>	<p>1. <b>Kanuni ya 3</b> ifanyiwe marekebisho ili kuendana tafsiri iliyopo kwenye <b>kifungu cha 3</b> cha Sheria Usimamizi wa Mazingira.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p><b>Tatizo</b></p> <p><b>Kanuni ya 3</b> ya Sheria Ndogo itoa tafsiri isiyojitosheleza ya maneno "taka hatarishi" Ikinganishwa na tafsiri pana ya maneno hayo iliyo katika <b>Kifungu cha 3</b> cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.</p> <p>2. Kifungu cha 3 kimetoa ufanuzi kuhusu maana ya ardhi hatari ikihusisha maeneo ya vyanzo vya maji, maeneo ya barabara, maeneo ya miteremko au maeneo yaliyotengwa na</p>	<p>2. <b>Kanuni ya 3</b> ifanyiwe marekebisho kwa kutoa taarifa inayojitoshelea ya neon Hatarishi kama inavobainishwa katika <b>Kifungu cha 3</b> cha Shria mama</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>halmashauri kwa madhumuni yoyote yale.</p> <p><b>Tatizo</b> Kifungu kimetumia neno hatari ambalo linaweza kuleta tafsiri isiyokusudiwa.</p>	(Sheria Usimamizi ya wa Mazingira)
11.	<b>(TS Na. 375) 27/05/2022</b>	Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Mji Wa Bunda, 2022	Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) (Sura ya 288)  (Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 89 (1))	Ofisi ya Rais TAMISEMI	<p>1. Mtiririko wa vifungu vya Sehemu ya Tano vinaanzia <b>Kifungu cha 41</b> hadi <b>Kifungu cha 54.</b></p> <p><b>Tatizo</b> Katika mpangilio huo, Kifungu cha 43 kinakosekana. Hii inaweza kuwa, imetokana na makosa ya kiuchapaji au kusahaulika kwa</p>	<p>1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo kwa kuweka mtiririko unaofaa/mzuri</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>kifungu hicho. Hali inasababisha kutokuwepo kwa ukamilifu wa Sheria Ndogo hii.</p> <p>2. Kifungu cha 15 kinaweka sharti kwa wauzaji wa chakula kutumia masanduku ya mbaو yaliyo na vioo kuhifadhia chakula.</p> <p><b>Tatizo</b> Kifungu kimeweka sharti la matumizi ya masanduku ya mbaو yenye vioo kuhifadhia chakula pasipo kuzingatia uwepo wa masanduku ya aina nyingine.</p>	<p>2. Marekebisho yafanyike ili kutambua aina nyingine za masanduku ya kuhifadhia vyakula.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>3. <b>Jedwali la Kwanza</b>  linaloonesha kuwa  limetokana na  <b>Kifungu cha 25</b>  linahusu ada ya  ukaguzi wa afya. Kwa  kawaida Kifungu  kinachotajwa  kuanzishwa kwa  Jedwali huwa na  maudhui  yanayomrejesha  msomaji kwenye  Jedwali linalohusika.</p> <p><b>Tatizo</b>  <b>Jedwali la Kwanza</b>  linarejea kuanzishwa  chini ya <b>Kifungu cha</b>  <b>25</b> ambacho  maudhui yake  hayahusiani <b>Jedwali</b>  hilo.</p>	<p>3. Marekebisho  yafanyike katika  Sheria Ndogo hii  kwa kuainisha  kifungu  kinachoanzisha  Jedwali husika.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>4. <b>Jedwali la Pili</b>          linaloonesha kuwa limetokana na <b>Kifungu cha 31(1)</b>          linahusu ada ya uzoaji taka kwa kaya, biashara na taasisi.          Kwa kawaida Kifungu kinachotajwa kuanzishwa kwa Jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha msomaji kwenye Jedwali linalohusika.</p> <p><b>Tatizo</b>  <b>Jedwali la Pili</b>          linarejea kuanzishwa chini ya <b>Kifungu cha 31(1)</b> ambacho maudhui yake hayahusiani na <b>Jedwali</b> hilo.</p>	<p>4. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kuainisha kifungu kinachoanzisha Jedwali husika.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>5. <b>Jedwali la Tatu</b>          linaloonesha kuwa          limetokana na  <b>Kifungu cha 45</b>          linahusu ilani ya          kuijenga choo. Kwa          kawaida Kifungu          kinachotajwa          kuanzishwa kwa          Jedwali huwa na          maudhui          yanayomrejesha          msomaji kwenye          Jedwali linalohusika.</p> <p><b>Tatizo</b>  <b>Jedwali la Tatu</b>          linarejea kuanzishwa          chini ya <b>Kifungu cha</b>  <b>45</b> ambacho          maudhui yake          hayahusiani na  <b>Jedwali</b> hilo.</p>	<p>5. Marekebisho          yafanyike katika          Sheria Ndogo hii          kwa kuainisha          kifungu          kinachoanzisha          Jedwali husika.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>6. <b>Jedwali la Nne</b>  linaonesha kuwa  limetokana na  <b>Kifungu cha 47(1)</b>  linahusu ilani  yakuondoa kero. Kwa  kawaida Kifungu  kinachotajwa  kuanzishwa kwa  Jedwali huwa na  maudhui  yanayomrejesha  msomaji kwenye  Jedwali linalohusika.</p> <p><b>Tatizo</b>  <b>Jedwali la Nne</b>  linarejea kuanzishwa  chini ya <b>Kifungu cha 47(1)</b> ambacho  maudhui yake  hayahusiani <b>Jedwali</b>  hilo.</p>	6. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kuainisha kifungu kinachoanzisha Jedwali linalohusika.

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>7. <b>Jedwali la Tano</b>  linaonesha kuwa  limetokana na  <b>Kifungu cha 52</b>  linahusu hati ya kukiri  kosa. Kwa kawaida  Kifungu kinachotajwa  kuanzishwa kwa  Jedwali huwa na  maudhui  yanayomrejesha  msomaji kwenye  Jedwali linalohusika.</p> <p><b>Tatizo</b>  <b>Jedwali la Tano</b>  linarejea kuanzishwa  chini ya <b>Kifungu cha 52</b> ambacho  maudhui yake  hayahusiani <b>Jedwali</b>  hilo.</p>	<p>7. Marekebisho  yafanyike kwenye  sheria ndogo hii  kwa kuainisha  kifungu  kinachoanzisha  hati/Jedwali husika  la kukiri kosa.</p>
12.	<b>(TS Na. 376) 27/05/2022</b>	Sheria Ndogo za Ada na	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa,	Ofisi ya Rais TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungu cha 6 (6)</b>  kimetumia neno</p>	<p>1. Marekebisho  yafanyike katika</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
		Ushuru za Halmashauri ya Wilaya Ya Songea, 2022	(Sura ya 290)  (Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))		<p>"afisa masuuli". kuwa ndiye atakayetoea idhini ya kukamata na kuuza bidhaa au mali iliyokamatwa.</p> <p><b>Tatizo</b> Neno "afisa masuuli" ni mamlaka ya Mkurugenzi wa Halmashauri katika masuala ya fedha na si jina la cheo kinachotambuliwa kwa mujibu wa Sheria.</p> <p>2. <b>Sehemu T ya Jedwali la Kwanza</b> inabainisha viwango ushuru wa maegesho magari yanayobeba makaa ya mawe katika maeneo ya</p>	<p>Sheria Ndogo hii kwa kufuta neno "afisa masuuli" na badala yake kuandika neno Mkurugenzi ili kuondoa mkanganyiko kati ya mamlaka na cheo cha ukurugnzi kinachotambulika kisheria</p> <p>2. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kubainisha muda wa ulipaji wa viwango vya ushuru na uzito wa</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>halmashauri kwa mchanauo ufuatao:-</p> <p>(i) Kuanzia tani 1 hadi tani 10 shilingi 1,000/-; na</p> <p>(ii) Tani 10 nakuendelea shilingi 30,000/-.</p> <p><b><u>Tatizo kwanza</u></b></p> <p>Sheria ndogo haijabainisha iwapo viwango vya ushuru vitalipwa kwa siku au kwa kuegesha gari kwa mara moja au vinginevyo.</p> <p>Kutobainishwa wa muda mahsus wa malipo ya ushuru huo kunaweza kusababisha utozaji usiokuwa na</p>	<p>gari ili kuondoa mkanganyiko utakaoleta changamoto katika utekelezaji wa sheria hii.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>muongozo.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Gari lenye uzito wa tani kumi linatajwa katika ushuru wa shilingi 1000/- halikadhalika katika ushuru wa shilingi 30,000/-. Hali inaweza kuleta mkanganyiko wakati wa utekelezaji kuhusu ulipaji wa ushuru wa Gari lenye uzito wa tani 10.</p>	
13.	<b>(TS Na. 480) 8/07/2022</b>	Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, 2022	Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura ya 290)  (Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1)	Ofisi ya Rais TAMISEMI	<b>Sehemu (c) (ii) ya Jedwali la Kwanza</b> imeainisha viwango vya ada za kusaifirisha mifugo kwa mchanganuo ufuatao:- (i) Kusafirisha Mbuzi nje ya Halmashauri shilingi 1500/-;	Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kubainisha idadi ya mifugo Iliyokusudiwa kutozwa ili kuweza kupata muongozo wa namna ya utozaji ushuru kwa usafirishaji

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>(ii) Kusafirisha nguruwe nje ya Halmashauri shilingi 1500/-;</p> <p>(iii) Kusafirisha kuku/bata/kanga wakubwa nje ya Halmashauri shilingi 200/-; na</p> <p>(iv) Kusafirisha vifaranga vyatatu kuku/bata/kanga shilingi 1,000/-.</p> <p><b><u>Tatizo la kwanza</u></b></p> <p>Viwango vyatatu ada vilivyoainishwa havijaonesha iwapo vimekusudiwa kutozwa kwa mfugo mmoja mmoja au kwa idadi yoyote ya mifugo itakayosafirishwa nje ya Halmashauri.</p>	<p>wa mifugo.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>Kutowelwa vema kwa namna ya ulipaji wa ada hizo kunasababisha kukosekana kwa muongozo wa utozaji, hali inayoweza kupunguza mapato ya halmashauri yatokanayo na ada ya mifugo inayohusika.</p> <p><b><u>Tatizo la pili</u></b></p> <p>Uwezekano wa kukosekana kwa uhalisia wa namna ya ulipaji wa wa ada ya kusafirisha mifugo ndani ya Halmashauri</p>	
<b>SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA TISA WA BUNGE</b>						
14.	(TS Na. 559)  16/9/2022	The Banking and Financial Institutions (Mortgage	The Banking and Financial Institution Act (2006)	Wizara ya Fedha na Mipango	1. <b>Kanuni ya 6(3)(b)</b> inaweka kiwango cha ada ya usajili ya shilingi milioni tano au	1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa mwanya wa Benki Kuu

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
		Refinance Companies) Regulations, 2022			<p>kiwango kingine kitakachoamuliwa na Benki Kuu, kwa mtu anayetaka kuanza biashara ya mortgage re – financing.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b>            Kanuni imetoa mwanya kwa Benki Kuu kutoza ada ya usajili inayoweza kuzidi au kupungua. Kiasi hicho kilichotajwa hakifafanui ukomo wa chini wala wa juu. Hali hiyo inaweza kusababisha kutoeleweka kwa ada halisi ya usajili, uwezekano wa uwepo wa viwango</p>	kutoza ada ya usajili inayoweza kuzidi au kupungua

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>mbalimbali vya ada ya usajili na kuleta mkanganyiko kwa watekelezaji wa kanuni hizi.</p> <p>2. <b>Kanuni ya 10(1)(2)</b> inaweka vigezo na uzoefu wa Wajumbe watakaopendekezw a kuwa katika Bodi ya Wakurugenzi.</p> <p><b>Tatizo</b> Kanuni haioneshi endapo hatua inatakayochukuliwa na Benki Kuu ikiwa Mjumbe aliyependekezwa atakosa sifa zilizotajwa kwa mujibu wa Kanuni</p>	<p>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka utaratibu wa kikanuni utakaofuatwa baada ya Benki Kuu kutoridhishwa na sifa za mjumbe/wajumbe watakaopendekez wa na kampuni kuwa sehemu ya Bodi ya Wakurugenzi.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>3. <b>Kanuni ya 31</b> inaonesha uwezo wa Benki kuu kutoa adhabu mbalimbali inapotokea masharti ya Kanuni hizi yamevunjwa. Masharti hayo yametajwa katika aya ya (c), (d), (e), (f) na (g) ambayo ni kuzuiwa kwa muda kupata huduma za mikopo kutoka Benki Kuu, (<i>Suspension of capital expenditure</i>), fursa ya kutoa mikopo na kuzuia kwa muda mkurugenzi, afisa au mwajiriwa aliyekiye masharti ya kanuni hizi asitekeleze</p>	<p>3. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka ukomo wa zui o la muda pamoja na mazingira yatakayopelekea kusitishwa na adhabu.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>majukumu yaliyoainishwa chini ya Kanuni hizi.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b></p> <p>Kanuni hazioneshi ukomo wa ukomo wa muda wa zuio na wala hazioneshi mazingira yanayoweza kuruhusu wahusika au kampuni kuendelea na majukumu au kazi ikiwa marekebisho au maboresho yatafanyika kuondoa kasoro zilizosababisha kuwekwa kwa zuio la muda.</p> <p>Hali hiyo inaweza kutatiza uzingatiaji wa misingi ya haki kwa kampuni au wahusika</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>waliosahihisha kasoro au dosari hizo.</p> <p>4. <b>Jedwali la Tatu</b>  linataja sifa na uzoefu za Wajumbe wanotakiwa kuwa katika Bodi ya Wakurugenzi.</p> <p><b>Tatizo la kwanza</b>  Kipengele cha 1 (b) kinataja sifa mojawapo kuwa wasifu wa jumla wa mjambe au Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi bila kuhusisha taaluma ya wajumbe hao.  Hali hii inaweza kuleta mkanganyiko wakati wa utekelezaji hususan katika</p>	<p>4. <b>Jedwali la Tatu</b>  lifanyiwe marekebisho katika:-  (i) kipengele cha 1  (b) kwa kuonesha kuwa wasifu wa mjambe utakaozingatiw a na Benki Kuu utakua ni ule Uliotokana na taaluma ya mjambe huyo; na</p> <p>(ii) Jedwali la tatu la Kanuni lifanyiwe marekebisho</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>upimaji wa wasifu wa jumla wa mjambe au wajumbe waliopendekezwa.</p> <p><b><u>Tatizo la Pili</u></b></p> <p>Kipengele cha Tatu cha Jedwali kinaipa mamlaka Benki Kuu kuweka vigezo vingine vyovyote itakavyoona inafaa. Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika bayana kwa vigezo vinavyohusika, hivyo kuleta mkanganyiko mionganoni mwa walengwa.</p>	<p>kwa kwa kuondoa kipengele cha tatu kinachoipa Mamlaka Benki kuu kuongeza vigezo vingine vyovyote itakavyoona vinafaa.</p>
15.	(TS Na.560)  16/9/2022	Sheria Ndogo za Ada na Vibali vya Burudani za	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	<p>1. Kanuni hizi zinaonesha kuwa zimetungwa kwa mujibu wa <b>Kifungu</b></p>	<p>1. Marekebisho yafanyike kwa kuongeza <b>kifungu cha 68</b> cha sheria</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
		Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022	(Sura ya 290)  Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)		<p><b>cha 7(1)</b> cha Sheria Mama. Kifungu hicho hakioneshi lolote kuhusu mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni hizi.</p> <p><b>Tatizo</b> Uwekaji wa kifungu wezeshi kisichohusika unakiuka matakwa yaliyowekwa na sheria ya utafsiri wa sheria inayoelekeza kuwa sheria au kifungu kinachorejewa kujitosheleza kimadhumuni. Hali hii inaweza kuleta mashaka juu wa uhalali wa kanuni hizi.</p>	mama kinachotoa mamlaka kwa Waziri kutunga Sheria Ndogo hizi.

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>2. <b>Kifungu cha 4(4)</b> ya Sheria Ndogo hizi kinaweka utaratibu wa kuwasilisha Nakala ya kibali cha kufanya burudani katika eneo la halmashauri kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ikiwa na viambatisho vyote vinavyohusika</p> <p><b>Tatizo</b>  Sheria Ndogo hii haijataja viambatisho vinavyotakiwa kuwasilishwa pamoja na nakala kwa mkuu wa polisi wa Wilaya. Kushindwa kutaja aina ya viambatisho vinavyotakiwa kuwasilishwa pamoja</p>	2. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii ili kubainisha viambatisho vilivvolengwa ili kuondoa usumbufo kwa wananchi katika kutimiza takwa hili.

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>na kibali hiko kunaweza kusababisha usumbu kwa wananchi katika kutimiza takwa hili.</p> <p>3. <b>Kanuni ya 8</b> inatoa wajibu kwa mtu yeyote au kikundi cha watu kinachotaka kufanya sherehe kwa kufunga barabara katika mtaa, kuomba na kupewa kibali cha kufunga barabara inayohusika.</p> <p><b>Tatizo</b> Tofauti na vibali vingine ndani ya kanuni hizi, maombi ya kibali cha kufunga</p>	<p>3. Sheria ndogo ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza fomu maalum ya maombi ya kibali cha kufanya sherehe kwa kufunga barabara katika mtaa.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>barabara hayajawekewa utaratibu wa kuwa na fomu maalumu pamoja na gharama zake.</p> <p>Hali hii inasababisha kuto kukamilika kwa kanuni hii na kutatiza madhumuni yaliowekwa na sheria mama. Hali inayoleta changamoto wakati wa uombaji wa kibali na malipo ya kibali hicho.</p> <p><b>4. Jedwali la Kwanza</b> linaloonesha kuwa limetokana na <b>Kifungu cha 4(2),</b> linahusu maombi ya burudani/sherehe/m aonesho. Kwa</p>	<p>4. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kufuta rejea ya <b>Kifungu cha 4</b> <b>(2)</b> na kufanya rejea sahihi ya</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>kawaida Kifungu  kinachotajwa  kuanzishwa kwa  Jedwali huwa na  maudhui  yanayomrejesha  msomaji kwenye  Jedwali linalohusika.</p> <p><b>Tatizo</b>  <b>Jedwali la Kwanza</b>  linarejea kuanzishwa  chini ya <b>Kifungu cha</b>  <b>4(2)</b> ambayo  maudhui yake  hayahusiani na  <b>Jedwali</b> hilo.  Urejeajji wa kanuni  isiyoendana  kimaudhui unakiuka  matakwa  yaliyowekwa na  sheria ya utafsiri wa  sheria inayoelekeza</p>	<p>kifungu  kinachoanzisha  Jedwali.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>kuwa sheria au kifungu kinachorejewa kujitosheleza kimadhumuni. Hali hii inaleta ugumu wa kueleweka kwa masharti ya kanuni na utekelezaji wa sheria mama.</p> <p>5. <b>Jedwali la pili</b> la kanuni hizi linaainisha Ada za Burudani/ Sherehe/ Maonesho zitakazotozwa kulingana na viwango vyahalmashauri hii.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>i) <b>Kipengele cha 11,</b> hakitaji muda wa kutoza makusanyo</p>	<p>5. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii ili kubainisha muda wa kutoza makusanyo ya asilimia 10 yatokanayo na bahati nasibu pamoja na kuweka viwango halisi vinavyo akisi uhalisia wa shughuli</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>ya asilimia 10%  yatokanayo na Bahati nasibu.  Kutokubainishwa kwa muda mahsus wa malipo ya ya asilimia 10% kunawenza kusababisha utozaji usiokuwa na mwongozo na usiotabirika, jambo ambalo ni kunyume na kanuni za utekelezaji bora wa sheria.</p> <p>ii) Viwango vya ada ya vibali vya burudani vilivyoainishwa haviakisi uhalsia wa shughuli</p>	zilizokusudiwa.

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					zilizokusudiwa. Hali hii inaweza kusababisha kero kwa walengwa.	
16.	(TS Na. 561)  16/9/2022	Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, (Sura ya 290) Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	<p>1. Sheria Ndogo hizi zinaonesha kuwa zimetungwa kwa mujibu wa <b>Kifungu cha 7(1)</b> cha Sheria Mama. Kifungu hicho hakioneshi lolote kuhusu mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni hizi.</p> <p><b>Tatizo.</b> Uwekaji wa kifungu wezeshi kisichohusika unakiuka matakwa yaliyowekwa na sheria ya utafsiri wa sheria inayoelekeza kuwa sheria au kifungu</p>	<p>1. Marekebisho yafanyike kwa kuongeza <b>kifungu cha 68</b> cha sheria mama kinachotoa mamlaka kwa Waziri kutunga Sheria Ndogo hizi.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>kinachorejewa kujitosheleza kimadhumuni. Hali hii inaweza kuleta mashaka juu wa uhalali wa kanuni hizi.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 4(3)</b> kinaweka masharti kwa Mabasi na daladala zinazojishughulisha na shughuli za usafirishaji wa abiria ndani na nje ya Halmashauri kuanzia safari zake katika vituo vikuu vya mabasi au katika kituo cha daladala na si vinginevyo.</p> <p><b>Tatizo</b> Kanuni hii hajataja kituo mahususi cha</p>	<p>2. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kurekebisha <b>Kifungu cha 4 (3)</b> ili kubainisha kituo mahsusni cha daladala kinachotakiwa kuwa kituo cha kuanzia safari.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>daladala kinachotakiwa kuwa kituo cha kuanzia safari. Hali hii itasababisha Kukosekana kwa mwongozo sahihi katika maeneo ya kuanzia safari na kupelekea mkanganyiko kuhusu kituo kinachohusika na kutozwa kwa ada na ushuru wa stendi.</p> <p>3. <b>Kifungu cha 8</b> kinaweka kosa kutembeza chakula katika eneo la Stendi.</p> <p><b>Tatizo</b> Kifungu hakifafanui ni aina gani au namna ya utembezaji wa</p>	<p>3. Marekebisho yafanyike Katika Sheria Ndogo hii kwa kuondoa Kifungu cha 8 kinachozua wananchi kutembeza chakula eneo la</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					chakula unaokusudiwa. Hali hii inaweza kuleta changamoto ya utekelezaji wa masharti ya Sheria Ndogo hizi.	stendi.
17.	(TS NA. 563) 16/9/2022	Sheria Ndogo za Ada ya Ukusanyaji na Uzoaji Taka za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, (Sura ya 290) Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)	Ofisi ya Rais – TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungu cha 4</b> kinaanzisha Jedwali la Kwanza linalohusu ada/tozo zitakazotozwa kwa ukusanyaji na uzoaji wa taka.</p> <p><b>Tatizo</b> Jedwali hilo linataja viwango vya Tozo na ada zinazotakiwa kutozwa katika kata tano (5) tu kati ya kata kumi na nne (14) za halmashauri hii kama ambavyo</p>	<p>1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hizi ili kujumuisha Kata zote za Halmashauri zinazopaswa kulipa tozo ya ukusanyaji na uzoaji wa taka.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>imeoneshwa kwenye kichwa cha habari cha jedwali.</p> <p>Kwa kutokutaja kata nyingine zinazopatikana ndani ya halmashauri hiyo inamaanisha kwamba kaya ambazo zipo kwenye kata zisizo tajwa haziguswi na tozo/ada zinazohusika.</p> <p>Hali hiyo inaweza kutafsiriwa kama ina kinzana na dhamira ya Bunge ya kuruhusu Sheria Ndogo zinazoweka mfumo sahihi na uliokamilika, wa kukusanya na kusimamia mapato ya ndani ya</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>halmashauri. Aidha inaweza kusababisha hisia za wananchi ndani ya halmashauri moja kuona wanabebeshwa mzigo Zaidi ya sehemu nyingine kutokana na kata nyingine kupendelewa.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 5,</b> inaweka ulazima kwa kila kaya au kila mtu kuwa na chombo cha kutunzia taka ambacho kitakuwa na mfuniko na ukubwa ambao unakubalika na Halmashauri.</p>	<p>2. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hizi kwa kubainisha vipimo na aina ya vyombo vinavyokusudiwa kwa ajili ya kutunzia taka ili kulinda afya ya wananchi.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p><b>Tatizo</b></p> <p>Sheria hizi hazijabainisha ukubwa unaotakiwa kwa chombo cha kuwekea taka, jambo linaloweza kusababisha kutokuelewaka kwa masharti kuhusu chombo cha kuhifadhiwa taka.</p> <p>Hali hii inaweka mkanganyiko katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo. Jambo ambalo halina tija katika utungaji wa sheria.</p> <p>3. <b>Kifungu cha 12</b> kinaweka adhabu ya jumla iwapo mtu atakiuka masharti</p>	<p>3. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kurekebisha</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>yoyote yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Adhabu iliyowekwa inajumuisha makosa ambayo tayari yana adhabu mahsus kwa mujibu wa Sheria Mama na adhabu hizo ni ndogo ikilinganishwa na adhabu iliyopo katika Sheria Ndogo hizi.</p>	<p><b>Kifungu cha 12</b> ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo hayajawekewa adhabu mahsus.</p>
18.	(TS NA. 564) 16/9/2022	Sheria Ndogo za Udhhibit wa Uchimbaji wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, (Sura ya 290) Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungu cha 7(1)</b> inazungumzia kuwa malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi utalipwa kwa kuzingatia uzito wa madini yanayohusika.</p>	<p>1. Kifungu kifanyiwe marekbisho ili kufuta neno “<b>uzito</b>” na badala yake kuandika neno “<b>ujazo</b>” ili kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p><b>Tatizo</b>  <b>Jedwali la Pili</b>  lililotajwa na Kifungu cha 7(1) linaonesha viwango vya ushuru wa madini ya ujenzi kwa kuzingatia ujazo na si uzito.</p> <p>Hali hiyo inaweza kuleta changamoto ya utekelezaji wa masharti ya Sheria Ndogo kuhusu kipimo kinachokusudiwa.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 8(4)</b>  kinaweka sharti kwamba, ikiwa chombo kilichokamatwa kitakaa zaidi ya siku 30 bila mmiliki wake kukichukua, kitauzwa kwa njia ya mnada na baada ya mauzo, Halmashauri itakata fedha za faini na</p>	changamoto wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>ushuru na gharama za ulinzi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, na fedha zitakiao baki baada ya makato atarudishiwa mmiliki wa chombo hicho.</p> <p><b>Tatizo</b>  Sheria Ndogo haioneshi sharti la kupata idhini ya mahakama kabla ya kufanya mnada wa kuza chombo kilichokamatwa. Hali hiyo inaweza kusababisha kuuzwa kwa vyombo vyatatu pasipo kufuata utaratibu wa kisheria. Jambo ambalo litakua kero kwa wananchi.</p>	
19.	(TS NA. 567)	Sheria Ndogo (Ada na	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa,	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	1. <b>Kifungu cha 9 (6) na pamoja na 13 (iii)</b>	1. Sheria Ndogo ifanyiwe

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
	16/9/2022	Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, 2022	(Sura ya 290) Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)		<p>cha Sheria Ndogo hizi kinaondoa/hakitoi uwajibikaji au wajibu wa Halmashauri kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b></p> <p><b>Kifungu cha 9(6)</b></p> <p>kinaiondoa halmashauri katika uwajibikaji kutokana na kupotea kwa mali iliyokamatwa na kushikiliwa na halmashauri hiyo.</p> <p>Kuondoa wajibu wa Halmashauri kwa hasara ambayo</p>	<p>marekebisho kwa kuweka sharti la halmashauri kuwajibika iwapo hasara itatokana na uzembe wakati wa ukusanyaji madeni au mali.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>inaweza kutokea kwa uzembe wa watumishi wake kunaweza kupunguza umakini wa kutokfua utaratibu wa ukamataji na kuleta hasara kwa jamii ambayo ni kero isiyotakiwa.</p> <p>Hili hiyo inaweza kuwakatisha tamaa wananchi katika kufanya shughuli za kiuchumi na hivyo kukiuka lengo la serikali la kuwezesha ustawi wa watu.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 15(1)</b>  kinaweka muda kupakia na kushusha abiria na mizigo stendi.</p>	<p>2. <b>Kifungu cha 15 (1)</b>  kifanyiwe marekebisho ili kuainisha muda uliokusudiwa kwa</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p><b>Tatizo</b></p> <p>Kifungu kimekosa ukamilifu kwa kutokuainisha muda mahsusini wa alfajiri uliokusudiwa.</p> <p>Hali hiyo inaweza kuleta mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa masharti yaliyokusudiwa na Sheria Ndogo hizi.</p> <p>3. <b>Kifungu cha 15(2)</b> kinakataza gari la abiria kuendelea kuwepo stendi baada ya muda uliopangwa.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Sheria Ndogo haijabainisha muda mahsusini uliopangwa</p>	<p>lengo la kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.</p> <p>3. Marekebisho yafanyike katika <b>Kifungu cha 15 (2)</b> kwa kubainisha muda uliopangwa kwa gari kuendelea kuwepo stendi.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>kwa gari kuendelea kuwepo stendi. Athari ya jambo hili ni uwezekano wa mkanganyiko kuhusu kueleweka kwa muda uliopangwa mionganini mwa walengwa wa Sheria Ndogo hizi.</p> <p>4. <b>Jedwali namba xix</b> lililotungwa chini ya <b>kifungu cha 4 (1)</b> na lenye kichwa cha habari "ADA YA KIBALI CA UPIMAJI WA AFYA", orodha ya nne ndani ya jedwali hilo iazungumzia ada ya kibali cha unyunyuziaji wa viatilifu kutolewakwa ghamama ya shilingi</p>	<p>4. Marekebisho yafanyike katika <b>Jedwali namba xix</b> kwa kuandika ghamama ya kibali inayo akisi uhalsia wa hali ya wananchi ambao ndio wanufaika wa zoezi la unyunyiziwaji.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>1,000,000/=</p> <p><b><u>Tatizo</u></b></p> <p>Gharama iliyowekwa kwa kibali husika haiakisi uhalsia wa hali ya wananchi ambaeo ndio wanufaika wakubwa wa zoezi la unyuniyizwaji.</p> <p>Hali hii inaweza kuleta shida katika utimilifu wa sheria hii katika matumizi yake.</p> <p>5. Sheria Ndogo imeweka Majedwali ishirini na tatu yanayoonesha viwango mbalimbali vya ada na ushuru.</p>	<p>5. Sheria Ndogo ifanyiwe marekebisho kwa kupitia upya Majedwali yote ili kuondoa kasoro zilizobainika.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p><b><u>Tatizo</u></b></p> <p>Majedwali yote yana dosari nyingi kama vile:-</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(i) Viwango vya ada kutoakisi uhalisia wa mazingira ya walengwa;</li> <li>(ii) Kukosa mtiririko mzuri mfano, kuchanganya huduma na bidhaa, mpangilio wa namba;</li> <li>(iii) Kutokuainishwa kwa ukomo wa muda wa malipo ya ada na ushuru mbalimbali (mfano iwapo utozaji ni kwa siku, mwezi, wiki au mwaka) na kipimo</li> </ul>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>cha ukubwa wa eneo (Mfano matumizi ya maneno ukumbi mkubwa na ukumbi mdogo).</p> <p>Makosa ya Majedwali katika Sheria Ndogo hizi, yanaweza kuleta changamoto wakati wa utekelezaji na kusababisha kutotimia kwa malengo yaliyokusudiwa.</p>	
20.	(TS NA. 574) 23/9/2022	The Mining (State Participation) Regulations, 2022	The Mining Act Sura 123  Zimetungwa chini ya Kifungu cha 10(4) na 129	Wizara ya Madini	<p>1. <b>Kanuni ya 6(2)</b> inamtaka mtu yeyote mwenye leseni ya kuchimba madini kutoa notisi ya siku tisini tangu tarehe ya kutangazwa kwa Kanuni hizi ili Tume ya</p>	<p>1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza kifungu kitakachonesha adhabu kwa kosa la kushindwa kutoa notisi kwa wakati uliowekwa kikanuni</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>Madini ianzishe mchakato wa makubaliano ya ushirikiano kuiwezesha serikali kuwa na hisa.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b></p> <p>Kanuni haioneshi adhabu kwa kushindwa kutoa notisi kwa wakati uliowekwa kikanuni. Kutokubainishwa kwa adhabu ya kushindwa kutoa notisi kwa wakati uliowekwa kunainyima nguvu kanuni hiyo na kusababisha isiwe na maana yoyote katika kusimamia ushiriki wa Serikali.</p>	ili kuipa nguvu kanuni hiyo.

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>2. Kanuni imerejea kuanzishwa chini ya Kifungu cha 10(4) na kifungu cha 129 cha Sheria Mama.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b>  <b>Kifungu cha 10(4)</b>  kinachorejewa  kuanzisha Kanuni hizi hakipo katika Sheria Mama.  Hali hii inaweza kuleta mashaka juu ya uhalali wa kanuni hizi.</p> <p>3. <b>Kanuni</b> hazijaweka vifungu vya makosa na vifungu vya adhabu vilevile haibainishi sheria au kanuni inayoweza kutumika iwapo masharti ya kanuni</p>	<p>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta kifungu cha 10 (4) kilichorejewa na kanuni hizi kama kifungu wezeshi. Kufutwa kwa kifungu hichi kutaondoa mashaka yatakayoibuka juu ya uhalali wa kanuni hizi.</p> <p>3. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka vifungu vinavyoonesha makosa na adhabu adhabu zitakazotolewa baada ya makosa</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>hizi yatakiukwa.</p> <p>Hali hii inasababisha kanuni hizi kukosa msukumo kwa watumiaji kutekeleza masharti yaliyowekwa na kanuni hizi.</p> <p>Aidha kwa namna zilivyo kanuni hizi zinaweza kutatiza usimamizi wa masharti sahihi yaliyowekwa.</p>	<p>hayo kufanyika ili kuongeza msukumo kwa watumiaji kutekeleza masharti yaliyowekwa na kanuni hizi.</p>
21.	<b>(TS NA. 575)</b>  23/9/2022	The Banking and Financial Institutions (Financial Leasing) Regulations, 2022	The Banking and Financial Institution Act (2006)	Wizara ya Fedha na Mipango	<p>1. Kanuni ya 51(c), (d), (e) na (g) inaonesha uwezo wa Benki kuu kutoa adhabu mbalimbali inapotokea masharti ya Kanuni hizi yamevunjwa.</p> <p>Masharti hayo</p>	<p>1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka ukomo wa zio la muda pamoja na mazingira yatakayopelekea kusitishwa na adhabu.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>yametajwa katika yamevunjwa.</p> <p>Masharti hayo yametajwa katika aya ya (c), (d), (e), na (g) ambayo ni kuzuiwa kwa muda kupata huduma za mikopo kutoka Benki Kuu, (<i>Suspension of capital expenditure</i>), fursa ya kutoa mikopo na kuzuia kwa muda mkurugenzi, afisa au mwajiriwa aliyekiye masharti ya kanuni hizi asitekeleze majukumu yaliyoainishwa chini ya Kanuni hizi.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b> Kanuni hazioni shi</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>ukomo wa muda wa zuio na wala hazioneshi mazingira yanayoweza kuruhusu wahusika au kampuni kuendelea na majukumu au kazi ikiwa marekebisho au maboresho yatafanyika kuondoa kasoro zilizosababisha kuwekwa kwa zuio la muda.</p> <p>Hali hiyo inaweza kutatiza uzingatiaji wa misingi ya haki kwa kampuni au wahusika waliosahihisha kasoro au dosari hizo.</p> <p>2. <b>Kanuni ya 9</b> ya Kanuni hizi, inazungumzia ada ya maombi ya leseni</p>	<p>2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa mwanya wa Benki Kuu</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>yanayotakiwa kuambatana na hundi ya shilingi milioni tano au kiasi chochote kitachoamuliwa na Benki.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b></p> <p>Kanuni imeipa mamlaka Benki kuongeza kiasi chochote mbali na kiwango cha chini cha shilingi milioni tano kilichotajwa.</p> <p>Mamlaka hayo ya matumizi ya utashi kwa Benki yanaodoa mantiki nzima ya uwepo wa kiwango cha chini cha shilingi milioni tano kama ada ya maombi ya</p>	<p>kutoza ada ya usajili inayoweza kuzidi au kupungua</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>leseni.</p> <p>Hali hiyo itapelekea ugumu katika utekelezaji wa takwa hili la kisheia lakini pia ni kinyume na kanuni za uandishi kama ambavyo zimeelekezwa ndani ya Sheria ya Tafsiri za Sheria (Cap 1) ya Tanzania.</p>	
22.	(TS NA. 581)  23/9/2022	The Environmental Management (Control of Ozone Depleting Substances and Hydrofluorocarbons) Regulations, 2022	The Environmental Management Act (No. 20 )	Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira	<p>1. <b>Jedwali la Nne</b>  linalohusu Muundo wa Taarifa ya Nusu Mwaka, limerejea kuanzishwa chini ya Kanuni ya 20(2) na 21 (2).</p> <p><b>Tatizo</b>  Kanuni ya 20(2) inayorejewa haihusiani na Jedwali</p>	<p>1. <b>Jedwali la Nne</b>  lifanyiwe marekebisho kwa kurejea Kanuni sahihi inayolianzisha.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>la Nne.          Urejeaji wa kanuni          isiyoendana          kimaudhui unakiuka          matakwa          yaliyowekwa na          sheria ya utafsiri wa          sheria inayoelekeza          kuwa sheria au          kifungu          kinachorejewa          kujitosheleza          kimadhumuni.</p> <p>Hali hii inaleta ugumu          wa kueleweka kwa          masharti ya kanuni na          utekelezaji wa sheria          mama.</p> <p>2. Kanuni ya 27 (b) kinampa mamlaka Afisa Forodha kukagua na kutambua ikiwa</p>	<p>2. Kanuni ifanyiwe          marekebisho kwa          kuonesha namna          ambavyo Afisa          Forodha atawenza</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>mzigo ulioingizwa nchini una chembechembe za kikemikali zenyе athari kwa Ozoni.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b> Kanuni hazoneshi kwa namna gani Afisa Forodha ataweza kutambua uwepo wa kemikali hiso.</p> <p>3. <b>Jedwali la kwanza</b> la linataja bidhaa zenyе viwango fulani vya kemikali hatarishi kwa Ozoni na haidroflorokaboni.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b> Kipengele cha kwanza kinataja</p>	<p>kutambua uwepo wa kemikali wakati wa ukaguzi wa mizigo inayoingizwa nchini.</p> <p>3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuleta ukamilifu wa maudhui Kipengele cha kwanza kinataja katika neno (Automobile and truck conditioning units) kwa kuongeza</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>(Automobile and truck conditioning units) kikiacha neno Air kabla ya neno Conditioning.</p> <p>Hali hii inaleta mkanganyiko wa kanuni katika kueleweka kwake.</p>	<p>neno "Air" kabla ya neno "Conditioning"</p>
23.	<b>(TS NA. 586)</b>  30/9/2022	Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, 2022	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, (Sura ya 290) Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungu cha 5 (5)</b> cha Sheria Ndogo hizi kinampa uwezo afisa mwidhiniwa kuingia katika jengo lolote na muda wowote kwa lengo la kukusanya ada au Ushuru.</p> <p><b>Tatizo</b> Mamlaka anayopewa afisa muhidhiniwa kuingia katika jengo muda</p>	<p>1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hizi kwa kubainisha muda ambao afisa mwindiniwa anaruhusiwa kuingia katika jengo. Muda unaokusudiwa ni muda wowote ndani ya masaa ya kazi.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>wowote yanaweza kusababisha ukiukwaji wa haki ya msingi ya faragha.</p> <p>Hali hiyo inasababisha kero kwa wananchi wanaowakilishwa na Bunge.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 5(9)</b> cha Sheria Ndogo hizi kinaondoa/hakitoi uwajibikaji au wajibu wa Halmashauri kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri.</p> <p><b>Tatizo</b></p>	<p>2. Sheria Ndogo ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la halmashauri kuwajibika kwa hasara itakayosababishwa na halmashauri kwa mali iliyokamatwa au wakati wa ukusanyaji wa madeni.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p><b>Kifungu cha 5(9)</b></p> <p>kinaiondoa halmashauri katika uwajibikaji kutokana na kupotea kwa mali iliyokamatwa na kushikiliwa na halmashauri hiyo.</p> <p>Kuondoa wajibu wa Halmashauri kwa hasara ambayo inaweza kutokea kwa uzembe wa watumishi wake kunaweza kupunguza umakini wa kutokufuata utaratibu wa ukamataji na kuleta hasara kwa jamii ambayo ni kero isiyotakiwa.</p> <p>Hili hiyo inaweza kuwakatisha tamaa wananchi katika</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					kufanya shughuli za kiuchumi na hivyo kukiuka lengo la serikali la kuwezesha ustawi wa watu.	
24.	(TS NA. 587)  30/9/2022	Sheria Ndogo za (Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, 2022	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, (Sura ya 290) Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungua kinachoweka</b> <b>6</b>  masharti kwa mmiliki/mtunza Hoteli, kuzuia kitanda kimoja kutumika na wageni wawili au zaidi wa jinsia moja.</p> <p><b>Tatizo</b>  Masharti hayo yanaweza kukiuka uhalisia kama vile mahitaji ya mama kutumia kitanda kimoja na mwanae au mama na Watoto wawili wa jinsia tofauti au mtu mzima anayemuuguza mtoto au mtu</p>	1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa ufanuzi zaidi kuhusu wageni wa jinsia moja wanaoruhusiwa kutumia kitanda kimoja kama vile mama na mwanae au mama na Watoto wawili wa jinsia tofauti au mtu mzima anayemuuguza mtoto au mtu

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>wawili wa jinsia tofauti hatakama ni wa jinsia moja.</p> <p>Hali hiyo inaweza kusababisha ugumu katika utekelezaji na uhasama katika wananchi na wasimamizi wa nyumba hizo.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 7(b)</b> kinaweka jukumu kwa kila mmiliki wa hoteli au nyumba ya kulala wageni kuhakikisha kuwa anaweka mahitaji ya msingi kwa wageni.</p> <p><b>Tatizo</b> Kifungu kimeweka jukumu kwa mmiliki</p>	<p>mzima wa jinsia moja lakini ni mgonjwa anayehitaji uangalizi na kuainisha watu wazima wa jinsia moja wasioruhusiwa kutumia kitanda kimoja.</p> <p>2. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii katika <b>Kifungu cha 7(b)</b> ili kubainisha mahitaji ya msingi kwa yanayotakiwa kuwekwa na mmiliki wa hoteli au nyumba ya kulala wageni ili kurahisisha</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>wa hoteli au nyumba ya kulala wageni kuweka mahitaji mengine muhimu kwa wageni pasipo kuyaainisha au kuyataja.</p> <p>Kutoainishwa kwa mahitaji hayo kunweza kusababisha mkanganyiko kwa walengwa kuhusu mahitaji yanayokusudiwa.</p>	<p>utekelezaji wa masharti ya sheria ndogo hizi na kuondoa mkanganyiko wakati wa utekelezaji</p>
25.	(TS NA. 588) 30/9/2022	Sheria Ndogo za (Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, 2022	Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287) (Imetungwa chini ya Kifungu cha 89)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungu cha 3</b> kinatafsiri neno "taka ngumu" kuwa ni kitu chochote ambacho baada ya kukitumia hakina thamani yoyote kwa jamii inayohusika, uwepo katika eneo husika unaweza</p>	<p>1. Tafsiri ya maneno "taka ngumu" ifanyiwe marekebisho ili kuendana tafsiri iliyopo Sheria Usimamizi wa Mazingira.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>kusababisha machukizo ya kiafya na kuhatarisha afya ya jamii.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b></p> <p><b>Kanuni ya 3</b> ya Sheria Ndogo itoa tafsiri isiyojitosheleza ya maneno "taka ngumu" Ikilinganishwa na tafsiri pana ya maneno hayo iliyo katika <b>Kifungu cha 3</b> cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Hali hiyo inaweza kusababisha kutokutimia kwa masharti yanayokusudiwa na Sheria nyingine za nchi.</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>2. <b>Kifungu cha 4(1)</b>  kinaipa halmashauri mamlaka ya kukagua nyumba yoyote, barabara, njia au uchochoro, mfereji wa maji ya mvua au ardhi yoyote katika eneno la halmashauri kwa muda wowote na kuchukua hatua zozote itakazoona zinafaa.</p> <p><b>Tatizo</b>  Sheria Ndogo:-</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(i) Haiweki ukomo wa muda wa halmashauri kukagua maeneo yanayohusika;</li> <li>(ii) Haiweki ukomo wa hatua</li> </ul>	<p>2. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii ili kubainisha ukomo wa muda wa ukagazi na ukomo wa hatua zitakazochukuliwa mara baada ya ukagazi kufanyika.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>zitakazochukuliwa Hali hiyo inaweza kusababisha matumizi mabaya ya mamlaka na kuleta kero kwa wananchi.</p> <p>3. <b>Kifungu cha 17(1)</b> kinaweka sharti kuwa taka zote zitapaswa kuchambuliwa sehemu zinapotoka, katika makundi ya taka zenye madhara na zisizo na madhara.</p> <p><b>Tatizo</b> Kifungu haijaaeleza muhusika anayepaswa kufanya uchambuzi wa taka. Hali hiyo inaweza kuleta mkanganyiko kutika utekelezaji wa</p>	<p>3. Marekebisho yafanyike katika <b>Kifungu cha 17 (1)</b> <b>cha Sheria Ndogo</b> hii kwa kubainisha muhsika anayepaswa kufanya uchambuzi wa taka.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>sharti hili.</p> <p>4. <b>Kifungu cha 20</b>  kinaweka jukumu kwa kila mkazi kuhakikisha kuwa maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama kwa kuyachemsha bila kujali yametoka kwenye chanzo gani.</p> <p><b>Tatizo</b>  Kifungu kimetaja njia moja tu ya kuyafanya maji yawe salama. Hali inayosababisha kutokutambua aina nyingine za kutibu maji ili kuwa salama kwa kunywa.</p>	<p>4. Marekebisho yatafanyika katika <b>Kifungu cha 20</b> kwa kubainisha jukumu la kila mkazi kuhakikisha kuwa maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>5. <b>Kifungu cha 23</b> cha sheria hii kinazungumzia uuza vyakula vilivyopikwa ambapo kinaweka amri ya kuhifadhi vyakula hivyo kwenye sanduku lilitengenezwa kwa mbao safi na kuwekewa kioo ili kuzuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.</p> <p><b>Tatizo</b> Amri ya kuhifadhi vyakula hivyo kwenye sanduku la mbao na kuwekewa kioo inaweza kuleta changamoto hasa katika upatikanaji wa</p>	<p>5. Marekebisho yafanyike katika <b>Kifungu cha 23</b> cha Sheria Ndogo hii kwa kuongeza matumizi ya malighafi nyingine katika kuhifadhia chakula ikiwemo aluminiamu (alminium) na malighafi zingine zinazoweza kupatikana kwa urahisi.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>malighafi ya mbao ambayo kwa sasa kazi yake inaweza kufanywa na malighafi nyingine kama aluminiamu (alminium). Masharti haya yanaleta Hii inaweza leta changamoto kwa wafanyabiashara wa vyakula kutokana na kulazimika kutumia malighafi ya mbao kwa gharama za juu ilihali kuna uwezekano wa kutumia malighafi nyingine kwa madhumuni hayo. Hivyo kuwakera wananchi katika shughuli zao za ustawi wa Maisha.</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>6. Kifungu cha 40 (1) kinaweka kosa kwa mtu yoyote kufuga mifugo wa aina yoyote bila kuwa na kibali cha halmashauri.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kifungu hakijaonesha sharti la idadi ya mifugo inayopaswa kuombewa kibali cha halmashauri. Kutokuoneshwa kwa idadi ya mifgo kunaleta ugumu katika utekelezaji kwa watumiaji wa Sheria Ndogo hizi,</p>	<p>6. Marekebisho yafanyike katika <b>Kifungu cha 40 (1)</b> cha Sheria ndogo hii kwa kuonyesha sharti la idadi ya mifugo inayopaswa kuombewa kibali cha Halmashauri.</p>
26.	(TS NA. 589) 30/9/2022	Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, (Sura ya 290) Zimetungwa chini	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	<b>Kifungu cha 10 (2)</b> cha sheria hii kinazungumzia fomu maalum ya kibali cha ununuzi wa Mazao.	Marekebisho yafanyike kwa kuongeza Nyongeza ya fomu maalum ya

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
		Wilaya Nsimbo, 2022	ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)		<p><b>Tatizo</b></p> <p>Fomu maalum inayotajwa na kifungu hiki haijawekwa ndani ya sheria hizi.</p> <p>Hali hii inasababisha kutokukamilika kwa Sheria hii na kutatiza madhumuni yaliowekwa na sheria mama.</p>	maombi ya kibali cha ununuzi wa mazao.
27.	(TS NA. 590) 30/9/2022	Sheria Ndogo (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, 2022	Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287) (Imetungwa chini ya kifungu cha 153)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungu cha 7</b> cha sheria kinampa uwezo afisa mwidhiniwa kuingia katika nyumba au jengo lolote kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Mamlaka anayopewa afisa muhidhiniwa kuingia</p>	<p>1. Marekebisho yafanyike katika <b>Kifungu cha 7</b> cha Sheria Ndogo hii ili kubainisha ukomo wa muda wa ukaguzi unaofanywa na afisa mwidhiniwa kufanyika muda wa saa za kazi.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>katika jengo muda wowote yanaweza kusababisha ukiukwaji wa haki ya msingi ya faragha.</p> <p>Hali hiyo inasababisha kero kwa wananchi wanaowakilishwa na Bunge.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 9(2)</b> kimeweuka katazo la kuchinja mifugo mahali ambapo si machinjio. Aidha, kimeweuka gharama za machinjio.</p> <p><b>Tatizo</b> Kifungu: (i) Kimeweuka ada ya machinjio kwa mbuzi na</p>	<p>2. Sheria ndogo ifanyiwe marekebisho ili kuweka Jedwali litakaloainisha viwango vya ada ya machinjio na kuongeza idadi ya mifugo inayokusudiwa.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>ng'ombe pekee; na</p> <p>(ii) Kimeweke ada ya machinjio badala ya kuweka katika Jedwali.</p>	
28.	<b>(TS NA. 591)</b> 30/9/2022	Sheria Ndogo (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, 2022	Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287) (Imetungwa chini ya kifungu cha 153)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	<p>1. <b>Kifungu cha 6(5)</b> kinatoa wajibu kwa dereva na mmiliki wa chombo cha usafiri kuweka chombo cha kutupia taka ndani ya gari na kuhakikisha zinatupwa katika sehemu maalumu iliyotengwa na halmashauri.</p> <p><b>Tatizo</b> Kifungu kimeweke wajibu wa jumla kwa mmiliki na dereva pasipo kutenganisha</p>	<p>1. Kifungu kifanyiwe marekebisho ili kutenganisha wajibu wa dereva na mmiliki wa gari kuwajibika na kosa linalotokana na kutoweka chombo cha kutupa taka ndani ya gari.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>wajibu huo. Hali hiyo inaweza kusababisha mmiliki kuwajibika kwa kosa lililotendwa na dereva.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 14</b> cha sheria hizi kinazungumzia wajibu na jukumu la afisa mwidhiniwa wa halmashauri ikiwemo jukumu la ukaguzi wa majengo au maeneo.</p> <p><b>Tatizo</b> Katika Kifungu hicho, afisa mwidhiniwa amepewa mamlaka ya kuingia eneo lolote wakati wowote bila kuwekewa kikomo cha muda wa</p>	<p>2. Marekebisho yafanyike katika Kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo hii ili kuweka ukomo wa muda wa ukaguzi unaofanywa na afisa mwidhiniwa. Sheria ndogo itasisitiza Ukaguzi huo kufanyika wakati wa saa za kazi ili kulinda haki ya msingi ya faragha.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>kutimiza jukumu hilo.  Mamlaka  anayopewa afisa  muhidhiniwa kuingia  katika jengo muda  wowote yanaweza  kusababisha ukiukwaji  wa haki ya msingi ya  faragha.</p> <p>Hali hiyo  inasababisha kero  kwa wananchi  wanaowakilishwa na  Bunge.</p> <p>3. <b>Kifungu cha 20(1)</b>  kinaweka sharti kwa  wauza vyakula katika  magenge, jengo  lolote la chakula au  vinywaji kupimwa  afya zao mara moja  kila mwezi na kuwa  na sare wakati wote</p>	<p>3. Marekebisho  yafanyike katika  <b>Kifungu cha 20 (1)</b>  <b>cha Sheria Ndogo</b>  kwa kubadilisha  muda wa upimaji  wa afya kutoka  kila mwezi na  kuwa kila baada</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>akiwa kazini.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kifungu kimeweke sharti la upimaji wa afya kila mwezi. Hali inaweza kuchochea kero kwa walengwa.</p> <p>4. <b>Kifungu cha 21 (2)</b> kinatoa sharti kwa kila mmiliki wa Nyumba kuweka madirisha yasiyopungua 1/8 ya ukubwa wa chumba.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Kipimo kilichowekwa cha 1/8 ya ukubwa wa chumba kinakinzana na vipimo vyta kawaida vyta ukubwa wa madirisha ambavyo</p>	<p>ya miezi sita.</p> <p>4. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kuweka vipimo sahihi vyta uwiano wa madirisha kwa ukuta au sakafu.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>hutegemea ukubwa wa ukuta ama ukubwa wa sakafu.</p> <p>5. <b>Kifungu cha 22 (6)</b>          cha sheria hii kinaorodhesha makosa mbalimbali ambayo yataadhibiwa ndani ya sheria hiyo. Kifungu kidogo cha sita cha kifungu 22 (6) kinataja kosa kwa mtu yejote kuuza vyakula kwa kubeba katika ndoo, sufuria au beseni hata kama vimefunikwa.</p> <p><b>Tatizo</b>          Sheria hii haijaweka mwongozzo wa vibebeo ambavyo</p>	<p>5. Marekebisho yafanyike katika <b>Kifungu cha 22 (6)</b> cha Sheria Ndogo hii kwa kuweka bayana mwongozo wa aina ya vibebeo vinavyoruhusiwa kutumika kwa ajili ya kubeba vyakula nya kuuza.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					halmashauri inaruhusu kutumika. Hali hii inaleta utata kuhusu vyombo vingine Zaidi ya kabati vilivyotajwa katika kifungu cha 22(1), na hivyo kusababisha ugumu wa utekelezaji wa sheria.	
29.	<b>(TS NA. 605)</b> 21/10/2022	Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, 2022	Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), (Sura ya 287) (Imetungwa chini ya kifungu cha 153)	Ofisi ya Rais - TAMISEMI	<p>1. Kifungu cha Tatu kinatoa Tafsiri ya neno "Taka ngumu"</p> <p><b>Tatizo</b> Tafsiri iliyowekwa kwenye kanuni hii inatofautiana na Tafsiri iliyopo kwenye sheria ya usimamizi wa Mazingira.</p>	<p>1. Tafsiri ya maneno "taka ngumu" ifanyiwe marekebisho ili kuendana tafsiri iliyopo Sheria Usimamizi wa Mazingira.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>2. <b>Kifungu cha 8 (2)</b>          kinaeleza kwamba itakuwa ni kosa kwa mwenye basi au dereva au kondakta iwapo abiria aliyeko ndani ya basi lake atatupa kitu chochote barabarani au stendi. Aidha <b>kifungu kidogo cha 3</b> kinaeleza kuwa Mwenye basi au dereva au kondakta atawaijibika kulipa faini ya shilingi elfu hamsini baada ya kujaziwa fomu ya ilani na afisa muidhiniwa wa Mji endapo abiria aliyeko ndani ya gari lake atatupa uchafu</p> <p>2. Marekebisho yafanyike ili kuweka adhabu kwa abiria aliyeko ndani atakayetupa taka au kitu chochote stendi au barabarani badala ya mwenye basi au dereva. Aidha sheria ndogo itaweka wajibu wa Kondakta au Dereva kuhakikisha anaweka chombo ndani ya gari cha abiria kutupa taka na kuwapatia elimu abiria ya umhimu wa kutupa taka kwenye chombo hicho.</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>katika barabara au kituo cha mabasi.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b></p> <p>Kifungu hiki kinawapa adhabu watu kwa makosa ya wengine. Wanaoadhibiwa hawana namna ya kumzuia mkosaji halisi na wala sio waliomshawishi mkosaji kutenda kosa.</p> <p>Hali hiyo haizuii kosa kurudiwa na mfanyaji wa kosa wala mtu mwingine kwasababu atakayeadhibiwa siye mtenda kosa.</p> <p>3. <b>Kifungu cha 22 (2)</b> kinaweka adhabu ya</p>	<p>3. Marekebisho yafanyike kwa</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>jumla kwa mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hizi ambapo kinatamka Mtu atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo hizi atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichozidi shilingi laki mbili au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Adhabu iliyotolewa na kifungu hicho inatofautiana na adhabu ya jumla ilio katika kifungu cha 36(1) ambayo ni faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi</p>	<p>kuweka kifungu kimoja tu chenye adhabu ya jumla.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>sita au vyote kwa pamoja. Hali hii inaleta mkanganyiko kuhusu adhabu ya jumla iliyokusudiwa na Sheria Ndogo hizi.</p> <p>4. <b>Kifungu cha 39 (3)</b> kinatoa sharti kwa kila mmiliki wa Nyumba kuweka madirisha yasiyopungua 1/8 ya ukubwa wa chumba.</p> <p><b>Tatizo</b> Kipimo kilichowekwa cha 1/8 ya ukubwa wa chumba kinakinzana na vipimo vyta kawaida vyta ukubwa wa madirisha ambavyo hutegemea ukubwa</p>	<p>4. Marekebisho yafanyike kwa kuweka sharti la mmiliki wa nyumba kutumia vipimo vyta madirisha kutegemeana na ukubwa wa ukuta ama sakafu.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>wa ukuta ama ukubwa wa sakafu.</p> <p>5. <b>Kifungu cha 40 (ii)</b>  kinazungumzia muda uliopangwa kwa siku ya usafi ya jumamosi ya mwisho wa mwezi na kutaja muda wa kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka saa 4:00 asubuhi na kuweka sitisho la shughuli ye yeyote kufanyika ndani ya muda huo.</p> <p><b>Tatizo</b>  Muda uliotengwa kwa shughuli za usafi katika jumamosi ya mwisho wa mwezi na kuweka zuio la shughuli zote za</p>	<p>5. Marekebisho yafanyike katika <b>Kifungu cha 40 (ii)</b> cha Sheria Ndogo hii kwa kuweka masharti ya kushiriki katika shughuli za usafi pasipo kuathiri shughuli za kijamii na kiuchumi siku ya usafi.</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>kijamii na kiuchumi ni muda mrefu.  Hali hii itaathiri uendeshaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi kwa kiwango cha kuwa kero kwa wananchi.</p> <p>6. <b>Jedwali la Kwanza</b>  linahusu ada za huduma za usafi na uzoaji taka.</p> <p><b>Tatizo</b>  Jedwali lina makosa katika:-</p> <p>(i) <b>Kipengele cha 9</b>  kimetaja  mitandao kwa majina na kuacha  mitandao  mingine;</p> <p>(ii) Mpangilio wa</p>	<p>6. Sheria Ndogo ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari zilizobainishwa.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>namba za vipengele vy a majedwali hazina mtiririko;</p> <p>(iii) <b>Kipengele cha 39</b> kwa kuweka gharama zisizoakisi uhalsia wa shughuli zinazotekelizwa;n a</p> <p>(iv) <b>Kipengele cha 42</b> haina maelezo yoyote kuhusu kiwango cha ada. Dosari himo zinaweza kusababisha mkanganyiko wa usomaji na utekelezaji wa Sheria Ndogo.</p>	
30.	<b>(TS NA. 606)</b>	Sheria Ndogo (Ushuru wa Madini ya	Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura ya 290).	Ofisi ya Raisi TAMISEMI.	<p>1. <b>Kifungu cha 4(1)</b> kinatoa wajibu kwa mtu anayekusudia</p>	<p>1. <b>Kifungu cha 4(1)</b> kifanyiwe marekebisho kwa</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
		Ujenzi na Shughuli za madini ya vitu) za Halmashauri ya wilaya ya Misungwi 2022.	Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1).		<p>kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la halmashauri kutoa taarifa kwa halmashauri ili eneo hilo likaguliwe.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b>  Sheria hiyo imetumia "<b>utaenda kinyume</b>". Maneno hayo hayaleti maana iliyokusudiwa na Kifungu hiki.</p> <p>2. <b>Kifungu cha 6(1)</b>  kimefanya rejea ya Jedwali la Pili linalohusu viwango vya ushuru wa kusafirisha madini ya ujenzi.</p>	<p>kuondoa maneno "<b>utaenda kinyume</b>" na badala yake kuweka maneno yenye maana iliyokusudiwa na Kifungu hiki.</p> <p>2. Marekebisho yafanyike katika Kifungu cha 6 (2) kwa kuweka Jedwali la Pili lenye kuonesha viwango vya ushuru wa kusafirishia madini</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p><b>Tatizo</b></p> <p>Jedwali la Pili linalorejewa halipo katika Sheria Ndogo hizi.</p> <p>Kutokuwepo kwa Jedwali hili kunaondoa ukamilifu wa Sheria Ndogo, hali inayoweza kuathiri malengo yaliyokusudiwa.</p> <p>3. Sheria Ndogo hizi hizi zinaonesha kuwa zimetungwa kwa mujibu wa <b>Kifungu cha 7(1)</b> cha Sheria Mama. Kifungu hicho hakioneshi lolote kuhusu mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni hizi.</p>	<p>ya ujenzi.</p> <p>3. Marekebisho yafanyike kwa kuongeza <b>kifungu cha 68</b> cha sheria mama kinachotoa mamlaka kwa Waziri kutunga Sheria Ndogo hizi.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p><b>Tatizo.</b></p> <p>Uwekaji wa kifungu wezeshi kisichohusika unakiuka matakwa yaliyowekwa na sheria ya utafsiri wa sheria inayoelekeza kuwa sheria au kifungu kinachorejewa kujitosheleza kimadhumuni.</p> <p>Hali hii inaweza kuleta mashaka juu wa uhalali wa kanuni hizi.</p> <p>4. <b>Jedwali Kwanza B</b> linahusu ada ya kibali cha kuchimba madini.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Jedwali halijaonesha viwango vya ada</p>	<p>4. Jedwali lifanyiwe marekebisho katika Jedwali ili kuonesha muda wa ulipaji wa viwango na utaratibu wa ulipaji wake.</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					vitalipwa kwa muda gani au utaratibu upi (Siku, Mwezi, Mwaka au kwa tripu). Kutokuainishwa kwa muda au utaratibu wa utozaji kunaweza kusababisha utozaji wa ada usio na muongozo.	
31.	(TS NA. 636)  28/10/2022	The Environmental Management (Control and Management Of Carbon Trading) Regulations, 2022	The Environment Magement Act, 2004	Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira	<p>1. Kanuni inarejea kuanzishwa chini ya <b>Kifungu cha 75 na Kifungu namba 230(2)</b> cha Sheria Mama.  <u><b>Tatizo</b></u>  <b>Kifungu cha 230(2) na 75</b> vinavyorejewa kama vifungu wezeshi havihuiani na mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni, badala yake vinahusu mambo</p>	<p>1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta rejea ya Kifungu cha 75 na 230(2) na badala yake kurejea Kifungu cha 230(1).</p>

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>mengine mangineyo ambayo Waziri atayatungia Kanuni na hatua za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa. Katika uandishi wa Sheria Ndogo, rejea ya kifungu wezeshi inaonesha chimbuko lamadaraka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo hiyo. Changamoto ya kuweka rejea kifungu cha 75 ambayo haihusiani na mamlaka ya utungwaji wake inaweza kusababisha mashaka kuhusu uhalali wa Sheria Ndogo hiyo.</p>	

<b>Na</b>	<b>Tangazo la Serikali</b>	<b>Jina la Sheria Ndogo</b>	<b>Sheria inayotoa madaraka</b>	<b>Mamlaka inayohusika</b>	<b>Yatokanayo na Uchambuzi</b>	<b>Maoni</b>
					<p>2. Fomu C katika Jedwali la Kwanza linahusu maombi ya biashara ya kaboni.</p> <p><b><u>Tatizo</u></b></p> <p>Imeweka viwango fedha za kimarekani kwa thamani ya milioni. Hali inayoashiria waombaji wote, kuwa watatakiwa kujaza viwango vya mradi vilivyo na thamani ya milioni, hivyo kutotambua waombaji ambao miradi yao hajifikia thamani hiyo.</p> <p>3. <b>Jedwali la Pili</b> linahusu viwango ada na ghamama ya maombi</p>	<p>2. Fomu C ifanyiwe marekebisho kwa kufuta viwango vya dola vyenye thamani ya milioni vilivyoandikwa ndani ya fomu na badala yake ioneshe malipo yatakuwa kwa dola za marekani pasipo kuonesha thamani ya mradi.</p> <p>3. Jedwali la Pili lifanyiwe marekebisho kwa</p>

Na	Tangazo la Serikali	Jina la Sheria Ndogo	Sheria inayotoa madaraka	Mamlaka inayohusika	Yatokanayo na Uchambuzi	Maoni
					<p>ya kusajili wazo la mradi.</p> <p><b>Tatizo</b></p> <p>Viwango vya ada maombi ya usajili inayopaswa kulipa na muombaji mzawa imewekwa kwa viwango vya dola za marekani.</p>	<p>kubadilisha viwango vya ada ya maombi ya kusajili mradi kwa raia wa Tanzania kutoka dola za kimarekani na kuwa shilingi za kitanzania.</p>

Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb.

**MWENYEKITI**

**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo**

8 Februari, 2023